**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 19 Julai, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULLO):**

Taarifa ya Amri ya Serikali ya Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo *(The Public Finance Livestock Development Fund] [Establishment) Order, 2007 (G.N. No. 148 of 8$^{th}$ June, 2007).*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania kwa Mwaka 2005/2006 (*The Annual Report and Audited Accounts of Tanzania Wildlife Research Institute (TAWIRI) for the year 2005/2006).*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSI NA WATOTO:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2007/2008.

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2007/2008.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 245

### Tatizo la Mwingiliano wa Mpaka

**MHE. FATMA A. MIKIDADI** aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya mipaka hapa nchini kati ya Mkoa na Mkoa, Wilaya na Wilaya na Jimbo na Jimbo huingiliana hali inayosababisha kiongozi wa maeneo hayo anapofanya ziara eneo lake kulazimika kutembea katika eneo la mtu mwingine kwa mda mrefu kabla hajafika katika eneo lake, kama ilivyo kwenda Masasi ambapo mtu hulazimika kupita Lindi katika vijiji kumi na tano na kijiji cha Namangale Wilayani Lindi lazima upitie Nanganga Mkoani Mtwara; na kwa kuwa, Majimbo yamekuwa makubwa na watu wameongezeka:-

(a) Kwa kuwa, mipaka mingi naamini iliwekwa zamani sana na hailingani na idadi ya watu, na haikuwekwa kitaalam. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuifanyia tathmini mipaka hiyo na kuisawazisha?

(b) Je, upo uwezekano wa kuongeza majimbo kwa kuwa, maeneo mengi kwa sasa yana watu wengi kuliko zamani?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri, nilipenda mtambue kwamba kwa sasa hivi wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu amesafiri kwenda Dar es Salaam kikazi, kiongozi wa Shughuli za Serikali humu Bungeni ni Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib. (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, taratibu za mipaka ya vijiji, Kata na maeneo yote ya kiutawala kuanzia kwenye Halmashauri husika na katika vikao husika vya Wilaya, Mkoa na baadaye kupelekwa kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kwa hatua

zaidi. Lakini kubwa zaidi ni uzingatiaji wa vigezo kwa mujibu wa kanuni na taratibu za nchi. Mipaka ya Lindi iliwekwa mwaka 1930 kwa tangazo la Serikali Na. 13 la tarehe Januari, 1930.

Lakini kutokana na ongezeko la idadi ya watu mipaka mingi imekuwa ikibadilishwa mwaka hadi mwaka. Kwa mfano mwaka 1971 Lindi ilifanywa kuwa Mkoa na kugawanywa katika Wilaya ya Kilwa, Lindi na Nachingwea. Kadhalika mwaka 1975 Wilaya ya Nachingwea iligawanywa kuwa Wilaya ya Nachingwea na Liwale na mipaka iliwekwa upya pia. *(Makofi)*

Mwaka 1995 Wilaya ya Lindi ilizaa Wilaya ya Ruangwa na mipaka ya Wilaya hizo ikawekwa na kutamkwa kisheria kwa *GN. No. 349* ya tarehe 8 Novemba, 1996 ambayo ni makubaliano ya wananchi wa Wilaya zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2006/2007 Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi iliendesha zoezi la kupima vijiji 392 kati ya 440 ambavyo vilikuwa katika Mkoa wa Lindi.

Upimaji ulifanywa kitaalamu na ziliwekwa alama za mawe za mipaka ya vijiji na vijiji, Kata na Kata, Tarafa na Tarafa, Jimbo na Jimbo, Wilaya na Wilaya hadi sasa vijiji 435 kati ya vijiji vyote 440 vya Mkoa wa Lindi vimepimwa na mipaka imeainishwa kati ya kijiji na kijiji. Kwa kufanya hivyo Serikali imekuwa ikiifanyia tathmini mipaka yote na hivyo pia kusawazishwa kitaalamu.

(b) Mheshimiwa Spika, uwezekano wa kuongeza majimbo kutokana na sababu alizozieleza Mheshimiwa Mbunge upo. Lakini utekelezaji wake utazingatia zaidi Sheria, Kanuni na Taratibu za kuanzisha majimbo ya Uchaguzi.

Kwa mfano, kifungu cha 4(2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Mwaka 1985, kinaelekeza kwamba Tume ya Uchaguzi ndiyo yenye mamlaka ya kusimamia shughuli za uchaguzi kwa ujumla, wakati ambapo kifungu cha 74(6)(c) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano kinaipa Tume hiyo jukumu la kuigawa Jamhuri ya Muungano katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi wa Wabunge.

Pia kifungu Na. 75 (4) kinaeleza bayana kwamba Tume inaweza angalau kila baada ya miaka 10 kuchunguza mgawanyo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika majimbo ya Uchaguzi.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini kwa mpango huo huo basi wa kuagiza Tume na kuagiza wanaohusika na mtiririko huo huo wa kugawa Wilaya basi mimi ningeomba sasa hivi ni wakati muafaka wa kupanga mipango na kuigawa Wilaya na Majimbo, kwa sababu sasa hivi watu wameongezeka.

Kwa mfano Kilwa kuna watu 172 wakati wanatakiwa watu 100,000 kwa mpango angalau watu 100,000 kwa kila Wilaya. Nachingwea watu 163 badala ya 100,000, Ruangwa watu 125, Lindi Vijijini watu

**SPIKA:** Swali !!! swali

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshsimiwa Spika, sasa ni wakati muafaka wa kukaa chini na kupanga mipango kugawa tena upya Majimbo, Wilaya na kadhalika.

Ahsante Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Basi Naibu Waziri unaombwa kuigawa nchi nzima kwa majimbo ya watu 100,000 sijui kutakuwa na Wabunge wangapi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa sasa vigezo vyote vya kugawa Majimbo, Wilaya, Mikoa vinapitiwa upya kulingana na mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii na ongezeko la idadi ya watu.

Kwa hiyo, maombi mengi tayari yameshafika kwenye Ofisi zetu na tunayafanyia kazi. Kwa hiyo mpango huo upo, lakini ninachoshauri zaidi kwamba mipango hii iwe inaanzia kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya na kupita kwenye vikao husika ndipo vije katika Ofisi yangu kwa hatua zaidi.

Na. 246

**Uwiano wa Maendeleo Kimkoa/Kiwilaya**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete katika hotuba zake nyingi ameelekeza Serikali kuzidi kupunguza tofauti za Maendeleo zilizopo kati ya Mkoa na Mkoa au kati ya Wilaya na Wilaya ili kuleta uwiano mzuri wa Maendeleo:-

(a) Je, ni hatua gani zimeshachukuliwa na Serikali za kuandaa mipango itakayojibu azma ya Mheshimiwa Rais katika Bajeti ya 2007/2008 na ile ya baadaye?

(b) Kwa kuwa, Mikoa mingi ya pembezoni haina vivutio vya kuwafanya watumishi wapende kwenda Mikoa hiyo, na kwa kuzingatia ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuweka vivutio rasmi maeneo hayo; Je, ni mambo yapi kwa sasa yameandaliwa?

(c) Je, ni nini hatma ya Serikali kujenga nyumba za watumishi kwenye maeneo kama hayo yaliyotajwa katika swali hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIANI) (K.n.y. WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kabla ya kujibu swali la Mhe. Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Nilipokuwa najibu swali Na. 143 la Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mbunge wa Lulindi, nilieleza kuwa Serikali katika kugawa raslimali za Taifa kwa Mikoa mbalimbali inazingatia vigezo vifuatavyo:-

(i) Takwimu rasmi zinazotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Kwa mfano takwimu zinazotokana na: Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka 2002, pato la kimkoa, vifo vya watoto walio chini ya miaka 5 na mtawanyiko wa watu *(population density).*

(ii) Hali ya umaskini kwa ujumla na ukubwa wa eneo (ukiondoa hifadhi za misitu na maeneo ya maziwa) na

(iii) Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 ambayo inaelekeza Serikali kupeleka madaraka kwa wananchi kwa kupeleka rasilimali – fedha, rasilimali watu na nyenzo za kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Paul Kimiti, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali katika bajeti yake 2007/2008 imegawa rasilimali fedha na watu kwa Mikoa yote kwa kuzingatia vigezo nilivyovianisha hapo juu. Kwa kuzingatia vigezo hivyo Serikali itahakikisha kuwa Mikoa na Wilaya zilizokuwa nyuma kimaendeleo zinapata rasilimali zaidi ya Mikoa na Wilaya zilizokuwa na nafuu kwa lengo la kuharakisha Maendeleo katika Mikoa/maeneo hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la mikoa ya pembezoni sio watumishi kutokupenda kwenda huko kwa sababu tu mikoa hiyo iko pembezoni. Bali ni kukosekana kwa miundombinu muhimu kama vile barabara umeme na kuwepo na vivutio kwa watumishi.

Serikali kwa kulijua hili imejitahidi kuanzisha programu mbalimbali zilizokuwa na mwelekeo wa kukuza na kuchochea fursa mbalimbali za maendeleo katika maeneo na mikoa hiyo pamoja na kuendeleza miundombinu muhimu.

Kama nilivyotangulia kusema awali jitihada zote za Serikali za kuondoa umaskini ni kwa nchi nzima na zinazingatia vigezo tulivyojiweka vya kupima Maendeleo.

Kwa sasa vigezo hivyo vinatumika kwa namna nyingine Serikali imeamua kutekeleza programu za kanda za Maendeleo kama vile Mtwara *Development Corridor, Central Corridor* na *Northern Development orridor* na kadhalika kwa lengo la kuchochea maendeleo ya miundombinu katika maeneo na mikoa ambayo, licha ya kuwa na rasilimali nyingi za kimaendeleo, lakini bado iko nyuma.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi pamoja na wahisani wa maendeleo *(Development Partners*) imebuni na kutekeleza miradi mbalimbali ya Maendeleo katika Mikoa mbalimbali hapa nchini ikiwemo Mikoa iliyo pembezoni kwa lengo la kuharakisha ukuaji wa uchumi na kuondoa umaskini.

(c) Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ya kujenga nyumba za watumishi inaendelea na lengo ni kufanya ifanyike kwa mikoa yote ikiwa ni pamoja na maeneo niliyoyataja. Kwa upande mmoja hili linategemea kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2006 Mikoa 18 ya Tanzania Bara ilitembelewa na Bodi ya Wasanifu wa Majengo na Wakandarasi na kukagua sehemu ya majenzi 389. Mikoa hiyo ni pamoja na Rukwa, Ruvuma, Iringa, Mwanza, Kagera, Mara na Shinyanga, Lindi, Mtwara, Morogoro, Dodoma, Pwani, Tanga, Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Dar es Salaam. *(Makofi)*

Aidha, Kitengo cha Mikopo ya Ujenzi wa nyumba kiliidhinisha mikopo 677 kwa ujumla katika Bajeti ya mwaka huu Serikali inategemea kujenga nyumba 100 mikoani ili kukopesha watumishi, na hii inajumuisha mikoa hiyo ya pembezoni. *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI**: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri aliyoyasema, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza kabla ya kuuliza swali nataka nitoe nafasi hii kuwashukuru wenzetu wa Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* kupitia kwako Mheshimiwa Spika kwa kazi nzuri waliyoifanyia nchi hii na kuwa kituo bora duniani. Hiyo ni misingi ambayo uliiweka wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na Ndugu Ole Naiko anaiendeleza, hivyo nawashukuru kwa hilo.

Swali la kwanza, kwa kuwa katika taarifa ya Mwaka 2006, Kituo hiki cha Uwekezaji kiliidhinisha miradi kadhaa Dar es Salaam ikiongoza kwa kuwa na miradi 419 ikifuatiwa na Arusha 111 na Mwanza 40.

Lakini ni mikoa mingine iliidhinishiwa miradi 2 na mradi mmojawapo ambao sisi tunafahamu upande wa Sumbawanga ni mradi wa Mheshimiwa Mzindakaya na mikoa mingine hata mradi mmoja haupo.

Je, katika utaratibu huo huoni ya kwamba vijana wetu wengi sana wataendelea kukimbilia Dar es Salaam na kufanya mji wa Dar es Salaam uwe ni mji ambao huwezi kutawalika kwa urahisi kwa sababu ya wingi wa vijana wanaokwenda kule badala ya kupeleka mikoa mingine?

La pili, kwa sababu katika kipindi kilichopita mwaka 2006 niliomba msaada kutoka Ubalozi fulani ili usaidie Mkoa wa Rukwa kwa mradi ya maji miwili.

Lakini majibu tuliyopewa ya kwamba haitawezekana kutokana na umbali kutoka Makao Makuu hadi Sumbawanga. Maana yake mikoa iliyoko mbali itaendelea kupata matatizo. Swali katika misingi hiyo je azma ya Serikali na Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, Mabalozi na wengine kusaidia mikoa ambayo iko pembeni itawezekana? Kama haitawezekana kwa nini tusitumie?

**SPIKA:** Basi umeeleweka. Swali refu mno. Nadhani umeeleweka.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIANI - K.n.y. WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI):** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kwa niaba ya Waziri wa Mipango nipokee pongezi kwa niaba yake kwa ajili ya pongezi hizo zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kituo hiki cha uwekezaji *(TIC)*.

Aidha, kwa kujibu swali lake la kwanza napenda tu kumhakikishia Mbunge kwamba sasa hivi kituo hiki cha *TIC* kimeanza kuanzisha ofisi katika kanda zetu kwa hivyo utekelezaji wa miradi na uibuaji na upitishaji utakuwa rahisi zaidi kuliko ilivyokuwa hapo nyuma. Kwa hivyo namwomba ajue tu kwamba utaratibu wa kuhakikisha kwamba ufanisi unaboreshwa umezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, suala la pili la Mheshimiwa Mbunge ni kwamba je mikoa iliyoko pembezoni itaendelea kupata matatizo kutokana na kukosa miradi hiyo muhimu kama ya maji. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na hasa kufuatia hitimisho la hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba kwa mwaka huu mikoa yote ambayo tuliainisha kwamba iko pembezoni imepata fedha nyingi zaidi katika Bajeti yake ya Maendeleo.

Naomba tu nitaje kwa mfano Mkoa wa Rukwa ambao mwaka 2006/2007 ulikuwa umepata shilingi bilioni 1,900,400, 000 na mwaka huu umetengewa 11,269,764,000 ili ni ongezeko la zaidi ya elfu moja.

Kwa hivyo namwomba Mheshimiwa Mbunge ajue tu kwamba Serikali inazingatia matatizo yaliyopo katika maeneo hayo na tumepanga mikakati maalum ya kurekebisha.

Na. 247

**Namba za Usajili Kwenye Magari Zanzibar na Tanzania Bara**

**MHE. ALI SAID SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:-

Je, kwa nini magari yenye namba za usajili za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hayaruhusiwi kutembea Tanzania Bara wakati magari yenye namba za usajili wa Tanzania Bara yanaruhusiwa kutembea huko Tanzania Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULLO):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazosimamia uandikishaji wa magari Tanzania Bara na Tanzania Visiwani zinatofautiana. Kwa upande wa Tanzania Bara, uandikishaji wa magari unazingatia Sheria kuu tatu, nazo ni *Road Traffic Act, 1972, Motor Vehicle (Tax on Registration and Transfer) Act, 1972* na *Traffic (Foreign Vehicles) Rules, 1978.*

Jedwali namba 3 la Sheria ya Barabara (*Road Traffic Act, 1973*) limeorodhesha tarakimu za kuandikisha magari zinazotambuliwa kisheria. Namba za kuandikisha magari Zanzibar haziko kwenye orodha hiyo.

Mheshimiwa Spika, magari yenye usajili wa Tanzania Bara yanaruhusiwa kutembea Zanzibar kwa kuwa Sheria za Usajili wa Magari Tanzania Zanzibar zinaruhusu.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaweza kurekebishwa kwa kuhuisha Sheria za pande zote mbili na kuwa Sheria moja itakayosimamia uandikishaji wa magari katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nzima.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu hayo kwa kawaida ya Serikali. Hata hivyo nina masuala mawili.

La kwanza, kwa kuwa suala hili linakuwa linaulizwa katika kila Mkutano wa Bunge hili. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba hili ni miongoni mwa kero mojawapo kubwa ya Muungano?

Swali la pili, kwa kuwa Naibu Waziri kama yeye alipojibu suala hili katika Mkutano huu huu wa Bunge alisema kwamba na kama alivyosema yeye kwamba wanajaribu kupitia sheria ili iwe moja ili hatimaye ipatikane suluhu.

Lakini kwa kuwa mchakato huo unaweza kuchukua miaka miwili au zaidi kabla ya kukamilika.

Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba sasa umefika wakati kuweza kutoa kauli humu Bungeni kwamba wakati tunasubiri mchakato huu ukamilike magari hayo ya Zanzibar yenye *ZNZ* yakaruhusiwa kutumika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULLO):** Mheshimiwa Spika, la kwanza nilisema kuna sheria. Sasa hatuwezi kuvunja sheria. Isipokuwa kama sheria itakuwa imebadilishwa na Bunge hili. Kwa hiyo, kwa Serikali kutoa kauli kabla sheria haijabadilishwa haiwezekani.

La pili, kwa kweli hili sio kero ya Muungano. Tunaweza tukaondoa tatizo hili kwa urahisi kabisa kwa kuamua kuwa na Sheria moja ya kuandikisha magari ya kisasa. Tukiweza kufanya hivyo hata katika muda wa mwezi mmoja hli litakuwa limetoweka.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa ni hivi karibuni kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetoa tamko kusajili magari yote yanayotoka Tanzania Bara hamwoni kwamba huu ni mwanzo wa malumbano kati ya Jamhuri zetu mbili na kwamba iko haja sasa hivi ya kukaa kitako kuanza kuzungumza suala hili ili kuondoa hali hiyo ya wasiwasi ambayo imejitokeza.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULLO):** Mheshimiwa Spika, tumesoma kwenye magazeti kwamba kuna kauli zimetolewa ndani ya Baraza la Wawakilishi, Serikali ya Muungano haijalipata rasmi.

Lakini wakati nikijibu suala la namna hii hii wiki iliyopita tulisema kwamba tatizo hili ni mojawapo ambalo limepelekwa kwenye ile Kamati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi.

Mheshimiwa Spika ni matumaini yangu kwamba kama ni kweli kwamba yale yaliyotamkwa ndani ya Baraza la Wawakilishi basi Waziri Kiongozi atayapeleka katika kikao kile cha Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi. *(Makofi)*

Na. 248

**Usumbufu wa Kupata Malipo ya Uzeeni**

**MHE. MUSSA A. ZUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa Wastaafu wa Serikali wanapata shida sana wakati wa kufuatilia malipo yao ya uzeeni (pensheni); na kwa kuwa hulazimika kukaa kwenye foleni kwa muda mrefu bila mafanikio ikizingatiwa kuwa wastaafu hao ndio hazina ya Taifa letu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia huduma hiyo kwa urahisi na kwa haraka bila usumbufu kama huo wanauopata sasa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Musa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Zungu kuwa Wazee ni hazina kubwa ya Taifa kwa busara zao na kwamba wanahitaji mafunzo kutokana na uwajibikaji wao kwa Taifa wakati walipokuwa wanafanya kazi. Napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwa ujumla kwamba Serikali ina nia ya kuona si Wazee tu, bali wananchi wake wote wanaishi maisha mazuri na yenye furaha.

Mheshimiwa Spika, wengi wa wastaafu wanaofuatilia malipo Hazina wanatoka mikoani. Kwa upande wa Dar es salaam kuna wawakilishi wanaopaswa kufuatilia malipo hayo. Hazina kwa kutambua hilo imechukua hatua mbali mbali kwa lengo la kuwaondolea kero wastaafu kama ifuatavyo:-

(i) Kuanzisha Hazina Ndogo katika Mikoa yote hapa nchini ambazo pamoja na majukumu mengine zina jukumu la kuwahudumia wastaafu huko mikoani. Pia husambaza hundi za mafao ya wastaafu badala ya wastaafu/wategemezi kulazimika kufuatilia Hazina Dar es Salaam.

(ii) Kuwasisitizia waajiri mtindo wa wawakilishi kufuatilia malipo ya wastaafu badala ya wastaafu kuja Hazina kufuata malipo hayo. Maafisa hao wanapofuatilia malipo hayo hupewa orodha ya hundi za wastaafu/miradhi zilizo tayari kulipwa ili waweze kuwajulisha wahusika kuja Hazina kuchukua hundi zao. Wawakilishi hao pia hupewa ufafanuzi wa mwenendo wa majalada na malipo ya wastaafu /miradhi wao ili wawajulishe wahusika.

(iii)Kuandaa mwongozo unaomwelekeza mwajiri mambo anayotakiwa kutekeleza miezi mitatu kabla mstaafu na kuwasilisha Hazina jalada au majalada ya mtumishi yakiwa na nyaraka muhimu ili malipo yaweze kuandaliwa kabla ya tarehe ya kustaafu mtumishi kufika. Aidha, kama nilivyosema tarehe 26/06/2007 wakati najibu swali Na. 93 la Mheshimiwa Degera katika kikao cha 10 cha Mkutano huu wa Bunge lako tukufu. Serikali katika mwaka wa fedha 2007/2008 itafanya mchakato wa kuwahamishia wastaafu wanaolipwa na Hazina kwenye Mifuko ya Pensheni ya *PPF, PSPF, NSSF* na *GEPF* ili kuwaondolea usumbufu.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kupunguza muda wa malipo kutoka mara mbili kwa mwaka, iwe angalau mara nne kwa mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, Serikali imeishapokea mapendekezo ya kupunguza muda kutoka miezi sita hadi miezi mitatu. Hazina inayafanyia kazi mapendekezo haya, ni matumaini yangu kwamba inawezekana mwaka huu tukaanza kuwalipa kwa miezi mitatu badala ya miezi sita.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Swali la kwanza!

**SPIKA:** Ni moja tu!

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna wastaafu waliokupua (Kupata mafao yao kwa mara moja) na baada ya Serikali kuona kwamba wana hali mbaya, waliombwa kurudishwa kwenye orodha, lakini inachukua muda mrefu sana hawajapata hizo pesa; Je, kigezo cha mtu kujaza *form* ya kurudishwa kwenye orodha na kupata pesa inachukua muda gani? Pili, …

**SPIKA:** Swali ni moja tu!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA – MHE. MUSTAFA H. MKULO:** Mheshimiwa Spika, Serikali ni kweli iliamua kuwarudisha wale ambao karatasi zao zote ziko sawa sawa. Inachukua si zaidi ya miezi mitatu kwa mtu kupata pensheni yake.

Lakini, kuna wengine kwa sababu walishalipwa mara moja, wakapoteza kila kitu, sasa inabidi Hazina yenyewe ianze kutafuta *details* za mhusika ili tuweze kuziweka kwenye kompyuta, aingizwe tena kwenye pensheni, ili aweze kulipwa. Kwa hiyo, wanaopata tabu ni wale ambao karatasi zao haziko sawa sawa. Kama karatasi ziko sawa sawa, katika muda wa miezi mitatu mtu anapata pensheni yake.

**SPIKA:** Wheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, nahisi leo ukumbi umepooza sana! Isije ikawa ni kutokana na tangazo langu kuhusu Jumamosi! Yale mambo ya Jumamosi ni ya hiari! Ingawa nilitazamia kama viongozi tutaonyesha mfano! *(Kicheko)*

Na. 249

**Mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa**

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Kwa kuwa Sekta ya Madini inachangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa na wananchi wa maeneo ilipo hiyo migodi wananufaika kwa kiasi kikubwa:-

(a) Je, ni migodi mingapi iliyo katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na inachangia kiasi gani kila mmoja kwenye pato la Taifa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuwashirikisha zaidi Watanzania katika umiliki wa migodi hiyo badala ya kuwaachia wawekezaji wageni kumiliki asilimia mia moja (100%)?

(c) Kwa kuwa baadhi ya kampuni zinapogundua migodi huuza hisa zao katika masoko ya hisa huko *New York, London, Toronto* na kadhalika na kwamba, kinachouzwa ni pamoja na rasilimali iliyopo hapa Tanzania (migodi), je, hadi sasa Serikali imekusanya kodi na ushuru kwa baadhi ya kampuni kama *Kahama Mining*, *Ashanti Goldfield*, *Samax Resources* – Afrika Mashariki kwa kuuza hisa zake?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mikoa ya Kanda ya Ziwa Victoria kuna migodi mikubwa mitano (5) ya dhahabu na mmoja wa almasi. Migodi ya dhahabu ni Mgodi wa Geita uliopo Mwanza, Mgodi wa Bulyanhulu ulioko Mkoani Shinyanga, Mgodi wa Tulawaka ulioko Mkoani Kagera na Mgodi wa *North Mara* na Buhemba iliyoko Mkoani Mara. Mgodi wa Almasi ni wa Mwadui ulioko Mkoani Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, migodi niliyoitaja imechangia katika pato la Taifa kwa kulipia kodi mbali mbali kama ifuatavyo:-

(i) Mgodi wa Geita ulilipa Dola za Marekani 85,784,706 katika kipindi cha 2000 hadi 2006.

(ii) Mgodi wa Bulyanhulu ulilipa Dola za Marekani 81,872,062 katika kipindi cha 2000 hadi 2006;

(iii) Mgodi wa *North* Mara ulilipa Dola za Marekani 29,982,137 katika kipindi cha 1997 hadi 2006;

(iv) Mgodi wa Buhemba ulilipa Dola za Marekani 5,143,617 katika kipindi cha 2002 hadi 2006

(v) Mgodi wa Tulawaka ulilipa Dola za Marekani 15,434,855 katika mwaka 2006 na;

(vi) Mgodi wa Mwadui ulilipa Dola za Marekani 30,368,809 katika kipindi cha 1997 hadi 2006.

(b) Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika sekta ya madini unahitaji mitaji mikubwa. Hali hii imesababisha Watazania kushindwa kushiriki ipasavyo katika umiliki wa migodi mikubwa ya madini. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha mazingira yatakayowawezesha Watanzania kuwekeza fedha zao kwenye migodi mikubwa iliyoko hapa nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kuondoa vikwazo vinavyosababisha kampuni za madini kushindwa kujiandikisha kwenye soko la hisa la Dar es salaam, kuondoa vikwazo vinavyozuia Watanzania kununua hisa kwenye kampuni za madini zilizoandikishwa nje ya nchi na kwa kuwahimiza Watanzania wenye leseni za utafutaji wa madini kufanya utafutaji wa madini wa awali wa maeneo yao ili waweze

kupata wabia wa kuwekeza na kuyaongezea thamani maeneo yao. Aidha, Serikali inapitia upya Sera ya Madini kwa lengo ala kuongeza ushiriki wa Serikali katika umiliki wa migodi kwa njia ya hisa kwa kuzingatia rasilimali na michango ya Serikali katika utafiti wa miundombinu.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria ya ushuru wa stempu ya mwaka 1972 *(Stamp Duty Act, 1972)*, wamiliki wa migodi waliuoza hisa zao katika masoko ya hisa nje ya nchi hawawajibiki kulipa ushuru wa stempu wa mauzo ya hisa yaliyofanyika. Mauzo ya hisa yanayofanywa na kampuni za madini nje ya nchi ni sawa na mauzo ya hisa yanayofanywa na kampuni mbali mbali katika soko la hisa la Dar es salaam ambayo hayatozwi ushuru wa stempu.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kweli amejibu kwa kina na mimi nimefurahi sana. Nina maswali mawili madogo; La kwanza, kwa kuwa wachimbaji wadogo wadogo ndio wagunduzi wa awali wa migodi hii na *once* wakishakuwa wamegundua migodi hii, wanafukuzwa katika maeneo husika; na kwa kuwa baadhi ya wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo kama ya Ngasamo katika Jimbo la Busega sasa hivi wako kwenye heka heka ya kufukuzwa katika maeneo yao ambayo wanafanyia kazi. Je, kwa nini Serikali isiweke utaratibu mzuri wa kuwashirikisha vyema hao wachimbaji wadogo wadogo katika suala zima la migodi? La pili, kwa kuwa umiliki wa migodi hii ni vigumu kwa Watanzania kuweza kumiliki moja kwa moja, lakini kupitia Soko la Hisa la Dar es salaam yawezekane kabisa. Kwa nini Serikali isijaribu kubadilisha utaratibu na sheria nzima ya madini pamoja na ya Kodi kuwa yafanya makampuni hayo yaweze kuwashirikisha Watanzania katika suala zima la kumiliki migodi badala ya kuachia asilimia mia kwa mia kwa wageni?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimshukuru kwa kuridhika na majibu ya msingi ambayo tumetoa kwenye swali lake. Lakini, pili, tunatambua umuhimu wa wachimbaji wadogo na kwa kweli tumekuwa tukifafanua mara kadhaa katika Bunge lako Tukufu kwamba sasa hivi Serikali inaendelea na mchakato wa kupitia taratibu zetu upya, tunaongea pia na wenye leseni kubwa ambao wamechukua maeneo mengi sana kuhakikisha kwamba baadhi yake yanaachiwa kwa wachimbaji wadogo na kwa kweli kwa eneo ambalo amelitaja Mheshimiwa Dr. Rapahael M. Chegeni, eneo la Ngasamo, hili ni mojawapo ya maeneo ambayo Serikali imeishayabainisha na tumeishakubaliana na wenye leseni katika maeneo hayo kwamba litakuwa kwa wachimbaji wadogo. Kwa hiyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili tumelizingatia na tunalifanyia kazi kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, la pili, kama tulivyosema katika jibu la msingi,. Ni kweli kwamba sasa hivi tunaendelea na taratibu, Serikali katika Kada mbali mbali katika Mamlaka mbali mbali tunawasiliana kuhakikisha kwamba sheria inaboreshwa na taratibu zinaboreshwa kama tulivyosema kwenye jibu la msingi, kuhakikisha kwamba Watanzania wengi wanashiriki katika umiliki wa hisa hasa kwenye makampuni ya madini.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Naibu Waziri amekirti kwamba Sera iko katika maandalizi, nataka nijue hiyo sera italetwa lini ili wananchi wanaoishi na hizi dhahabu wajue kwamba sasa na wenyewe wananufaika na dhahabu hizi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tumeisha sema, narudia tena kusema na tunaendelea kusisitiza kwamba sera hii tumepanga kuileta mbele ya Bunge lako Tukufu ndani ya kipindi hiki cha fedha cha mwaka 2007/2008. Na kwa kweli matarajio yetu ni kabla ya kumalizika kwa mwaka 2007.

Na. 250

**Mradi wa Kueneza Umeme Vijijini**

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu imekumbwa na ukame kwa miaka mitatu mfululizo; na kwa kuwa utegemezi wa kupata umeme kupitia nguvu ya maji umepunua sana hali iliyosababissha nchi kupata umeme kwa mgawo:

(a) Je, Serikali inaweza kulieleza Taifa sasa kuwa Mradi wa kueneza umeme vijijini umeathirika kiasi gani?

(b) Je, utaratibu wa mradi huo utaanza lini kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Umeme Vijijini inatekelezwa kutokana na fedha zinazotokana na vyanzo viwili ambavyo ni fedha zinaotengwa kwenye bajeti ya Serikali kila mwaka na fedha zinazotolewa na nchi wahisani pamoja na Taasisi za Fedha za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na miradi hiyo kuwa mingi na inayohitaji fedha nyingi, inalazimu kutekeleza miradi hiyo kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Mheshimiwa Spika, ukame ulioikumba nchi yetu kwa miaka mitatu mfululizo uliathiri uzalishaji wa umeme na hivyo kusababisha upungufu wa umeme na hatimaye mgao wa umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshinmiwa Hamza A. Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tatizo la ukame lililazimu Serikali kuingilia kati na kuelekeza rasilimali nyingi kupata umeme wa dharura. Hatua hii ilikuwa ya lazima ili kuhakikisha sekta muhimu za uchumi haziathiriki. Hivyo, mipango ya miradi ya usambazaji wa umeme vijijini iliathirika kwa kiwango kikubwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kati ya kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka 2007/2008 ni uanzishwaji wa Wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Agency)* pamoja na Mfuko wake *(Rural Energy Fund)*. Kwenye Bajeti ya mwaka huu, Wizara imepangiwa shilingi bilioni 10 kama kianzio kama ilivyojitokeza wakati tunawasilisha Makadirio ya Matumizi ya Mapato kwa Wizara yetu.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza. Je, Mkoa wa Morogoro umewahi kupangiwa mradi wowote wa umeme na ni sehemu gani? La pili, sasa tumepata utaratibu, mvua tumepata na maji yemejaa na mradi wa umeme vijijini umeishapangiwa utaratibu wa kauzishwa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi sasa kwamba nimeomba sana juu ya umeme na atashawishi taasisi hii kuweka mradi wa umeme vijiji Morogoro Kusini kama *priority?*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mkoa w Morogoro mara kadhaa umeishapangiwa miradi hasa ya nishati kwa ajili ya kutekelezwa kwa faida ya wananchi wa Mkoa wa Morogoro, lakini pia kwa maslahi ya Taifa. Miradi ambayo inatekelezwa kupitia Wizara ya Nishati na Madini ni pamoja na ile inayoratibiwa na Shirika la *TANESCO*. Lakini, ipo miradi ambayo inakuwa inaratibiwa na Wizara moja kwa moja. Mheshimiwa Spika, kwa mfano sasa hivi kumhakikishia Mbunge, kwenye huu mpango ambao unafadhiliwa na *MCC*, Mkoa wa Morogoro ni Mkoa mmojawapo ya Mikoa ya Tanzania ambayo itafaidika na mradi huu. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu wa Mkoa wa Morogoro na tutaendelea kuhakikisha kwamba huduma ya umeme ama nishati inawafikia Watanzania wengi wanaoishi Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sehemu ya pili ya swali lake, tunafahamu kama ilivyojitokeza hata wakati wa mjadala wa Bajeti yetu, Mheshimiwa Mwenegoha amekuwa na malalamiko ya muda mrefu na hili limejitokeza na akataja baadhi ya maeneo na athari ambazo amezipata tangu aanze kulalamikia suala la nishati.

Lakini, kama tulivyoeleza na pengine kwa sababu ya ufinyu wa muda hatukuweza kupata nafasi ya kueleza majibu yote kwa hoja ambazo zilitolewa na Waheshimia Wabunge, Mkoa wa Morogoro tunafahamu kuna baadhi ya maeneo hasa kwa mfano eneo la Kilosa, uthamini ulishahafanyika na inatakiwa milioni 60. Hili tumeishaliandaa na tumemuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea kutafuta fedha kwa kasi ili kuhakikisha kwamba usambazaji wa umeme katika maeneo hayo, ufanikiwe.

Lakini, pia kwenye maeneo ya vijiji kama Matombo, Kisaki, Dutumi, Mvuha na Bwakili alivyoelezea, tumweleze Mheshimiwa kwamba tunawaelekeza *TANESCO* waende kule wafanye tathmini ili tujue gharama zitakazohitajika ni kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kimsingi tunaendelea kuujali Mkoa w Morogoro na pia sehemu zingine za Tanzania.

Na. 251

**Ajira Katika Balozi Zilizopo Hapa Nchini**

**MHE. IBRAHIMU MOHAMMED SANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Ofisi za Ubalozi wa Nje zilizopo hapa nchini hutoa ajira; ikiwa ni pamoja na madereva na wafanyakazi wa majumbani; na kwa kuwa katika maeneo hayo muhimu lazima ziambatane na mikataba maalum katika kazi na haki zao za msingi ambazo wanapokuwa kazini na watakapomaliza muda wao wa kazi ambapo Serikali itahakikisha kuwa vinalindwa vizuri:-

(a) Je, Serikali inafuata utaratibu gani katika kusimamia ajira zinazotolewa na Balozi zilizopo hapa nchini?

(b) Je, viwango vyao vya mishahara vinavyotolewa na viwango vya utumishi nchini au vinatolewa kwa mujibu wa taratibu za ajira za nchi za Ubalozi husika?

(c) Je, Watanzania wanaoajiriwa katika Balozi hizo wanalipwa bima za maisha hasa kwa kuzingatia usalama wa maisha yao na unyeti wa ofisi zenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. BALOZI SEIF ALI IDDI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Mohammed Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Katika kusimamia ajira zinazotolewa na Balozi za nje zilizopo hapa nchini, Serikali imetoa uhuru kwa mwajiri kuajiri kwa kutumia sheria ya nchi yake au ya *Tanzania Employment and Labour Relations Act No. 6* ya 2004. Hata hivyo, vipo vigezo ambavyo mwajiri anapaswa kuvitumia katika kuajiri au anapoingia mkataba na mwajiriwa bila kuzingatia sheria anayotumia. Mkataba ni lazima uonyeshe:-

(i) Sheria ya kazi inayotumika;
(ii) Muda wa mkataba;
(iii) Mshahara wa mwajiriwa;
(iv) Saa za kazi;
(v) Likizo na haki zake; na
(vi) Mafao ya kustaafu au kuachishwa kazi
(vii)Marupurupu, usafiri, matibabu na kodi ya pango la nyumba.

(viii) Ofisi za ubalozi vile vile zinatakiwa kufuata sheria za Mfuko wa Akiba wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* kwa kuwasajili na kuwasilisha michango yao kwa mfuko huo.

(b)Mheshimiwa Spika, kuhusu viwango vya mshahara vinavyotolewa na ofisi za Ubalozi wa nje ni kama ilivyoelezwa hapo awali kuwa kama mkataba wa ajira umechaguliwa kuwa ni wa nchi ambayo Ubalozi wake upo hapa nchini *(sending state)* viwango vitakuwa kulingana na sheria zao ili mradi visiwe chini ya kima cha chini cha mshahara wa Tanzania, yaani shilingi za kitanzania 48,000/- kama ilivyoainishwa katika Gazeti la Serikali Na.311 la mwaka 2002.

(c)Mheshimiwa Spika, Watanzania walioajiriwa katika Balozi hizo huwa hawalipwi Bima za maisha isipokuwa wanapoumia kazini hulipwa fidia. Mwajiri anapaswa kufuata sheria ya *NSSF* kuwasajili watumishi wake *Locally Engaged Staff* na kuwalipia watumishi *NSSF* kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Vienna kuhusu uhusiano wa Kidiplomasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa migogoro na matatizo katika ajira za watumishi hao kama vile kutolipwa viinua mgongo, haki za mafao yao baada ya kuachishwa au kufukuzwa kazi kinyume cha sheria, Wizara yangu imeamua kuingilia kati suala hili la ajira za Watanzania katika ofisi za Ubalozi za Nje zilizopo nchini kuangalia uwezekano wa kila mwajiri kuwasilisha orodha ya watumishi Watanzania wanaofanya kazi katika ofisi hizo na pia kuleta nakala ya mkataba Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kila wanapoajiri, hiyo tunaamini itasaidia kutatua migogoro ya kazi pindi inapotokea.

**MHE. IBRAHIM MOHAMMED SANYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru na nitoe taarifa tu kwamba mimi Jumamosi nimetokewa na dharura ya kwenda Morogoro kidogo! Kwa hiyo nafikiri, nitasamehewa! *(Kicheko)*

**SPIKA:** Nilisema! Wameanza sasa! *(Kicheko)*

**MHE. IBRAHIM MOHAMMED SANYA:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza: Mabalozi wanaofanya kazi huwa wana muda wa contracts na Serikali zao; Je, Mabalozo hao wanapomaliza muda wao wa kazi, uajiri hutolewa upya kwa wale wanaoendelea na kazi katika Balozi ile, au wale wale huendelea na kazi waliyokuwa nayo?

Pili, kwa kuzingatia usalama wa maeneo haya nyeti na kwamba iliwahi kutokea hali ya dharura katika Balozi moja hapa nchini; Serikali imeandaa mikakati gani ya kuwafunza wafanyakazi wanaofanya kazi katika Balozi hizi, tahadhari iwapo hali ya dharura itatokea?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA - MHE. BALOZI SEIF ALI IDDI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza,

mwajiriwa anapoajiriwa na Ubalozi huwa anaajiriwa na Ubalozi na siyo Balozi. Kwa hiyo, hata Balozi huyo akiondoka, mwajiriwa huyu ataendelea kufanya kazi katika Ubalozi ule mpaka wakati wake wa kustaafu ikifika. Isipokuwa kama yatatokea mambo mengine ambapo mwajiriwa anaweza akaacha kazi au kuachishwa kazi.

Mheshimiwa Spika, hatuna hivi sasa mkakati wa kusema tunawaelimisha Watanzania wanaofanya kazi katika Balozi kwa sababu Ubalozi unalindwa, kama nilivyosema Mkataba wa Vienna kuhusu uhusiano wa Kidiplomasia. Kwa hiyo, kufanya kitu chochote kwa mwajiriwa wa Ubalozi, maana yake ni kuingilia mambo ya ndani ya Ubalozi ule au kuingilia mambo ya ndani ya nchi iliyoleta Ubalozi ule. Suala la uhusiano kati ya Ubalozi na mwajiriwa, kwa kweli ni suala linalohusu Ubalozi na mwajiriwa mwenyewe.

Na. 252

**Uwindaji wa Wanyamapori**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, uwindaji wa wanyamapori unafanyika katika *Hunting Blocks* zilizopo katika Wilaya zetu ambapo wananchi waishio katika maeneo hayo wanasaidia sana katika kuwahifadhi wanyamapori hao; na Halmashauri husika, zinahakikisha utunzaji wa mazingira katika maeneo hayo ya uwindaji:-

(a) Je, ni kwa nini leseni za uwindaji wa kitalii zinatolewa na Idara ya Wanyamapori Makao Makuu bila kuzihusisha Wilaya husika?

(b) Kwa kuwa, asilimia ishirini na tano ya mapato ya uwindaji hutolewa kwenye Halmashauri za Wilaya. Je, ni asilimia ngapi ya fedha ambayo Halmashauri za Wilaya hazijui wakati wa ukokotoaji wa kupata hilo pato dogo kwa Halmashauri?

(c) Je, ni Sheria gani ilitumika kunyang'anya wananchi maeneo ya wazi ambayo walikuwa wamekata leseni na kuwinda kwa kujipatia kitoweo na kuyagawa kwa wawindaji wa kitalii?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori Sura Na.283 iliyorekebishwa mwaka 2002, mamlaka ya kutoa leseni kwa ajili ya uwindaji yamewekwa chini ya Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori. Kwa kuzingatia mamlaka hayo, Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori hutoa vibali vya uwindaji wa kitalii kwa wageni wote wanaokuja kufanya uwindaji nchini. Vibali hutolewa baada ya

tathmini kufanywa na Idara ya Wanyamapori na kuwasilishwa kwenye Kamati ya Ushauri ya Kugawa vitalu kwa kukaguliwa, kujadiliwa na kutolewa ushauri stahili.

Ushauri huo huwasilishwa kwa Waziri ili utumike katika ugawaji wa vitalu. Kwa kutambua kuwa Halmashauri za Wilaya ni wadau wakuu katika kuendesha na kusimamia shughuli za uwindaji wa kitalii nchini. Maafisa Wanyamapori wa Wilaya wamepewa jukumu la kuhakiki maeneo ya vitalu vya uwindaji wa kitalii kwenye mapori tengefu na mapori ya wazi yenye wanyamapori katika Wilaya husika. Taarifa hiyo hutumiwa na Idara ya Wanyamapori katika kugawa kota ya uwindaji wa kitalii, uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi. Aidha, majukumu mengine ya Maafisa Wanyamapori wa Wilaya ni pamoja na kuwateua Maafisa wasimamizi wa safari za uwindaji pamoja na kutoa taarifa ya kazi hiyo kila baada ya msimu wa uwindaji kumalizika.Kwa msingi huo, Halmashauri za Wilaya zinahusishwa kikamilifu katika suala zima la kusimamia matumizi ya vibali vya uwindaji wa kitalii ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri stahili kuhusu utekelezaji wa shughuli za uhifadhi wa wanyamapori na uwindaji wa kitalii.

(b)Mheshimiwa Spika, mgao wa asilimia 25 ya fedha za uwindaji wa kitalii zinatokana na ada za wanyamapori waliowindwa kwenye vitabu vilivyoko kwenye Wilaya husika. Kwa kuwa Halmashauri za Wilaya huwakilishwa na Afisa Wanyamapori wa Wilaya katika kutekeleza majukumu ya kusimamia uwindaji wa kitalii, wajibu huo unamwezesha kufahamu aina na idadi ya wanyamapori waliowindwa katika maeneo yao kwa kila msimu wa uwindaji. Hivyo, kuwaweka katika nafasi ya kufahamu mgao stahili wa fedha za asilimia 25 kwa ajili ya Halmashauri zao.

(c) Mheshimiwa Spika, kazi ya kutambua na kutenga vitalu vipya hufanywa na Idara kwa kushirikiana na Maafisa Wanyamapori wa Wilaya husika. Wizara yangu haijapokea taarifa ya wawindaji wenyeji na wageni wakazi kunyang'anywa leseni za kuwinda kwa ajili ya kitoweo ili kugawa maeneo kwa wawindaji wa kitalii. Utaratibu unaotumika ni kwa wawindaji wenyeji na wageni wakazi kutoa taarifa kwa Kampuni za uwindaji wa kitalii kuhusu shughuli zao za uwindaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikipokea maombi kutoka kwa baadhi ya Halmashauri za Wilaya na Vijiji kutaka maeneo yao yatengwe kuwa vitalu vya uwindaji wa kitalii na yagawiwe kwa kampuni zenye sifa stahili. Maombi hayo yanatokana na Halmashauri hizo kutambua umuhimu wa shughuli za uwindaji wa kitalii, hasa mgao wa 25% ya mapato kutokana na uwindaji huo pamoja na michango inayotolewa kusaidia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ya vijiji vilivyo karibu na vitalu vya uwindaji. Wilaya ambazo zimeleta maombi hayo ni pamoja na Wilaya ya Nkasi, Serengeti, Manyoni, Rufiji, Kilwa na Sikonge.

**MHE. SAIDI JUMA NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wanaozunguka maeneo ya vitalu wanayo haki wanapotimiza masharti yote yanayowekwa ya uwindaji katika maeneo waliyoruhusiwa, wanayo haki ya kuwinda, kufanya shughuli zao za kiuchumi kama kulina asali na kadhalika. Na kwa kuwa baada tu

ya wawindaji hawa kitalii kupewa maeneo wananchi wamekuwa wanafukuzwa katika maeneo hayo wananchi wamekuwa wanafukuzwa katika maeneo hayo.

(a) Je, Serikali inatoa tamko gani la kuwaruhusu wananchi wanapokuwa wametimiza masharti yote waweze kwenda sambamba na wawindaji wa kitalii katika shughuli zao za kiuchumi ambazo ziko katika masharti ambayo wao watakuwa wamepewa? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa wawindaji wa kitalii baadhi yao wamekuwa wanachangia shughuli za Maendeleo katika vijiji ambavyo vinazunguka katika maeneo lakini baadhi yao wamekuwa wakorofi hawataki ushirikiano na wananchi wanaozunguka katika maeneo yale na kubeza na kuona kwamba suala la kuchangia ni hisani. Je, Serikali kupitia fursa hii ya Bunge Tukufu inatoa tamko gani kuwakumbusha hawa wawindaji wa kitalii kwamba ni wajibu wao kuchangia shughuli za Maendeleo yanayohusika? (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtaona naendelea kidogo tulitumia muda wa matangazo leo yale ya Kamati na taarifa yalichukua dakika 8. Kwa hiyo, tunaendelea kidogo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Said Nkumba, kwa jinsi anavyoshughulikia matatizo ya wananchi wake hasa panapokuwa panatokea bugudha inayotokana na wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, wawindaji wenyewe na wageni wa kazi huwa wana winda kwenye mapori tengefu na mapori ya wazi baada ya kupata leseni kwa Afisa Wanyamapori wa Wilaya. Kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi wakishapata leseni wanapaswa kutoa taarifa kwa Maafisa Wanyapori wa Wilaya kuhusu dhamira yao ya kwenda kuwinda. Lakini kama nilivyojibu kwamba taarifa hii ni ya muhimu tu kwa sababu za kiusalama. Sasa kusema kweli wananchi hawa kama alivyosema Mheshimiwa Nkumba, wana haki ya kuwinda katika maeneo haya ambayo nimeyataja. Haki hiyo ni ya kwao. Hivyo basi kama itatokea wawindaji wenyeji na wageni wakazi kubugudhiwa na hayo makampuni, wawindaji wa kitalii ama kunyang'anywa leseni na maafisa wanyamapori kwa kweli tungeomba watoe taarifa haraka iwezekanavyo kwa Wizara hususan Idara ya Wanyamapori ili hatua stahili ziweze kuchukuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo naomba nichukue nafasi hii kuwaonya wote wale ambao wana tabia hiyo ya kuwanyanyasa wananchi hawa waache. (*Makofi*)

Swali la pili, miongoni mwa masharti ambayo mmiliki wa kitalu cha uwindaji wa wanyamapori anapaswa kutekeleza ambayo ni sharti ni pamoja na kuchangia Maendeleo ya miradi ya wananchi, hilo ni sharti muhimu ambalo linatakiwa kutekelezwa. Hivyo basi kipengele hiki cha uchangiaji wa miradi ya Maendeleo ya wananchi vile vile huzingatiwa wakati ambapo vitalu vinagawiwa upya tena baada ya miaka mitano. Hasa iwapo kampuni ya utalii itakuwa haikutekeleza sharti hili itakuwa ni miongoni mwa sababu za kutoweza kuendelea tena na uwindaji wa kitalii katika maeneo hayo. (*Makofi*)

**MHE. HAROUB S. MASOUD:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo hii sisi tunatarajia kupitisha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, ambayo inasimamia mambo ya *Gender* na kwa kuwa kuna taarifa za kuaminika kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii inaelewa kwamba wanyamapori ni rasilimali kubwa ya nchi hii lakini pale inapotakiwa kuwapunguza baadhi ya wanyama, wanyama wanaoliwa ni wale madume tu. Je, hiyo ni haki? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Masoud hilo swali halina hata ushahidi wowote. *(Kicheko)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema wanashirikisha Halmashauri kupata ushauri kutoka Wilayani na kwa kuwa hakutaja kama wananchi husika huwa wanashirikishwa na kupata maoni yao kabla eneo halijagawanywa kuwa kitalu na kwa kuwa kati ya wananchi wanaoathirika ni pamoja na Wahadzabe ambao kwao nyama ndio chakula pekee pamoja na mizizi na kwa kuwa kabila hili sasa liko kwenye hatari ya kutoweka na kitalu kikitolewa wanyama wote huondoka.

Je, Serikai sasa iko tayari kusitisha zoezi la kutoa vitalu katika eneo la Yaeda Chini na inayoelekea Karatu ili hawa Wahadzabe wapate haki yao ya kuishi kwa wanyama hawa kubaki katika eneo lao ili wapate chakula mpaka utaratibu mwingine utakapoandaliwa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza Wizara yangu inashirikiana sana na Halmashauri za Wilaya na ninategemea kabisa kwamba kila Halmashauri ya Wilaya ina Diwani wa kila eneo ambaye anajua kwamba eneo lake limepangwa kuwa kitalu na kuiomba Wizara ifanye hivyo. Kwa hiyo, haiwezekani kwamba eneo linaweza kutengwa kuwa kitalu bila fursa ya wananchi wa eneo hilo kupatikana.

Pili, uwindaji wa kitalii haumalizi wanyama walioko katika eneo. Uwindaji huo unafanywa kwa makini kwa kuchagua wanyama kwa *quarter* ili kuruhusu wanyama zaidi waweze kuongezeka. Kwa hiyo, haiwezekani kabisa kwamba eneo linafanywa kitalu cha uwindaji wa kitalii ili wanyama watoweke.

Hivyo hivyo katika maeneo hayo ya Wahadzabe eneo ambalo limetengwa kuwa kitalu yule aliyepewa kitalu hiki wala hawindi. Kazi yake kubwa ni kuleta watalii wa kupiga picha na kuendeleza eneo hilo kwa faida ya wananchi anaowataja na katika kipindi cha mwaka huu unaofika wamepanga mpaka shilingi bilioni 8 kwa ajili ya Maendeleo ya wananchi wa eneo hilo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaishia hapa lakini kwa mamlaka niliyonayo chini ya Kanuni 126 ningeomba swali alilouliza Mheshimiwa Haroub Masoud, Naibu Waziri aweze kulijibu lina umuhimu. Kwa nini wanyama madume tu ndiyo wanaouawawa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, katika kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Slaa, nilisema kwamba uwindaji unalenga kupata nafasi ili wanyama waongezeke katika maeneo husika. Kwa hiyo, baada ya maelezo hayo napenda sasa nimjibu Mheshimiwa Haroub Masoud, kama ifuatavyo:-

Ili kuhakikisha kwamba wanyama wanaongezeka katika maeneo husika leseni zinatolewa kuwinda wanyama ambao ni wazee, ambao hawazai tena na hawa wanaweza kuwa madume au majike. Aidha, katika *ekolojia* ya wanyama wanyama majike ndiyo msingi mkubwa wa kuongezeka kwa wanyama. Kwa sababu hiyo huwezi kuwawinda majike ambao bado wana uzazi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi ana maelezo ya ziada. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa jibu zuri, nina nyongeza ndogo tu. Katika ekologia ya wanyama, mnyama dume mmoja ana-*service*/anahudumia majike wengi ndiyo maana kuwapunguza madume hakuna athari katika kuzaliana kwa wanyama. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge, baada ya majibu hayo ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ambayo ni ya kisayansi kabisa, muda wa maswali umekwisha. Maswali mawili yaliyosalia tutashughulikia wakati mwingine.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Waziri wa Ulinzi anaye mgeni wake ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Kata ya Kaliua kule Wilayani Urambo, Ndugu Ramadhan Kahumbila, yule pale. Karibu sana. Ahsante sana.

Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Naibu Waziri wa Ulinzi na JKT na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, wanaye mgeni wao Mheshimiwa Borafya Silima Juma, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mjini Zanzibar. Yuko pale *Speakers Gallery*. Karibu sana Mwenyekiti, tunafurahi sana kukuona hapa na huwa tunapenda Ndugu zetu kutoka Zanzibar mnapokuja hapa Dodoma kuona shughuli za Bunge karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Juma Killimbah, anao wageni kutoka jimboni kwake kama ifuatavyo:- Bwana Abbas Majule naomba asimame, Katibu Kata Kinampanda Bwana Theosela Simon, Bwana Juma Nkungu, Bi Fatma Fathil na Bwana John Kingu. Karibuni sana. Napenda kuwahakikishia kwamba Mbunge wenu anafanyakazi vizuri hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Sophia Simba, anao wageni ambao hawakutajwa wanatoka wapi nadhani wanatoka Dar es Salaam: Bwana Hassan Mang'elele, Hadija Uzia, ningeomba wasimame wale pale mkono wa kulia, Ali Rashid, Bwana Busoro Pazi, Raul Criph, Jumanne Shaab, Soud Simba, huyu sijui ni Ndugu yake Waziri. Lakini Simba ni jina la kawaida kwa hiyo pengine siyo au ndiye. Ndugu Abdallah Mkoma, Salehe Kitala, Saadi Kiinji, Bi Evelini Ngoko, Bi Joyce Nzwala na John Solombi. Hawa naambiwa wanatoka Ilala Dar es Salaam. Naona Mheshimiwa Zungu watu wana kubipu. Wapo

wanafunzi wawili kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe nao ni Josephine Lwiza na Lilian Nelson wale pale. Ahsante sana wasomi wetu msome kwa bidii Tanzania inahitaji wasomi waliobobea.

Mikutano, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje anawaarifu kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo ya Mambo ya Nje leo tarehe 19 Julai, 2007 saa tano asubuhi ukumbi 219. Aidha Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anaomba wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, wakutane leo tarehe 19 Julai , 2007 saa saba mchana ukumbi na. 231.

Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, anaomba wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Kilimo na Ardhi wakutane leo saa tano asubuhi ukumbi 432.

Mheshimiwa William Shellukindo, mratibu wa *Bunge Range Club* anaeleza kwamba kutakuwa na zoezi la kulenga shabaha litakalofanyika siku ya Jumapili tarehe 22 Julai, 2007 wanachama watie sahihi kwenye orodha iliyoko kwenye *lounge* ya Jengo la Bunge kabla ya kujumuika katika muda ambao watakubaliana kwenda kulenga shabaha. Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu, wanakaribishwa na Bodi ya usajili ya Wakandarasi *(CRB)* katika ufunguzi wa mkutano wa Wakandarasi wa kanda ya kati. Shughuli hiyo ya ufunguzi inafanyika leo kuanzia saa tano katika ukumbi wa *St. Gasper* hapa hapa Dodoma.

Kwa hiyo, Bodi ya usajili wa Wakandarasi saa tano kamili pale kwenye Ukumbi wa Mtakatifu *Gasper.*Nilikuwa naomba tu kutoa taarifa kwamba kesho nitakwenda Dar es Salaam kwa ajili ya shughuli muhimu ya kuapishwa kwa Jaji Mkuu mpya. Kwa hiyo, sitakuwepo siku nzima. Lakini zaidi ya hapo wiki ijayo nitakuwa nawakilisha katika Mkutano wa *CPA Africa Region* ambao unafanyika *Cape Town*. Kwa hiyo, kwa siku kadhaa za siku ijayo sitakuwepo hapo Dodoma.

**WABUNGE FULANI:** Jumamosi.

**SPIKA:** Bado mbona mna haraka. Matangazo hayajaisha hii inazidi kudhihirisha hofu mliyonayo kuhusu shughuli hiyo. (*Kicheko*)

Nilikuwa naelezea safari yangu kwamba sitakuwepo, Kwa siku ya Jumamosi kwanza saa 12.00 ni *VIP Race* zile mbio zetu za kawaida zinazofadhiliwa na *Cargo Star*, halafu kiasi cha saa mbili tutakuwa tumemaliza na saa tatu kamili katika eneo litakalopangwa, litakalojumuisha wananchi ndiyo tutakuwa na vipimo vile vya UKIMWI kumwunga mkono Mheshimiwa Rais. Kesho tutatoa ratiba nzima kadri itakavyokuwa. Kwa hiyo, wote mnakaribishwa ingawa jambo lenyewe linasemekana ni la hiari lakini kwa kiongozi kukwepa mambo ya namna hii nayo kidogo ina athari zake kisiasa. Kwa hiyo, ni hiari sawa lakini vizuri mnakaribishwa.

Nimeelezwa na Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba mara ya mwisho ulipotokea wito wa kupima katika Bunge lililopita mwaka 2000 walijitokeza Waheshimiwa 20 tu. Sasa natumaini hali hii tena isijirudie hili ni Bunge jingine kabisa jipya tuna tumaini sote tutakuwa pale. Kama nilivyosema mimi mwenyewe ndiyo nitakuwa wa kwanza ndiyo itifaki. Kwa hiyo, shughuli zitakuwa hivyo.

Basi nashukuru kwamba nitaliacha Bunge mikononi mwa Naibu Spka, ambaye kama mnavyomfahamu ni mtu mahiri sana, anajua shughuli hii. Kitu kimoja tu kuhusu Naibu Spika, kinanipa shida ni kwamba ikiwa ataamua kugombea Uspika mwaka 2010 itabidi mimi niachie ngazi tu. Baada ya kusema hayo sasa naomba Mheshimiwa Jenista Mhagama, aje aongoze shughuli na mkutano hivi punde. (*Makofi/Kicheko*)

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo ya Mheshimiwa Spika, sasa tutaendelea na *Order Paper* kadri inavyotueleza.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008
### Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Watoto

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, iliyochambua Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2007/2008.Utangulizi, awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha salama katika kipindi kingine cha kuwasilisha bajeti ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Serikali. Nianze kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuliongoza Taifa letu vizuri kwa kipindi chote toka ameingia madarakani. Rais ameonyesha umahiri mkubwa wa uongozi katika nyanja zote za maendeleo ya nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri samahani kidogo. Waheshimiwa Wabunge, naomba wale wanaotoka basi waondoke taratibu kusudi Hotuba ya Waziri iweze kusikika vizuri. Mheshimiwa Waziri unaweza ukaendelea.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa juhudi zake kubwa za kumshauri Rais, kuimarisha Muungano na kwa kuhamasisha utekelezaji wa Sera mbalimbali za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa - Waziri Mkuu, kwa hotuba yake ambayo imekuwa dira ya mjadala wetu hapa Bungeni.

Aidha nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Juma Ngasongwa, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Mheshimiwa Zakhia Hamdani Meghji, Waziri wa Fedha, kwa hotuba zao ambazo zimetupa mwelekeo mzuri wa hali ya uchumi na bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha 2007/08. Mwelekeo huo umezingatiwa kikamilifu katika maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha miaka miwili ya Awamu ya Nne, wewe mwenyewe umeonesha uhodari mkubwa katika kusimamia na kuratibu shughuli za Bunge. Nachukua nafasi hii kumpongeza Spika wa Bunge hili kwa kazi nzuri unayoifanya. Aidha nawapongeza pia Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti, kwa kuliongoza bunge vizuri wakati ulipokuwa na majukumu mengine nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa namna ya pekee kuishukuru Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ikiongozwa na Mwenyekiti wake wewe mwenyewe Mheshimiwa Jenista Mhagama na Makamu wake Mheshimiwa Horoub S. Masoud, kwa kuichambua na kuijadili bajeti ya Wizara yangu kwa kina. Wizara yangu inaahidi kuimarisha ushirikiano uliopo katika kuleta maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kumpongeza Dr.Asha-Rose Migiro aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Uteuzi huo umetuletea heshima kubwa duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, kwa kuchaguliwa kwake na wananchi wa Jimbo la Tunduru kwa kura nyingi. Pia nampongeza Mheshimiwa Dada yangu Frolence S. Kyendesya kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Niruhusu nitumie fursa hii kwa mara nyingine kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya marehemu Juma Jamaldin Akukweti, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge) aliyefariki Dunia tarehe 4 Januari 2007, kutokana na ajali mbaya ya ndege iliyotokea huko Mbeya mwezi Desemba, 2006. Natoa pia salaam za rambirambi kwa familia za marehemu wengine waliokufa katika ajali hiyo mbaya ya ndege.

Aidha kwa masikitiko na majonzi makubwa natoa salamu za rambirambi kwa familia ya marehemu, aliyekuwa kijana na mpenzi wetu Amina Chifupa Mpakanjia aliyetutoka ghafla tarehe 26 Juni, 2007. Vile vile natoa salaam za rambirambi kwa familia za marehemu kaka zangu Stephen Kazi na pia kaka yangu Omari Chubi ambao nao pia wametutangulia mbele ya haki.

Nachukua nafasi hii pia kutoa pole kwa ndugu na jamaa wa abiria waliofariki katika ajali zilizotokea hivi karibuni katika Mikoa ya Arusha na Singida. Tunaomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo, napenda kuchukua fursa hii sasa kufanya mapitio ya utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara yangu katika kipindi cha 2006/07 na makusudio ya utekelezaji katika kipindi cha 2007/08.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji Wa Mpango na Majukumu ya Wizara Kwa Mwaka 2006/07 Maendeleo ya Jamii, Katika jitihada za kutafuta rasilimali za kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Maendeleo ya Jamii, kwa ufanisi zaidi, Wizara yangu iliandaa Waraka kuhusu Mapendekezo ya Kuimarisha Sekta ya Maendeleo ya Jamii kwa kuzingatia maoni na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge.

Waraka huo ulijadiliwa katika vikao mbali mbali na hatimaye kupitishwa na Baraza la Mawaziri tarehe 19/3/2007. Utekelezaji wa mapendekezo yaliyopitishwa utaongeza ushiriki wa wananchi katika mchakato wa kujiletea maendeleo yao kiuchumi, kijamii na hata kisiasa na hivyo kuwa na kasi nzuri ya maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 (Sura ya 8), miongoni mwa majukumu ya msingi yaliyopo mbele yetu Watanzania ni kuwashirikisha wananchi wote kwa njia ya uwezeshaji katika kukuza uchumi na kutokomeza umaskini.

Ili kutekeleza jukumu la kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kujiletea maendeleo yao na ya Taifa kwa ujumla, Wizara yangu katika mwaka 2006/07, iliendesha mafunzo ya rejea na semina mbali mbali kwa Wataalam wa Maendeleo ya Jamii 371.

Mafunzo na semina hizo zilikuwa na madhumuni ya kuwajengea uwezo maafisa hao ili waweze kutumia elimu na stadi walizopata katika kuhamasisha wananchi kujiletea maendeleo endelevu. Wataalam hao walitoka katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Tanga, Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Iringa, Dodoma, Morogoro, Singida, Manyara, Kilimanjaro, Arusha, Pwani, Shinyanga, Tabora, Mwanza, Mara na Dar es salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006/07, nililiarifu Bunge lako kuwa, Wizara yangu ilikuwa imeziagiza Halmashauri kurejesha majumba ya maendeleo katika matumizi yaliyokusudiwa badala ya kuyakodisha kwa matumizi mengine.

Hata hivyo bado Halmashauri hazijatekeleza suala hilo kwa kutofikia mwisho wa mikataba ambayo iliishaingia na wakodishaji. Kwa sababu hiyo Wizara imepeleka seti kumi na moja (11) za luninga zilizonunuliwa 2005/2006 kwa ajili ya majengo hayo, kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilivyomo kwenye Halmashauri hizo.

Aidha, seti nyingine kumi (10) zilizonunuliwa 2006/2007 pia nazo zitapelekwa kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi zikisubiri kuchukuliwa na Halmashauri pindi zitakaporejesha majumba ya maendeleo kama njia mojawapo ya kutoa elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha utendaji kazi katika sekta ya Maendeleo ya Jamii, Wizara katika mwaka wa fedha 2006/2007, imeendelea na utaratibu wake wa kufanya Mkutano Mkuu wa kila mwaka. Mkutano wa Mwaka ulifanyika katika Ukumbi wa Benjamin Mkapa Jijini Mbeya kuanzia tarehe 29 Agosti, hadi tarehe 2 Septemba, 2006. Washiriki wa Mkutano huo walikuwa ni pamoja na viongozi na watendaji wakuu wa Wizara, Washauri wa Sekretarieti za Mikoa wa Masuala ya Maendeleo ya Jamii, Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri za Wilaya, Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, wawakilishi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Kazi, Ajira na Vijana. Vile vile, kulikuwa na uwakilishi wa Wizara ya Ajira, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto Zanzibar, bila kuwasahau wenyeji wetu wa Jiji la Mbeya. Wadau walitathmini utendaji wa kazi wa sekta na kuweka mikakati ya kuiendeleza pamoja na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wa Maendeleo ya Jamii ndio waraghbishi wakuu na chachu ya kuwezesha watu kushiriki katika kubuni, kupanga, kutekeleza na kutathmini shughuli zao za maendeleo. Wataalam hao hata hivyo bado ni wachache sana katika ngazi ya kata kuweza kukidhi umuhimu wa kuwa na angalau mtaalam mmoja wa Maendeleo ya Jamii. Kwa kuzingatia uchache huo Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya jamii katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Missungwi na Rungemba ambapo jumla ya wanachuo 597 wakiwemo wanawake 414 na wanaume 183 walipata mafunzo ngazi ya Cheti. Aidha Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kilisomesha wanachuo 638 wakiwemo wanawake 384 na wanaume 254 katika ngazi ya Stashahada ya Juu. Wizara iliendelea na utaratibu wake wa kuwaendeleza watumishi waliopo kwenye Halmashauri ambao wana cheti cha Maendeleo ya Jamii, kwa kutenga asilimia 60 ya nafasi za kujiunga na Chuo cha Tengeru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara vile vile katika kipindi cha 2006/07 imetekeleza mikakati yake ya kuviendeleza Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili viende na wakati kulingana na mahitaji ya sasa ya taaluma. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara imedurusu mitaala ya cheti ili kukidhi mahitaji ya sasa. Aidha imeandaa Mitaala mipya ya ngazi ya stashahada ili kuviwezesha Vyuo vya Buhare, Missungwi na Rungemba kusajili wanafunzi wa ngazi ya stashahada. Vyuo hivyo vitaanza kutoa Stashahada kuanzia mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu imefanya mapitio ya Mkakati wa Kijamii wa Kuwakinga Wanawake na Watoto dhidi ya Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) na magonjwa ya zinaa. Madhumuni yalikuwa kuuboresha ili uweze kutumika katika mapambano dhidi ya UKIMWI na maambukizi ya VVU katika jamii. Aidha, katika kila mafunzo/semina zilizotolewa, masuala ya UKIMWI yalifundishwa kama sehemu ya utekelezaji wa Mkakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,, Sote tunafahamu kuwa hifadhi ya mazingira ni mojawapo ya masuala yaliyopewa kipaumbele katika awamu hii ya nne. Uharibifu wa mazingira hususan ukataji miti ovyo, na uchafuzi wa vyanzo vya maji, ni miongoni mwa sababu zinazozidisha umaskini. Wizara yangu imeandaa Mkakati wa Hifadhi ya Mazingira na kuanza kuutekeleza katika kipindi cha mwaka 2006/2007. Shughuli zilizofanyika ni kuongeza masuala ya hifadhi ya mazingira katika mitaala ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi; upandaji wa miti 27,450 na kufanya usafi wa mazingira katika maeneo ya Vyuo; kuwaelimisha viongozi wa vijiji na Jamii kuhusu kupanga mikakati ya kuhifadhi vyanzo vya maji katika wilaya za Mufindi na Mbarali; kutoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii na Wakufunzi wa Vyuo 50 kutoka mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Lindi, Manyara, Mara, Morogoro, Mwanza, Shinyanga, Singida, Tabora, na Tanga, mikoa ambayo kuna uharibifu mkubwa wa mazingira unaotokana na ufugaji holela wa mifugo na ukataji miti.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea na jukumu lake la kutoa elimu na mafunzo ya kazi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 58 nchini. Katika mwaka 2006/2007, wananchi wapato 27,907 walipatiwa mafunzo hayo wakiwemo wanawake 13,054 na wanaume 14,853. Mafunzo hayo yalilenga katika kuwapatia ujuzi wa kazi mbali mbali pamoja na uelewa katika masuala yanayowazunguka ili kuwawezesha kujitegemea na kuwa raia wema. Aidha, Wizara imeandaa mpango wa maboresho (Reforms) katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kupitia Mpango wa Kuboresha Elimu ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha na kuboresha mazingira ya Vyuo, Wizara imeendelea na jitihada zake za kukarabati majengo na miundombinu vyuoni. Vyuo vya Malampaka (Maswa), Chilala (Lindi), Buhangija (Shinyanga Mjini) na Munguri (Kondoa) vilipatiwa fedha za ukarabati mkubwa ambapo vyuo vya Arnatoglou (Ilala), na Sofi (Ulanga) vilipatiwa fedha za ukarabati mdogo. Aidha, Vyuo vya Chisalu (Mpwapwa) na Ulembwe (Njombe) vilipatiwa fedha kwa ajili ya kuweka mitambo ya umeme unaotokana na nguvu ya jua. Wizara imenunua pikipiki kumi (10) kwa ajili ya Vyuo vilivyoko umbali mkubwa zaidi kutoka Makao Makuu ya Wilaya. Vyuo vilivyohusika ni Chala, Chilala, Chisalu, Kiwanda, Malya, Mlale, Msaginya, Msingi, Muhukuru na Sofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia masuala ya teknolojia ya kisasa na mawasiliano, Wizara pia imeendelea na ununuzi wa kompyuta kumi (10) ili zielekezwe kwa vyuo vingine katika mfululizo huu wa kuendeleza teknolojia Vyuoni. Vyuo vilivyopelekewa Kompyuta ni Kilosa, Kilwa Masoko, Kisarawe, Mabughai, Mamtukuna, Mbinga, Msinga, Mtawanya, Mwanva na Newala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuvipatia Vyuo Hati za kumiliki ardhi na hivyo kuondoa migororo ya kugombea mipaka, Wizara yangu ilituma fedha kwa Vyuo vya Nzega, Ilula na Arnatoglou kwa ajili ya upimaji wa ardhi na uandaaji wa hatimiliki. Chuo cha Katumba tayari kina hatimiliki. Aidha Chuo cha Monduli ambacho tayari kilikuwa na

hatimiliki kinahitaji kufanyiwa marekebisho baada ya sehemu ya ardhi yake kugawiwa Taasisi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya jinsia, mojawapo ya malengo ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ni kuhakikisha kunakuwepo uwiano wa kijinsia katika kuleta maendeleo, ili kupunguza umasikini miongoni mwa jamii. Hiyo itawezekana kwa kuwawezesha wanawake kiuchumi. Katika kutekeleza azma hiyo Wizara ikishirikiana na Taasisi mbalimbali, imewapatia wafanyabiashara wadogo wadogo wanawake fursa ya kushiriki katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara nje na ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea na utaratibu wa kuiwezesha jamii kujiletea maendeleo yake kwa utaratibu wa kutoa mafunzo mbali mbali sambamba na uhamasishaji wa wanawake kujiunga na Vyama vya Kuweka na Kukopa. Aidha, kupitia mafunzo hayo, wanawake wamewezeshwa kuunda vikundi vyao vya wajasiriamali ikiwa ni njia mojawapo ya kupata mikopo kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo kwa wadau kuhusu namna ya kuingiza masuala ya jinsia katika Sera, Mikakati, Mipango na Programu mbali mbali za maendeleo, sambamba na kuelekeza matumizi ya Mkakati wa Maendeleo ya Jinsia kwa Watendaji wa Dawati la Jinsia yametolewa. Mafunzo hayo yameendeshwa katika Halmashauri za Miji na Manispaa za Mikoa mbali mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeanzisha mchakato wa uanzishaji wa Benki ya Wanawake. Benki hii imesha sajiliwa na kupewa jina la "Benki ya Wanawake Tanzania Ltd." kwa namba ya usajili 59271. Akaunti ya kukusanyia fedha *(ASCROW)* imefunguliwa katika Benki ya Taifa ya Biashara *(NBC)* Ltd. Tawi la *Corporate* kwa Akaunti Na. 011103028717. Ili Benki iweze kupata Leseni ya Benki Kuu, mtaji wa shillingi bilioni mbili (2.0bn/-) unahitajika. Serikali imeanza kuhamasisha Mashirika, Waheshimiwa Wabunge na watu binafsi kama waanzilishi, kununua hisa ili kukuza mtaji. Sababu za kuanzisha Benki hiyo, ni kuviwezesha vikundi mbalimbali vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa ambavyo hadi sasa wanachama walio wengi ni wanawake wajasiriamali na watu binafsi kupata mikopo na huduma mbalimbali za kibenki ili kukuza uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya jinsia hayana budi kuzingatiwa katika sekta zote. Hii ni pamoja na haki za kisheria. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Sheria na Katiba imeendelea kushughulikia sheria zenye upungufu kijinsia. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, sheria ya mirathi, na kutunga sheria mpya ya watoto. Aidha katika kuhakikisha vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto vinatokomezwa, Wizara yangu imetoa mafunzo kuhusu haki za binadamu, haki za watoto na sheria zinazolinda haki za jamii kwa Maafisa 132 wa Serikali wanaosimamia utekelezaji wa sheria na upatikanaji wa haki katika jamii kutoka Mahakama na Usalama wa Raia wa mikoa ya Tabora, Singida, Dodoma, Dar es Salaam, Pwani, Kigoma, Morogoro na Kilimanjaro.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za makusudi ili kuhakikisha inaondoa upungufu kijinsia katika nyanja zote za maendeleo. Ili kufanikisha azma hiyo, Wizara imeandaa rasimu ya mapendekezo ya mchakato wa utekelezaji wa maelekezo ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Ibara ya 120 (a) ya Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbali mbali za uongozi na maamuzi ifikapo 2010. Aidha, Wizara imeunda Kamati ya Wataalam inayohusisha wadau mbali mbali kwa ajili ya kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa mchakato mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki katika Mikutano ya Kimataifa na Kikanda hutumika kupeana uzoefu, kutoa taarifa na kupitisha maazimio na mikakati ya utekelezaji wa mikutano hiyo. Wizara yangu imeshiriki mikutano kadhaa ya kimataifa ukiwemo wa Kamati ya Umoja wa Mataifa kuhusu Hali ya Wanawake *(CSW)* mwezi Machi, 2007 huko *New York* Marekani. Mkutano ulisisitiza uondoaji wa aina zote za unyanyasaji na ukatili dhidi ya mtoto wa kike.

Aidha, nchi yetu ni mwanachama wa Jumuiya ya Madola, ambapo nchi wanachama hukutana kila baada ya miaka mitatu kujadili maendeleo ya jinsia pamoja na mambo mengine ya Maendeleo. Ni katika mikutano hiyo kila nchi mwanachama hutakiwa kutoa taarifa ya utekelezaji wa masuala ya jinsia. Mwaka huu Wizara yangu imeshiriki mkutano huo uliohusu masuala ya jinsia ambao ulifanyika mwezi Juni, 2007 nchini Uganda. Taarifa zilizotolewa katika mkutano huo ziliwezesha nchi kujipima ni kwa kiasi gani imefanikiwa kutenga raslimali za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa masuala ya jinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani huadhimishwa tarehe 8 Machi ya kila mwaka. Wizara yangu imeendelea kuratibu Maadhimisho haya kimkoa. Kaulimbiu ya mwaka huu 2007 ilikuwa: “Wanawake na Mazingira: Tumia Vikapu vya Asili, Tunza Mazingira Yetu”. Kaulimbiu hiyo inatoa ujumbe wa kuelimisha jamii kutumia vikapu vya asili kama njia mbadala, matumizi ya mifuko ya plastiki maarufu kama “rambo”. Madhumuni ya Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ni kutoa nafasi kwa jamii kufanya tathmini ya shughuli mbalimbali za maendeleo ya wanawake na kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya motto. Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2006/2007, ilifuatilia tafiti mbalimbali, kuhusu jukumu la familia na jamii katika kupunguza ongozeko la watoto wanaoishi mitaani katika Manispaa za Iringa na Dodoma na wilaya za Mufindi, Ilemela, Magu na Chamwino. Lengo ni kubaini sababu zinazochangia kuwepo kwa ongezeko kubwa la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na kupata mbinu mbadala za kupunguza tatizo hilo. Tafiti hizo zinaonyesha kuwa ongezeko la watoto wa mitaani kwa kiasi kikubwa linatokana na kuwepo kwa mifarakano, umaskini uliokithiri, janga la UKIMWI na ukosefu wa huduma muhimu katika familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Wizara yangu ikishirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo na ustawi wa mototo imeandaa

Mkakati wa Taifa wa Watoto wakiwemo watoto yatima na walio katika mazingira magumu zaidi. Mkakati huo una lengo la kuhakikisha watoto, hususan watoto yatima na walio katika mazingira magumu zaidi wanapata haki zao za msingi, huduma bora na mahitaji muhimu ili wapate ustawi na maisha bora kama watoto wengine. Aidha mkakati huo una madhumuni ya kuhakikisha kuwa kila mtu kuanzia ngazi ya familia, kijiji, serikali za mitaa na Serikali kuu wanawajibika kuwatunza na kuwapatia watoto malezi na makuzi bora; kuhakikisha kwamba kila inapowezekana watoto wanalelewa ndani ya familia; pamoja na kuhakikisha kuwa watoto wote katika jamii wanazotoka, wanapata haki zote za msingi, kama haki ya elimu, afya, ulinzi, pamoja na haki ya kucheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuboresha hali ya maisha ya watoto hususan katika utoaji wa huduma mbalimbali, Wizara yangu ikishirikiana na wadau mbalimbali wa maswala ya watoto, imeanza mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Watoto Yatima na Walio katika Mazingira Hatarishi *(The Orphans and Most Vulnerable Children Trust Fund)*. Madhumuni ya Mfuko huu ni kuhakikiksha kuwa kundi hili la watoto linapatiwa mahitaji ya msingi kama vile chakula, malazi, mavazi, elimu, huduma za afya na ulinzi. Aidha, mfuko huu utaratibu juhudi za wadau katika uhamasishaji wa rasilimali, mipango na ufuatiliaji na kuhakisha kuwa huduma za mfuko huu zinawafikia walengwa na zinaingizwa katika mipango ya halmashauri ili kuwa endelevu kwa kuboresha hali za maisha ya watoto hao. Vyanzo vya mapato vya mfuko huu vitatoka serikalini, michango ya wadau wa maendeleo, AZISE, sekta binafsi na mapato ya halmashauri na vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2006/07, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wa masuala ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, imeandaa mfumo wa kuratibu utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na taasisi za serikali na zisizo za kiserikali kuhusu malezi na makuzi ya awali ya watoto ambao utasaidia kuboresha na kuimarisha sekta hiyo. Aidha, wizara kwa kushirikiana na sekta zinazoshughulikia masuala ya watoto ilizindua rasmi Taarifa ya mwaka ya Dunia ya utekelezaji wa mpango wa kuwapatia elimu watoto wote ikiwemo elimu ya awali *(Education for All Global Monitoring Report, 2007)* ambayo inazingatia umuhimu wa kuwapatia watoto wadogo huduma bora kama vile lishe bora, elimu ya awali na uchangamshi, matunzo na kulinda afya zao, kama msingi muhimu katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2006/2007, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo na ustawi wa mtoto iliandaa na kuwasilisha katika Umoja wa Mataifa taarifa ya nchi ya miaka mitano ya utekelezaji wa maazimio ya Mkutano Maalum wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kuhusu Watoto uliofanyika New York, Marekani tarehe 8-10 Mei, 2002. Maazimio hayo ni pamoja na utekelezaji wa Mpango wa Waraka wa Matokeo wa Dunia Iwafaayo Watoto *(UN Outcome Document: A World Fit For Children)*. Mpango huo wa utekelezaji ulikuwa unalenga katika kuboresha hali za afya ya watoto, kutoa elimu ya msingi iliyo bora, kupambana na UKIMWI na kuwalinda watoto dhidi ya vitendo viovu vya ukatili, unyanyasaji wa kijinsia, udhalilishwaji na unyonyaji wanavyofanyiwa katika familia na jamii. Aidha, taarifa za awali za utekelezaji wa itifaki za nyongeza za mkataba wa

kimataifa wa haki za mtoto ambazo nchi yetu imeziridhia, ziliandaliwa na kuwasilishwa Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi za wilaya na wakufunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi katika wilaya zote za mikoa ya Ruvuma, Mbeya na Rukwa kuhusu haki za msingi za mtoto ili waweze kufikisha elimu hiyo kwa familia na jamii wanazozihudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji na mila zingine zenye madhara kwa wanawake na watoto wa kike hapa nchini, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na mila zenye madhara hususan ukeketaji. Aidha, Wizara yangu iliandaa mkutano uliowahusisha Makamanda wa Polisi wa Wilaya, Mahakimu wa Wilaya, Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya na Wajumbe wa Sekretariati za Mikoa ya Manyara, Kilimanjaro na Arusha.

Mkutano huu uliowahusisha washiriki 35 ulikuwa maalum kwa kuwalenga Watumiaji na Wasimamizi wa Sheria *(Law enforcers)* zinazozuia ukeketaji pamoja na mila nyingine zenye kuleta madhara kwa wanawake na watoto ili kuhakikisha kuwa sheria zinasimamiwa na kutekelezwa ipasavyo na kujadili mbinu zitakazowezesha watumiaji na wasimamiaji kutekeleza wajibu wao hususan katika Sheria ya Makosa ya Kujamiana ya mwaka 1998.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya majukumu ya Wizara yangu ni kusimamia na kuratibu maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani ambayo huadhimishwa kila tarehe 15 Mei ya kila mwaka na Siku ya Mtoto wa Afrika ambayo huadhimishwa barani Afrika tarehe 16 Juni ya kila mwaka. Lengo kuu la Siku ya Familia Duniani ni kuifahamisha jamii hususan familia zenyewe kuhusu nafasi na umuhimu wao kama kitovu cha maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla. Aidha, katika siku ya Mtoto wa Afrika, Serikali na jamii hupata fursa ya kutafakari kwa kina matatizo mbalimbali yanayowakabili watoto na kujaribu kuyapatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2007, wizara yangu iliratibu maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani ambapo kaulimbiu ilikuwa jamii ziwajibike kwa malezi bora ya watoto. Lengo la kaulimbiu hii ni kuhamasisha, kushawishi na kuhimiza wazazi/walezi na wanafamilia kwa ujumla kuwapa malezi bora watoto wakiwemo watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi. Kaulimbiu ya Siku ya Mtoto wa Afrika ambayo maadhimisho yake yalifanyika kitaifa hapa Dodoma ilikuwa ni AFYA BORA KWA MTOTO NI MSINGI WA MAENDELEO. Lengo kuu la kaulimbiu hii ni kusisitiza juu ya umuhimu wa afya bora kwa watoto ili waweze kukua vizuri kiakili, kimwili na kimaadili hadi utu uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/07, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto-UNICEF, iliendelea kusaidia Mtandao wa Harakati za Watoto *(Tanzania Movement for and with Children)* na Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa ushauri na

kugharamia mikutano yao. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wakiwemo watoto na vijana iliandaa mwongozo wa mbinu shirikishi kwa ajili ya kukuza dhana ya ushiriki wa watoto nchini Tanzania. Lengo ni kuwapa watoto fursa katika masuala yanayowagusa, kusikilizwa na kufahamu kwamba yale wanayoyasema yanapewa uzito na kuzingatiwa katika mipango ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika yasiyo ya Kiserikali, Wizara yangu inalo jukumu la kuratibu na kufuatilia utendaji na utekelezaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* nchini na kuhakikisha mazingira bora kwa Mashirika hayo *(NGOs)* ili yaweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Jukumu hili linatekelezwa kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya *NGOs* ya mwaka 2001 na Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Wizara yangu iliendelea na mchakato wa kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001, Sheria ya *NGOs* Na. 24/2002 na kanuni za utekelezaji wake za mwaka 2004. Aidha, katika kuhimiza usajili wa *NGOs,* kupunguza urasimu na kufuatilia utendaji kazi wake, Wizara yangu iliimarisha ushirikiano na Wasajili Wasaidizi wa *NGOs* katika ngazi za Wilaya na Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002, Wizara yangu inasimamia vyombo viwili vya Kitaifa ambavyo ni Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs* na Baraza la Taifa la *NGOs.* Vyombo hivi vinalo jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba sekta ya *NGOs* nchini inawajibika vema na kujenga msingi wa kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Wizara yangu iliwezesha Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs* kufanya vikao 4 vya kisheria, kutembelea na kufanya kaguzi za shughuli za *NGOs* katika mkoa wa Morogoro. Aidha, hadi kufikia mwezi Juni 2007, Bodi imepitisha, kuhakiki na kuidhinisha maombi 1,674 ya Usajili wa *NGOs* na Cheti cha Ukubalifu. Kati ya idadi hii *NGOs 336* ni za Kiwilaya, 237. Kimkoa, 1,017 Kitaifa, na 84 Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuzingatia uboreshaji wa upatikanaji wa takwimu sahihi za Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara yangu imeendelea kuboresha na kuimarisha Benki ya Takwimu ya *NGOs* kwa kuweka utaratibu wa kuainisha maeneo ya kazi kisekta na kimkoa ili kurahisisha uratibu na ufuatiliaji. Benki hii inatoa mwongozo sahihi wa takwimu za *NGOs* ambazo zimesajiliwa chini ya Sheria Na. 24/2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya CCM ya mwaka 2000, imeweka bayana suala la uwazi na uwajibikaji katika Sekta mbalimbali nchini. Wizara yangu imeendelea kutumia taratibu za Kisheria kufuatilia na kukusanya taarifa za utekelezaji kazi wa *NGOs,* kuzichambua kikamilifu ili kuongeza uwazi na uwajibikaji miongoni mwa wadau wa sekta hii. Taarifa hizi zimesadia sana katika kupima ufanisi wa *NGOs* na mchango wao katika Maendeleo ya Taifa.

Aidha, pamoja na jitihada za kukusanya taarifa hizi bado kuna changamoto kubwa katika kupata takwimu kamilifu na sahihi za *NGOs* nchini kwa kuwa si mashirika yote yenye sifa za *NGOs* yamejisajili chini ya Sheria ya *NGOs.* Hili ni eneo ambalo linahitaji jitihada za pamoja kitaifa ili kuwepo na Benki ya Takwimu moja ya *NGOs* zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti., Sera na Mipango. Wizara yangu imedurusu Sera ya Maendeleo ya Mtoto na kuiwasilisha Serikalini kwa hatua zaidi. Pia Wizara imedurusu Sera ya Maendeleo ya Jamii na kukamilisha rasimu ya kwanza. Kazi hii imeiwezesha wizara kubaini masuala mapya ambayo katika sera za awali hayakujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006/07, Wizara yangu imetoa elimu ya namna ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na UKIMWI mahala pa kazi kwa Viongozi; Wakuu wa vyuo vya Maendeleo ya Jamii; Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi; pamoja na Maafisa Waandamizi wa Wizara. Katika mafunzo hayo yaliyotolewa Jijini Mbeya, mwezi Julai, 2006, Moshi Desemba 2006 na Shinyanga mwezi Januari 2007, mada mbalimbali zilitolewa na kujadiliwa na washiriki pamoja na kuweka mikakati ya kulikabili janga hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeanza kukusanya takwimu muhimu kwa ajili ya kuweka kwenye mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini Unaozingatia Jinsia *(Computerized Gender Sensitive, Monitoring and Evaluation System).* Takwimu hizi zitaufanya mfumo huu uweze kutumika ipasavyo. Wizara pia, imeendelea kuweka kumbukumbu muhimu zinazohusu wanawake, watoto, maendeleo ya jamii na jinsia kwenye tovuti ya Wizara ili ziweze kusomwa na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala na Utumishi, malengo ya Idara ya Utawala na Utumishi ni kuendeleza na kusimamia utendaji kazi wizarani kwa misingi ya Haki, Usawa, Uadilifu, Utawala Bora na Uwazi ikizingatiwa kuweka mkazo katika kudhibiti vitendo vya rushwa na uzembe kazini. Masuala haya ni ya msingi katika kuiwezesha Wizara kuwa na watumishi waadilifu na wanaowajibika, wenye ari, moyo, na msimamo thabiti kuhusu utumishi wa umma na walio tayari kutoa huduma bora kwa umma wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2005/2006, nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imekamilisha Mpango wa kuendeleza rasilimali watu na kwamba utekelezaji wake ungeanza katika mwaka wa fedha 2006/2007. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa utekelezaji wa mpango huu umeanza na jumla ya watumishi 130 wamepatiwa mafunzo ndani na nje ya nchi. Naishukuru Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kupitia Mfuko wa Kuboresha Ufanisi *(Performance Improvement Fund),* kwa kutuwezesha kufikia malengo ya mafunzo ambayo Wizara iliyojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu sasa, Wizara yangu imekuwa ikikabiliwa na upungufu mkubwa wa Watumishi hasa katika vyuo vyake vya Maendeleo ya Jamii na vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Nafarijika kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara yangu imeajiri jumla ya watumishi 98.

Idadi hii imesaidia kupunguza pengo kubwa lililopo kati ya mahitaji halisi ya watumishi na watumishi waliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara imefanya marekebisho ya Muundo wa Utumishi wa kada zilizo chini yake kwa lengo la kuziboresha na kuongeza zilizokuwa hazipo ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu, ikishirikiana na Wizara ya Ajira, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ya Serikali ya Zanzibar, iliandaa mkutano wa mashirikiano ambao ulishirikisha Watendaji Wakuu na maafisa wa ngazi za juu kutoka Wizara hizi uliofanyika Dar es Salaam tarehe 18.01.2007. Maazimio yaliyofikiwa katika mkutano huo yanaendeleza dhana ya ushirikiano wa karibu katika harakati za kuwaletea maendeleo endelevu wananchi wa pande zote mbili za Muungano kwa kuzingatia usawa wa Jinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ilikuwa ikikabiliwa na changamoto kubwa la ukosefu wa takwimu sahihi za watumishi ambao wengi wao wapo katika vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara yangu imekamilisha zoezi la kukusanya takwimu na kuzihifadhi kwenye kompyuta kwa matumizi mbalimbali ya kiofisi. Katika mwaka wa fedha 2006/07, Wizara yangu imeendelea kukiimarisha kitengo cha habari kwa kuwapatia mafunzo kazini wataalam wa Kitengo hiki.

MheshimiwaMwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara yangu iliitisha Kikao cha Baraza la Wafanyakazi Jijini Dar es Salaam tarehe 22- 23 Mei, 2007 ili kujadili masuala mbalimbali yanayohusu utendaji kazi na ustawi wa watumishi. Aidha, katika kikao hicho wajumbe walipata fursa ya kuijadili na kupitisha Bajeti ya Wizara ya mwaka 2007/2008 na rasimu ya Miundo ya Kada zilizo chini ya Wizara inayolenga kuifanya Miundo hiyo iende na wakati pamoja na kuondoa dosari zilizopo katika Miundo inayotumika hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu, katika mwaka 2006/07, imeendelea kufanya ukaguzi wa kina wa mahesabu na ugavi kuanzia Makao Makuu ya Wizara hadi katika vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Wananchi. Lengo ni kuhakikisha kuwa Sheria ya Fedha na Sheria ya Manunuzi ya Umma zinafuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo na malengo ya bajeti ya mwaka 2007/2008 maendeleo ya jamii. Kutokana na uamuzi wa Serikali wa kurejesha Majumba ya Maendeleo katika matumizi yake ya awali, natoa rai kwenu Waheshimiwa Wabunge na Halmashauri zote nchini kutekeleza uamuzi huo wa Serikali ili huduma hizi za Majumba ya Maendeleo ziweze kupatikana kwa wananchi mapema iwezekanavyo. Aidha pale ambapo majumba hayo hayapo itakuwa vyema iwapo uongozi wa Halmashauri utaamua kujenga Majumba ya Maendeleo mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendesha mafunzo ya rejea kwa Wataalam wa Maendeleo ya Jamii na Mafundi Sanifu wa Maendeleo ya Jamii kwa lengo la kuimarisha taaluma na ushiriki wa wananchi katika maendeleo yao. Mafunzo hayo yatahusu uandishi wa miradi shirikishi, matumizi ya teknolojia sahihi na masuala ya ushawishi *(advocacy).* Aidha, Wizara yangu itaendelea kuwaendeleza kitaaluma wataalamu wa Maendeleo ya Jamii wa ngazi ya Cheti ili waweze kufikia hatua ya ngazi ya Stashahada ya Juu ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 200720/08 Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo kwa wanachuo 1,120 kwenye taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika Vyuo vya Tengeru, Buhare, Missungwi na Rungemba. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya stadi mbali mbali kwa wananchi wapatao 30,000 kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 58.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha utendaji katika Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Wizara yangu itaendesha Mkutano Mkuu wa Mwaka utakaowajumuisha wadau mbali mbali wa sekta wakiwemo Watendaji wakuu 19 wa Wizara, Washauri wa Kisekta wa Maendeleo ya Jamii katika Sekretarieti za Mikoa, Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya na Wakuu wa Vyuo vyote 62 vya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2007/2008, ili kuboresha mazingira ya kufundishia katika vyuo 62 vilivyo chini ya Wizara, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vifuatavyo vitafanyiwa ukarabati:- Kanda ya Pwani – Ikwiriri (Rufiji), Ifakara (Kilombero) na Kusini – Chilala (Lindi), Masasi (Masasi), Newala (Newala), Nandembo (Tunduru) na Mbinga (Mbinga mjini), Nyanda za Juu Kusini – Msaginya (Mpanda), Ruaha (Iringa mjini), Njombe (Njombe) na Uyole (Mbeya mjini). Kanda ya Magharibi – Buhangija (Shinyanga mjini), Malampaka (Maswa), Kanda ya Ziwa – Gera (Bukoba vijijini), Malya (Kwimba), Musoma (Musoma mjini), Tarime (Tarime). Kanda ya Kaskazini – Monduli (Monduli). Mamtukuna (Rombo vijijini) na Handeni (Handeni). Kanda ya Kati – Chisalu (Mpwapwa) na Singida (Singida mjini). Aidha, Majengo na miundombinu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Tengeru, Buhare, Missungwi na Rungemba vitaendelea kufanyiwa ukarabati na upanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuondoa matatizo ya migogoro ya mipaka, Wizara yangu itaendelea na mchakato wa kuvipatia hatimiliki Vyuo vifuatavyo;- Bariadi, Bigwa, Mbinga; Chisalu; Handeni; Ikwiriri; Kilwa Masoko; Kiwanda; Mabughai; Malampaka; Malya; Mtawanya; Munguri; Mwanva; Sengerema; Urambo na Uyole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya jinsia. Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo kuhusu jinsia na namna ya kuingiza masuala ya jinsia katika mipango, sera na mikakati mbalimbali ya maendeleo kwa watendaji wa Dawati la Jinsia wa Halmashauri za mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Tabora na Kagera. Vile vile, Wizara itaendelea kushiriki na kuiwakilisha nchi katika mikutano ya kimataifa, kikanda inayohusu maendeleo ya wanawake na jinsia ili kutekeleza maamuzi mbalimbali yanayotolewa katika mikutano hiyo kwa kushirikiana na wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwawezesha wanawake kiuchumi, Wizara itaendeleza mikakati na programu mbalimbali ili kufanikisha azma hiyo. Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake katika Halmashauri. Katika azma ya kuwawezesha wanawake kiuchumi, Wizara itaendelea kuhamasisha wanawake na kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali kabla ya kupewa mikopo ili kuboresha uendeshaji wa biashara zao na marejesho ya mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau kuwawezesha wanawake kushiriki katika maonesho ya biashara ya ndani na nje ya nchi. Mchakato wa uwezeshaji wa Uanzishwaji wa Benki ya Wanawake unaendelea. Benki imekwishasajiliwa kwa jina la Benki ya Wanawake Tanzania na kufungua Akaunti ya *ASCROW*. Wizara yangu itaendelea kuhamasisha ununuzi wa hisa kwa kuzingatia mkakati wa muda mrefu na mfupi ulioandaliwa na mtaalam mwelekezi. Lengo ni kuiwezesha benki kukusanya bilioni sita (6) kwa ajili ya kuanzisha matawi katika mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Sheria na Katiba itaendelea kupitia sheria mbalimbali ili kuzirekebisha zile zinazowanyima wanawake haki. Aidha, Wizara yangu kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii itawahamasisha viongozi na wananchi hususan wanawake kuhusu sheria za makosa ya kujamiiana (1998), Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi ya Vijiji (1999).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto vinatokomezwa, Wizara yangu itatoa mafunzo kwa Maafisa 303 wa Serikali wanaosimamia utekelezaji wa sheria na upatikanaji wa haki katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya mototo, Wizara yangu imepewa jukumu la kuandaa, kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto Tanzania na Sera ya Maendeleo ya Familia kwa lengo la kuboresha maisha ya watoto wote na familia kwa ujumla. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo na ustawi wa watoto, itaendelea kuboresha Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto. Uandaaji wa mkakati huu wa utekelezaji wa sera hii utawawezesha watekelezaji walioainishwa kutekeleza wajibu na majukumu yao kulingana na hoja na matamko ya sera yaliyopewa kipaumbele kwa ufanisi zaidi. Halikadhalika, mkakati huu utasaidia katika kupima na kutathmini mafanikio na matatizo ya utekelezaji wa sera, kurekebisha na kutafuta ufumbuzi wa matatizo yatakayojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilvyoeleza hapo awali kuhusu uanzishwaji wa Mfuko wa kusaidia watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi, Wizara yangu katika kipindi cha 2007/08 itaandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu uanzishwaji wa mfuko huo ili uweze kutambuliwa na kuendeshwa kisheria. Aidha, wizara itasaidia kuhakikisha kuwa mfuko huu unaingizwa *(mainstreamed)* katika mipango ya maendeleo ya Taifa katika ngazi mbalimbali za utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunaelewa kuwa malezi bora ya awali ya mtoto ni msingi wa maisha ya mwanadamu yeyote. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, itakuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kanda ya Kusini mwa Afrika utakaofanyika mwezi Septemba, 2007.

Mkutano huu utajadili utekelezaji wa Ripoti ya Dunia ya Elimu kwa Wote *(Education for all Global Monitoring) ya* mwaka 2007. Ujumbe wa mkutano huo utakuwa Malezi ya Awali ya Watoto ni msingi wa Maendeleo. Mkutano huu unafanyika kufuatia makubaliano ya Mkutano wa Kanda ya Afrika uliofanyika Dakar Senegal mwezi Novemba 2006 ambapo Ripoti hiyo ilizinduliwa rasmi kwa nchi za Afrika.

Vile vile, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto *(UNICEF)* na wadau wengine itaendelea kukamilisha Mkakati wa Taifa wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto. Mkakati huu utaainisha majukumu ya kila mdau katika kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutekeleza Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Kudhibiti Ukeketaji (2001 hadi 2015) wa wanawake na watoto wa kike, Serikali kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za kijamii itaendelea kuelimisha jamii na kupiga vita mila na desturi zenye madhara hususan kwa wanawake na watoto wa kike. Aidha, Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa watumiaji na wasimamiaji wa sheria mbalimbali zinazozuia ukeketaji hapa nchini na kuhakikisha haki inatendeka na wale wote wanaoendelea kufanya vitendo viovu wanapatiwa adhabu zinazostahili kwa mujibu wa sheria. Vilevile, Wizara yangu itaendelea kutoa elimu ya idadi ya watu na maisha ya familia kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii 260 wa Halmashauri ili waweze kusambaza elimu hiyo kwa familia na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na wimbi la ongezeko la vitendo viovu vya ukatili, unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto katika familia na jamii. Kwa kupitia Bunge lako tukufu napenda kukemea vitendo hivyo na wale wote wanaohusika na vitendo hivyo kuacha mara moja ili kuhakikisha watoto wetu wanakua katika malezi bora na kuishi kwa amani katika jamii. Aidha, napenda pia kuwakumbusha wale wote wanaohusika kusimamia sheria, kutekeleza wajibu wao na kuwachukulia hatua kali kwa mujibu wa sheria za nchi wale wote watakaobainika kufanya vitendo hivyo. Katika kipindi cha mwaka 2007/08. Serikali kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuandaa na kutekeleza mikakati na programu mbalimbali za kuwalinda watoto dhidi ya vitendo viovu vya ukatili, unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia. Vile vile, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri itaendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya haki za msingi za watoto, wajibu wa familia katika kuboresha malezi na makuzi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2007/08, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ya watoto wakiwemo watoto wenyewe, itaendelea kutoa mafunzo na kusambaza zana za ushirikishwaji wa watoto *(child participatory tool kit)* kuhusu mbinu shirikishi. Mbinu hizi zitawajengea uwezo watoto tangu utotoni na kuwapatia fursa ya kutoa mawazo ambayo yatasaidia kuzingatiwa katika

mchakato mzima wa uandaaji wa sera, mipango na programu mbalimbali za maendeleo ya taifa zikiwemo za maendeleo yao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika yasiyo ya kiserikali, Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inao wajibu mkubwa wa kushiriki katika kuharakisha maendeleo ya watanzania ili kufikia malengo ya MKUKUTA na yale ya Milenia. Katika mwaka 2007/08, Wizara yangu itaendelea na jukumu la kuratibu shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini, kuweka mazingira bora yatakayowezesha Mashirika haya kujiendesha vizuri na kwa ufanisi ili kuleta mabadiliko chanya ya kiuchumi na kijamii. Aidha, jitihada zitaelekezwa katika kuhimiza *NGOs* kushirikiana kikamilifu na Serikali na wadau wengine ili kujenga jamii bora ya watanzania kiuchumi na kijamii hususan katika utekelezaji wa Mpango wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA), malengo ya milenia na *MKUKUTA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Kanuni za Maadili za *NGOs* ni muhimu sana katika kuimarisha moyo wa kujituma na mashirikiano kati ya *NGO*s na Serikali*, NGOs* wenyewe na kati ya NGOs na jamii kwa ujumla nchini. Mkazo mkubwa utakuwa hasa katika kuhakikisha kwamba Baraza la Taifa la NGOs linakamilisha kanuni hizi na kusimamia utekelezaji wake. Katika kufanikisha lengo hili Wizara yangu, itafuatilia kwa karibu zaidi taarifa za Mashirika hayo na kuendelea kutoa ushauri wa kitaalamu ili kuwezesha Mashirika haya kutandaa katika Mikoa mingi zaidi hususan katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuleta moyo wa ushindani miongoni mwa *NGOs* tunatarajia kuanzisha utaratibu wa kuibua miradi inayotekelezwa na *NGOs* kwa ufanisi mkubwa *(best practices)* na kuitangaza kitaifa ili iwe mifano ya kuigwa na wadau wengine. Ili kufanikisha suala hili Baraza la Taifa la *NGOs* linatakiwa kuwa mstari wa mbele kwa kushirikiana na Serikali kukusanya taarifa za *NGOs* kuzichambua na kuziingiza kwenye Tovuti ya Taifa ili wadau wa kitaifa na kimataifa waweze kujifunzia. Ili kutekeleza kazi hii kwa ufanisi itabidi kuwa na vigezo ambavyo vitatambuliwa na wadau wote wa sekta hii na kuwa na utaratibu maalum na wazi wa kuhakiki na kutoa tathmini ya matokeo bora ya utekelezaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi za Wilaya, Mikoa na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya *NGOs Na*. 24 ya mwaka 2002 ndiyo Sheria pekee nchini yenye kusajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini. Uzoefu umeonyesha kuwa uelewa wa wadau wengi kuhusu Sheria hii na kanuni zake bado ni mdogo hasa katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na Vijiji. Eneo hili linahitaji jitihada nyingi na hasa kushirikiana na wadau katika kujenga weledi wa wadau ili kurahisisha usajili wa *NGOs* katika maeneo husika. Aidha, jitihada zitaelekezwa katika kuwajengea uwezo Wasajili Wasaidizi ili waweze kutoa huduma nzuri na sahihi kwa wananchi na kurahisisha usajili na ufuatiliaji wa shughuli za NGOs katika maeneo yao. Ili kufanikisha zoezi hili, Wizara yangu, inatarajia kuwapatia mafunzo maalumu Maafisa Maendeleo ya Jamii na kuwateua rasmi kuwa Wasajili Wasaidizi wa NGOs kwa kuwa wanao uzoefu mkubwa katika kuhamasisha na kushirikisha wananchi katika sekta zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendeshaji wa NGOs nyingi nchini umejikita katika kutegemea misaada ya wafadhili kwa kiwango kikubwa. Katika kipindi cha mwaka 2007/08. Wizara yangu itaendelea kuhamasisha Taasisi, Asasi na Wafadhili mbalimbali nchini kujikita katika kuwajengea uwezo sekta ya NGOs katika kutumia Rasilimali na fursa zilizomo hapa nchini katika kujiendesha na kutekeleza majukumu yao. Kimsingi NGOs wanatakiwa kutengeneza faida isipokuwa wasitumie faida hiyo kugawana kama gawio (dividends) bali zitumike katika kutekeleza malengo waliyojiwekea. Iwapo NGOs watajijengea utaratibu wa kutengeneza vyanzo vya fedha vya hapa nchini itawapunguzia kwa kiwango kikubwa utegemezi kwa wafadhili, kuwajengea uendelevu na heshima kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera na Mipango. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itakamilisha kudurusu Sera ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996 na kuiwasilisha Serikalini kwa hatua zaidi. Aidha zoezi la kudurusu Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000 litaanza. Madhumuni ya kurekebisha sera hizi ni kuingiza masuala mapya yaliyojitokeza yanayohusu maendeleo ya jamii, wanawake na jinsia.Katika harakati za kupambana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI sehemu za kazi, katika mwaka wa fedha 2007/08, wizara itaendesha mafunzo kwa watumishi kuhusu jinsia katika Sera, na UKIMWI ambayo yatawaongezea watumishi uelewa wa namna ya kupanga mikakati na mbinu za kupambana na maambukizi ya UKIMWI sehemu za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inaendelea kukusanya takwimu muhimu kwa ajili ya kuweka kwenye mfumo wa ufuatiliaji wa tathmini inayozingatia Jinsia *(Computerized Gender Sensitive Monitoring and Evaluation System).* Takwimu hizi zitaufanya mfumo huu uweze kutumika ipasavyo. Wizara pia, itaendelea na kazi ya kuweka kumbukumbu muhimu zinazohusu wanawake, watoto, jinsia na maendeleo ya jamii kwa ujumla kwenye tovuti ya Wizara ili ziweze kusomwa na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imepanga mkakati wa kufuatilia na kutathimini miradi inayotekelezwa Wizara na katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na vya Maendeleo ya Jamii ili kuleta ufanisi katika matumizi ya fedha na mafanikio ya miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala na Utumishi, katika mwaka wa fedha 2007/08, Wizara yangu itaendelea kujenga mazingira mazuri ya kazi, yanayozingatia haki na usawa ambayo yataendeleza na kuwahamasisha watumishi wa Wizara kufanya kazi kwa bidii na kwa kujituma ili watoe huduma bora kwa misingi ya Utawala Bora, Uwazi na Uwajibikaji hivyo kuendeleza mafanikio yaliyopatikana tangu Serikali ya Awamu ya Nne ilipoingia madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia mojawapo ya kuongeza utaalam wa mtumishi ni kumpa mafunzo, kumuwezesha kupata utaalam na mbinu za kisasa zitakazomwezesha kufanya kazi yake kwa ufanisi. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2007/08, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo kwa kuzingatia Mpango wa Kuendeleza Rasilimali Watu ambao umeanza kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Wizara yangu inatarajia kuajiri watumishi 172 kutokana na ikama ya watumishi wapya tuliyoidhinishiwa. Upatikanaji wa watumishi hawa, ambao wengi wao watapelekwa vyuoni, utapunguza uwiano mkubwa uliopo kati ya wakufunzi na wanavyuo. Aidha, vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vitakuwa na uwezo zaidi wa kuwafikia na kuwapa stadi mbalimbali za maisha wananchi wanaovizunguka vyuo ambao ndiyo walengwa wakubwa wa mafunzo ya nje ya chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Wizara yangu inatarajia kuwaelimisha watumishi juu ya Mkataba wa Utoaji Huduma ambao una lengo la kujenga misingi thabiti ya kutoa huduma kwa wananchi na kuondoa ubabaishaji katika utoaji wa huduma hizo. Aidha, Wizara itafanya jitihada za makusudi kuhakikisha kuwa wananchi wanaelewa huduma tuzitoazo, namna ya kuzipata huduma hizo, wajibu wao katika kuzipata na namna ya kulalamika pale ambapo hawapati huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Nne imeweka mkazo mkubwa katika kulinda, kudumisha, kuendeleza na kuimarisha Muungano wetu. Katika mwaka 2007/08, Wizara yangu pamoja na Wizara ya Ajira, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ya Serikali ya Zanzibar zitaendelea na utaratibu tuliojiwekea wa kuwa na mikutano miwili ya mashirikiano kwa kila mwaka. Mikutano ya awali imeweka dira ya mashirikiano zaidi katika maeneo ya Sera, Miongozo na maadhimisho mbalimbali ya Siku ya Wanawake Duniani, Siku ya Familia na Siku ya Mtoto wa Afrika. Ni matarajio yangu kuwa kwa kuongeza kasi ya ushirikiano wetu, Wizara hizi za pande mbili za Muungano zitaunda timu imara ya kuwahamasisha wananchi kujiletea maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya Utawala Bora inasisitiza utamaduni wa kuwa na vikao vya mara kwa mara ili kujenga mahusiano mazuri ya kiutendaji na kutatua migogoro yoyote inayoweza kukwaza ufanisi kazini. Katika mwaka 2007/08, Wizara itaendelea kuwa na Vikao vya Baraza la Wafanyakazi mara mbili kwa mwaka kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Serikali ya Awamu ya Nne imeweka mazingira mazuri ya ushiriki wa sekta binafsi katika kuleta maendeleo ya nchi. Wizara yangu itaendelea kuzishirikisha Sekta Binafsi katika utoaji wa huduma za ulinzi wa ofisi pamoja na usafi wa ofisi na mazingira katika Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kama ilivyoelezwa katika hotuba zilizopita za Bajeti ya Wizara yangu kwamba Wizara hii ni mtambuka. Kwa mantiki hii, tutaendelea kuhitaji ushirikiano wa karibu sana na wadau wetu mbalimbali ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Lengo kubwa ni kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika jamii, na hivyo kuondoa umaskini na kuleta maisha bora kwa watu wote. Aidha, ushirikiano baina ya Wizara pamoja na Halmashauri ni muhimu sana katika kufanikisha malengo ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi na shukrani, baada ya kueleza hayo, naomba kuchukua nafasi hii, kumshukuru Mhe. Naibu Waziri, Salome Joseph Mbatia (Mb.), kwa ushirikiano wake. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mariam J. Mwaffisi, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watumishi wote wa Wizara yangu katika ngazi zote kwa ushirikiano na moyo waliouonyesha, hususan katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza hotuba yangu, sina budi kuwashukuru wale wote ambao tumekuwa tukishirikiana nao kwa njia moja au nyingine katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Naomba kutumia fursa hii na kwa kupitia Bunge lako tukufu kutoa shukrani zangu za dhati, kwa wafuatao:-

Shirika la Mtandao wa Jinsia Tanzania *(TGNP),* Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Shirikisho la Vyama vya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (FAWETA), Chama cha Wanawake Viongozi katika Kilimo na Mazingira Tanzania (TAWLAE), Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA), Plan International, Makampuni ya ndani, Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote *(EOTF),* Wanawake na Maendeleo (WAMA), Mashirika mbalimbali pamoja na wale wote tunaoshirikiana nao katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa manufaa ya jamii na Taifa zima kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru wahisani mbalimbali ambao wameendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kugharamia miradi mbalimbali nchini inayotekelezwa na Wizara yangu. Wahisani hao ni Serikali za Canada, Ireland, Italia, Netherlands, Norway na Sweden ambao wanaendelea kutusaidia kwa kupitia mashirika yao ya kimataifa; Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto *(UNICEF),* Benki ya Dunia *(WB),* Shirika la Kazi Duniani *(ILO),* Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu *(UNFPA),* Mfuko wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia Maendeleo ya Wanawake *(UNIFEM),* pamoja na Mashirika mengine ya nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Bajeti ya Wizara, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2007/08, sasa naliomba Bunge lako tukufu liidhinishe matumizi ya jumla ya shs. 10,982,464,000 Kati ya hizo shs.7,121,611,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shs.2,970,975,000 kwa ajili ya mishahara na shs. 4,150,636,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo *(Other Charges).* Aidha, kiasi cha shs.3,860,853,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo shs.2,661,000,000 ni fedha za hapa nchini na shs.1,199,853,000 zikiwa ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi na Naibu wako pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha Hotuba ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri tunakushukuru na tunakupongeza kwa hotuba yako. Ingawa nimekuwa nikiwasikia Wabunge wakiuliza huyo ndugu yako wa hiari ni nani mbona hukumtaja? *(Kicheko)*

Kwa hiyo, nafikiri kabla hujaanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge itakuwa vizuri kama utamtaja huyo ndugu yako wa hiari ili na Bunge nalo kwa kweli limpe *support* ya kuendelea kuku-*support* wewe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sasa naomba nimwite Msemaji wa Kamati, Mheshimiwa Kyendesya, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Mheshimiwa Kyendesya, Mbunge wa Viti Maalum tafadhali. *(Makofi)*

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, naomba kusoma Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto katika mwaka wa fedha 2006/2007 pamoja na maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo, kwa mwaka wa 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawasilisha mapendekezo haya ya Kamati naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana na wanawake wote wa Mkoa wa Mbeya kwa kuniunga mkono kunipa moyo na hatimaye kuweza kuwa mwakilishi wao Bungeni. Naahidi kuwatumikia kwa moyo mnyenyekevu mkubwa. *(Mkubwa)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 81(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, nachukuwa nafasi hii kukushukuru wewe kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya aliyekuwa mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Marehemu alijitolea katika mambo mengi muhimu ya jamii, likiwemo suala la kupambana na madawa ya kulevya, kusomesha watoto yatima na kuisaidia kwa hali na mali Timu ya Soka ya Taifa, mambo yaliyokuwa chini ya usimamizi wa Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marehemu Mheshimiwa Amina ameondoka lakini tuna imani vita alivyovianzisha vitaendelea kudumu na kuendelezwa na wanakamati wote. Marehemu ameondoka duniani akiwa shujaa, Mwenyezi Mungu ailaze roho yake Mahali Pema Peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii ambao ndio waliochambua Bajeti hii nao ni-:

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa. Fatma Othman Ally, Mheshimiwa Ameir A. Ameir, Mheshimiwa Zulekha Y. Haji, Mheshimiwa Issa K. Issa, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mhesihmiwa Kapt. John Komba, Mheshimiwa Maulidah Anna Komu, Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Kiumbwa M. Mbaraka, Mohamed A. Said, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Elitha N. Switi, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Benadeta Mushashu, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Khalifan A. Salim, Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 4 Juni, 2007, Mjini Dar- Es Salaam, Kamati ilifanya kikao na Wizara na kupata maelezo ya kina toka kwa Mheshimiwa Sofia Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Salome Mbatia, Naibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara. Timu hiyo ilielezea kwa kina kuhusu Dira na Muundo wa Wizara, Utekelezaji wa Maoni, Mapendekezo na Maagizo ya Kamati kwa Mwaka wa fedha 2006/2007. Mafanikio na Changamoto au Matatizo ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo katika kipindi cha mwaka 2006/2007. Aidha Kamati ilipata maelezo ya Maombi ya Fedha za Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maoni, mapendekezo na maagizo ya Kamati kwa mwaka 2006/2007, katika mwaka wa fedha uliopita, Kamati yetu ilitoa maoni na mapendekezo katika maeneo mbalimbali hasa yanayohusu mambo yafuatayo:-

(i) Kuimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi,

(ii) Upungufu wa Watumishi Katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto,

(iii) Pia Serikali kuweka Kumbukumbu za Taasisi Zisizo za Kiserikali mahali zilipo na namna zinavyosaidia kuleta Maendeleo kwa Jamii,

(iv) Pia namna ya kuimarisha Vituo vya Watoto Yatima na Watoto Waishio katika Mazingira Hatarishi; na

(v) Mikakati ya kupunguza Riba kubwa ya Mikopo kwa lengo la kuwawezesha Wanawake Kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, Wizara kwa kiasi kikubwa imeyafanyia kazi baadhi ya maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana.

Hata hivyo, katika maeneo ambayo Kamati imeona juhudi zaidi zinahitajika imeshauri ipasavyo. Mafanikio katika utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2006/2007.

Katika Mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 10.4 bilioni. Waziri alituelezea kwa undani kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2006/2007, mafanikio haya ni pamoja na

Wizara imeandaa Waraka kuhusu Mapendekezo ya Kuimarisha Sekta ya Jamii, Waraka huo ulipitishwa na Baraza la Mawaziri mwezi Machi, 2007.

Pia Serikali imevifanyia ukarabati wa majengo na miundombinu vyuo vya Buhare na Rungemba. Chuo cha Tengeru kinaendelea na ujenzi wa ukumbi wa mihadhara.

Vile vile mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake wanaoishi na virusi vya UKIMWI yametolewa kwa wanawake 200 kutoka mikoa yote Tanzania Bara. Aidha, mafunzo kuhusu kuzuia na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake mafunzo hayo yamefanyika kwa wasimamizi wa sheria 100.

Wizara imefanya maandalizi karibu yote ya kuanzisha Benki ya Wanawake na yaliyobaki yanaendelea vizuri.

Pia Wizara imekuwa ikiratibu Mashirika yasiyo ya Kiserikali ambapo hadi Juni, 2007 yapo Mashirika yasiokuwa ya Kiserikali yapatao 1,600 ambayo yamesajiliwa chini ya sheria ya *NGOs No. 24* ya mwaka 2002. Kati ya mashirika hayo yapo ya kitaifa, kimataifa, kimkoa na ya kiwilaya pia Wizara imedurusu Sera ya Maendeleo ya Mtoto na imeshafikishwa Serikalini kwa hatua zaidi.

Aidha, Sera ya Maendeleo ya Jamii imedurusiwa na rasimu ya kwanza imekamilika. Pia Mkakati wa kupambana na rushwa katika maeneo yote ya utoaji wa huduma umekamilika . Mkakati huu umeainisha maeneo yanayoweza kutoa mianya kwa watoaji na wapokeaji rushwa na kuyawekea mikakati ya kuziba mianya hiyo ili wananchi wawe na uhakika wa kupata huduma bora kwa wakati

Aidha Wizara ilipangiwa kukusanya shilingi 1.4. bilioni hadi kufikia mwezi Machi, 2007 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 18.9 milioni, haya ni mafanikio makubwa kwa Wizara hii. Kamati iliipongeza Wizara kwa kuitaka kuweka mikakati madhubuti ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali. *(Makofi)*

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto au matatizo katika kutekeleza Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2006/2007, pamoja na mafanikio, Waziri alielezea kwa kina changamoto au matatizo yaliyojitokeza katika kutekeleza bajeti ya Wizara kwa mwaka 2006/2007. Changamoto au matatizo hayo ni pamoja na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, ambavyo vinafundisha taaluma ya maendeleo ya jamii, vina uhaba wa jumla ya wakufunzi 27, sawa na 45% na katika Vyuo

vya Maendeleo ya Wananchi, kuna upungufu wa wakufunzi 356, sawa na 52%. Majengo na miundombinu ya vyuo vingi ambavyo matumizi yake yalibadilishwa kuwa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ni ya zamani, yamechakaa na hayajafanyiwa ukarabati mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hali ya mitambo na vyombo vya usafiri katika vyuo ni mbaya. Upungufu wa watumishi wenye sifa *(Professionals)* na hata baadhi ya waliopo, hawawajibiki ipasavyo hasa katika ngazi ya Mikoa na Halmashauri. Muundo wa Utumishi wa Maendeleo ya Jamii, unatamka kuwepo kwa watumishi wa Maendeleo ya Jamii hadi ngazi ya Kata. Hata hivyo, hawaajiriwi kutokana na baadhi ya Mamlaka kutoona umuhimu wa kuajiri Maafisa hawa na Sekta ya Maendeleo ya Jamii kupewa umuhimu finyu, hususan katika suala la utengaji wa rasilimali fedha na watu. Upo utaratibu wa kuwa na sekta nyeti katika Halmashauri na Serikali Kuu, na ugawaji wa fedha unazingatia unyeti huo. Hali hii imefanya Idara ya Maendeleo ya Jamii au Wizara hii kwa ujumla, kupewa umuhimu finyu katika ugawaji wa rasilimali. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba, Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, wana mchango mkubwa katika kuwezesha sekta hizo nyeti kufikia malengo yao. Vilevile kufifia kwa baadhi ya shughuli za maendeleo ya jamii zilizokuwa zikitambulisha umuhimu wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii. Hivyo, kuna haja ya kufufua programu hizo ili shughuli za maendeleo ya jamii ziweze kutekelezwa.

Aidha, kuna Vyuo vingi vya Maendeleo ya Jamii havitumiki ipasavyo. Wizara imekuwa ikitoa mafunzo katika Chuo chake cha Misungwi kila mwaka, kuhusiana na mafunzo ya ujenzi mdogo mdogo wa Miundombinu kama vile barabara vijijini, madaraja na visima. Ujuzi ambao ulikuwa unatumiwa na Vikosi vya Ujenzi, chini ya Idara ya Maendeleo ya Jamii lakini vikosi hivyo havifanyi kazi tena. Vikosi hivi vilikuwa vikitengeneza ujenzi mdogo mdogo wa madaraja, visima na miradi mbalimbali ya kujitolea. Barabara na madaraja hayo yalionesha ubora wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2007/2008, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2007/2008, inaomba kiasi cha Sh.10,982,464,000. Kati ya hizo, Sh.7,121,611,0007 ni Matumizi ya Kawaida na Sh.3, 860,853,000 Matumizi ya Maendeleo. Aidha, Kamati ilijadili kwa kina, malengo yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi katika mwaka 2007/2008 ya Wizara hii kujadiliwa na Kamati na kupitishwa, Serikali ilitoa maamuzi ya kupunguza bajeti ya kila Wizara kwa asilimia 17, kwa ajili ya kufidia pengo la miundombinu. Wizara hii imepunguziwa kiasi cha Sh.874,000,000. Kamati imeona kwamba, Wizara hii haikutendewa haki kwa kukatwa asilimia 17, kwani kila mwaka Wizara hii inapewa fedha kidogo sana hivyo, ingekuwa busara sana, kiwango cha asilimia kingepunguzwa kwa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushauri na maoni ya Kamati, baada ya kujadili kwa kina utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2007/2008, Kamati ilitoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa ukopeshaji kutoka katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake umekuwa haufanyi kazi kwa ufanisi mkubwa, Kamati inaishauri Serikali iandae Waraka ili fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake zipelekwe katika *SACCOS* zinazotambulika. Halmashauri ziruhusu vikundi vya akina mama kukopa kwenye *SACCOS* hizo, badala ya kupelekwa kwenye Halmashauri zetu

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara imekuwa ikiandaa sera na kuratibu sera hizo; ikiratibu pia utekelezaji wa Mikataba ya Kitaifa na Kimataifa kuhusu haki na ustawi wa watoto na familia; kubaini na kuelimisha jamii kuhusu vidokezo vya mila na desturi zinazozuia ukuaji na ustawi wa mtoto na kupendekeza jinsi ya kurekebisha sheria mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kutunga sheria mpya au kurekebisha za zamani; na kwa kuwa bado suala la watoto linahudumiwa na Wizara mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Halmashauri zetu; hii inaonesha kwamba, Serikali bado haijaonesha kipaumbele cha kutosha kuhusiana na suala la watoto; hivi ni kwa nini utungaji na urekebishwaji wa sheria zinazohusu watoto na wanawake zinachukua muda mrefu sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati inaishauri Wizara kuandaa mikakati ya kutosha ya kuunganisha (*Cordination*) huduma za mtoto, kwani huduma za mtoto kwa hivi sasa zimetupwa tupwa katika wizara mbalimbali, watoto bado hawajahudumiwa kama inavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sheria ni muhimu sana katika kutatua matatizo ya mtoto na kwa kuwa karibu nchi zote za *SADC,* zinazo sheria ya mtoto, Kamati inaishauri Serikali kuandaa Muswada wa Sheria ya Mtoto na kuletwa Bungeni mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwe na vituo vya kulea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi, kuliko kazi hiyo kuachia mashirika na watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii imekuwa inafanya kazi ya kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mashirika yasiyo ya kiserikali na Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002; aidha, kuratibu na kutoa mwongozo kuhusu uendeshaji wa shughuli za Mashirika yasiyo ya Kiserikali na kufuatilia na kufanya kaguzi ya shughuli za *NGOs*; na kwa kuwa *NGOs* nyingi zimekuwa zikifanya kazi kwa ufanisi hafifu na kuna malalamiko makubwa kuhusu matumizi mabaya ya fedha za wafadhili na kutowafikia walengwa: Kamati inaishauri Serikali kudhibiti na kufuatilia utendaji kazi wa *NGOs* hapa nchini; Serikali iangalie uwezekano wa kuunganisha sheria zote zinazohusiana na usajili wa *NGOs* hapa nchini; na Sheria ya *NGOs* ipewe nguvu (meno) katika kufuatilia utekelezaji wa kazi za *NGOs*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imefikia katika hatua nzuri kuhusu uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania; Kamati inaishauri Serikali iendelee na taratibu zote muhimu kukamilisha kazi hiyo na mikakati madhubuti iandaliwe katika utafutaji wa fedha kwa kuuza hisa; na uanzishwaji wa benki uwekewe muda wa kukamilisha benki hiyo *(time framework).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara ina majukumu ya kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii na Mwongozo wa Kuwashirikisha Wananchi katika Mchakato wa Kujiletea Maendeleo na Kueneza Dhana ya Maendeleo ya Jamii kwa Vitendo, lakini bado Sekta ya Maendeleo ya Jamii inakuwa inapewa umuhimu finyu hasa katika utengaji wa rasilimali; na kwa kuwa Wizara imeandaa Waraka wa kuboresha Sekta ya Maendeleo ya Jamii; Kamati inaishauri Serikali kuwaelimisha wananchi kuhusu Waraka huo na kuendelea na mikakati ya kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza Waraka huo; na pia Kamati inaishauri Wizara izidi kushawishi watengeneza sera wengine na waandaaji wa bajeti ili waweze kutoa kipaumbele kinachostahili hasa kifedha na watumishi

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Tengeru, kinakabiliwa na matatizo mengi na tatizo mojawapo ni upungufu wa walimu katika kuendesha kozi fupi fupi; Kamati inaishauri Serikali kuendelea na mikakati ya kuunganisha Chuo cha Tengeru na Chuo cha Mzumbe *(affiliation)* ili kuweza kuondoa tatizo la upungufu wa walimu na kuleta mafanikio ya Chuo cha Tengeru.  Pia Chuo kiendelee na mikakati ya kuboresha mazingira na kuwatumia walimu wa muda katika kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la kukeketwa linapigwa vita sana, semina mbalimbali zimefanyika katika kuwaelimisha wananchi lakini bado suala hilo linaendelea.  Kamati inaishauri Wizara, kuweka mikakati madhubuti na ya namna ya pekee katika kukabiliana na tatizo hilo na vilevil wanaume waelimishwe zaidi kuhusiana na suala hilo.  Mikakati Maalum iandaliwe ya kuwalinda watoto wachanga kukeketwa wakiwa wachanga, mara baada ya kuzaliwa na suala hili liwekewe mikakati ya kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Hazina imekuwa na tabia ya kuchelewa kutoa fedha kwa kutoa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuchelewa kwa makusanyo ya kodi na wafadhili kuchelewa kuleta fedha walizokuwa wameahidi kutoa. Kamati inaishauri HAZINA kuweka mikakati ya kuboresha utendaji wake wa kazi ili ucheleweshaji wa fedha  usiendelee kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Same, kinakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi hasa mhasibu, karibu miaka minane hakuna mhasibu; Kamati inaishauri Wizara na Hazina kuhakikisha kwamba, katika bajeti ya mwaka 2007/2008,  Chuo cha Same anapatikana mhasibu mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara imepata hati yenye mashaka katika mwaka 2005/2006, Kamati inaishauri Wizara kurekebisha mapungufu yake yote ili isiendelee kupata hati yenye mashaka tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mwanaume hawezi kabisa kupika kwa kutumia mafiga matatu ya kupikia, aidha, mwanaume hawezi kabisa kwenda msituni kukata kuni na kubeba kuni hizo kichwani/begani na kuleta nyumbani, lakini teknolojia ikiongezeka mfano jiko la kisasa la kupikia au matoroli ya kisasa ya kubebea mizigo,

mwanaume anaweza kupika na kufurahia kusukuma toroli na wakati huo atakuwa anamsaidia mwanamke; Kamati inaishauri Serikali kuandaa Mkakati Maalum wa kuongeza teknolojia ya kisasa ili kuwavutia wanaume kufanyakazi ya kumsaidia mwanamke. Kamati pia inaishauri Wizara itenge fedha za kutosha katika kuinua teknolojia ya majiko na matoroli ya kubebea mizigo kwa kuanza na wilaya chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, imekuwa ikipewa fedha kidogo kwa kusingizia kwamba, ugawaji wa rasilimali unafuata unyeti wa sekta. Hali hii imeifanya Wizara hii kutopata fedha za kutosha na kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuinua hali ya maisha ya jamii, kuboresha hali ya maisha ya watoto, kuboresha utendaji kazi wa mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* na kadhalika. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kiwango cha juu cha *budget ceiling* ya Wizara hii ili kupatiwa fedha za kutosha kwa ajili ya kuinua teknolojia katika jamii na kuleta maendeleo ya jamii. Vilevile Kamati inaishauri Serikali kwamba, sasa wakati umefika wa kutambua kwamba, Wataalam wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, wana mchango mkubwa katika kuwezesha sekta nyeti kufikia malengo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii ndio yenye jukumu la kuingiza masuala ya jinsia katika Sera, Programu, Mikakati na Mifumo ya Utekelezaji na kuona kwamba, wanawake na wanaume wanakuwepo katika ngazi zote za Serikali, Mashirika ya Umma, Taasisi mbalimbali na wananufaika na maendeleo yao; na kwa kuwa Wizara ndio mratibu wa Mkakati wa kufikia 50:50 na kwa kuwa mchakato huu unahitaji fedha za kutosha; Kamati inaishauri Serikali kuendelea na Mkakati huo ili kufanikisha suala hilo na washirikishwe Wajumbe wa Kamati kikamilifu katika Mkakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara imekuwa ikitoa mafunzo katika Chuo chake cha Misungwi kuhusu ujenzi mdogo mdogo vijijini kila mwaka chini ya Idara ya Maendeleo ya Jamii. Mafunzo hayo siku za nyuma ilikuwa yanatumiwa na Vikosi hivyo kutengeneza ujenzi mdogomdogo wa madaraja, visima na miradi mbalimbali ya kujitolea; Kamati inaishauri Serikali kufufua vikosi vya ujenzi, kwani ni muhimu sana kurudisha vikosi hivi katika muundo wa Halmashauri zetu.

Kwa kuwa upataji wa *tender* kwa vikosi hivi ilikuwa unachukuwa muda mrefu, pamoja na kwamba, ubora wa kazi yao ulikuwa unaonekana wazi; Kamati inashauri baada ya kurudishwa kwa vikosi hivi, utaratibu wa *tender* uangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, inakusudia kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi kila Wilaya hapa nchini kwa ajili ya kuboresha mafunzo ya ufundi:-

(a) Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kuona uwezekano wa kuvifufua Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ambavyo vipo karibu kila Wilaya na vinavyo nyenzo muhimu kwa kuwezesha mafunzo ya ufundi.

(b) Kamati inaishauri Serikali kuboresha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa kuvipatia vitendea kazi na kuboresha miundombinu ili viweze kutumika kwa mafunzo ya elimu ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Sofia M. Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Salome J. Mbatia, Katibu Mkuu, Ndugu Mariam Mwaffisi na Watumishi wote wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia Kamati katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Kamati inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru Wajumbe wenzangu, kwa ushauri na busara zao zilizowezesha kuiongoza Kamati hii. Michango yao kwa wakati wote ilitolewa kwa uwazi na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru kwa dhati, Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka na Katibu wa Kamati hii, Ndugu Lawrence Robert Makigi, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandalizi ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, kwa kusoma hotuba yake vizuri na kuweka msisitizo sana katika maeneo muhimu ya hotuba hiyo. Nilikuwa naomba tu niwatangazie mambo mawili mafupi, kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Kwanza, kabisa tunaona Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, *Chief Whip* hayupo. Waheshimiwa Wabunge naomba niwape taarifa kwamba, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Msaidizi wa *Chief Whip* wa Kambi ya Upinzani, yupo hapa ndani na anashika majukumu yake badala ya Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa.

Lakini nilikuwa naomba tu niwatangazie tu Waheshimiwa Wabunge, ambao watachangia hoja hii ili kama wapo nje ya Ukumbi wa Bunge, basi waweze kurudi hapa ndani na kufanya maandalizi ya kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Ruvuma, atafuatia Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Pemba na msemaji wa tatu atakuwa Mheshimiwa Ali Juma Haji. Kwa hiyo, ningeomba wasemaji hao watatu, waweze kuwa maeneo ya karibu ili tutakapoanza kuchangia hoja hii, wawepo ndani ya Ukumbi wa Bunge.

Baada ya matangazo hayo mawili, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Anna M. Komu, Msemaji wa Kambi ya Upinzani ili aweze kutoa mawazo ya Kambi ya Upinzani katika Hotuba ya Waziri.

**MHE. ANNA M. KOMU - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kutoa shukrani zangu kwa kupata wasaa huu ili kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b), (c) na 81(1), Toleo la 2004, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii, kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa Marehemu Amina Chifupa. Marehemu alikuwa mstari wa mbele kutetea maslahi ya vijana wa Kitanzania na Watanzania kwa ujumla na alikuwa miongoni mwa watu shupavu na wasiogopa kusema ukweli. Namwomba Mwenyezi Mungu, ampe makazi mema. *Amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila, kama sitakishukuru chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na mume wangu Bwana Valerian Komu, kwa ushirikiano ninaoupata katika utendaji kazi. Kama nilivyowaahidi kuwa nitafanya kila lililo ndani ya uwezo wangu, kutimiza majukumu niliyopewa na Watanzania kwa ujumla wake, nitaitunza imani yao kwangu na *inshallah* nitafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Kambi ya Upinzani hapa Bungeni, Kambi imara kabisa na inayofanya kazi kwa umakini mkubwa. Naishukuru kwa kuwa imeniamini na kunipa nafasi hii ya kuiwakilisha katika Wizara hii nyeti na kubwa. Nawashukuru pia kwa ushirikiano wanaonipa, bila kumsahau msaidizi wangu, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, kwa msaada wake katika hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii ambayo malengo yake makubwa ni kuhakikisha inajenga jamii yenye maendeleo na maadili mema ni lazima kuwa na uwezo thabiti wa kutambua matatizo yanayoikabili na kuyawekea mikakati ya kuyatatua kwa kutumia rasilimali zilizopo, kwa lengo la kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Ili kufikia azma hii, suala la kuwa na sera yakinifu, mipango inayotekelezeka na bajeti inayojali haliepukiki. Kambi ya Upinzani tunawasilisha tathmini na mapendekezo kwa lengo la kuhakikisha azma hii inatimia kwa manufaa ya Watanzania na mustakabali mwema wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea jamii kwa ujumla, tunaongelea mama, baba na watoto. Kutokana na jamii yetu ya Kiafrika, japokuwa tunaongelea usawa lakini ukweli ni kwamba, katika jamii yetu, baba bado ndio kichwa cha familia, yaani *male* ndiyo *bread winner* na kama hivyo ndivyo, basi tutambue kwamba, kama tutamsaidia baba basi tunaisaidia familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisinukuliwe vibaya ya kwamba, ninaunga mkono mfumo dume *(patriachy),* bali naomba itambulike ya kuwa, japokuwa tunapinga

lakini huu ni mfumo ambao bado unatawala kwenye jamii zetu hasa za Kiafrika. Hivyo, Serikali inatakiwa ijiulize ni kwa njia gani tunamsaidia baba huyu ili aweze kupata kipato kizuri na aweze kuiokoa familia yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama baba huyu tunakataa kumwongezea mshahara; je, tunasaidia vipi jamii zetu? Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani na kwa kupitia Wizara hii, naomba maelezo ya kutosha ya kuonesha ni kwa njia gani tunasaidia jamii zetu na kwa mikakati gani; na ni kwa jinsi gani mikakati hiyo inajitosheleza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipoweza kuangalia kwa undani zaidi kuhusu mishahara na kuwa wepesi kujibu, haitawezekana kwa sababu ya Pato la Taifa, basi kwa udhati kabisa tujue sisi ndio chanzo cha matabaka ya maisha ya Watanzania. Mfanyakazi yeyote aliyeajiriwa, kipato chake ni mshahara wake na si vinginevyo. Kama kweli Serikali inataka ipate tija kwa kazi anazofanya na kama tunataka kuendeleza msamiati wa maisha bora kwa kila Mtanzania inawezekana, basi tutimize wajibu wa kumwangalia Mtanzania huyu ili na yeye atimize kazi zake kwa muda aliopangiwa bila kigugumizi, sio tu kumhimiza awajibike kazini. Serikali pia inapaswa kuwajibika kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mishahara yote iliyopendekezwa haiwezekani, basi Serikali iangalie tena na isiwe chini, angalau shilingi elfu tano kwa siku kwa kima cha chini cha kula tu bila ya karo, bila ya watoto kwenda shule na bila ya kulipa kodi ya nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni busara Serikali ipange Mikakati Madhubuti ili iweze kumsaidia Mtanzania huyo ili aweze kuepukana na matatizo ambayo yanakwepeka kiurahisi sana, kwani suala la rushwa inayokithiri ndani ya jamii zetu ni kipato kidogo kisichotosheleza, ambacho hakimudu hata kutatua matatizo madogo madogo ya kifamilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii ya wazee ni muhimu sana, kwani sisi sote hapa tunaomba tufikie uzee. Tunapomwongelea mzee, tunamwongelea mzee wa Kitanzania. Wimbi kubwa la wagonjwa wa UKIMWI hivi sasa linakuwa mzigo kwa hawa wazee. Tangu kutunza wagonjwa wenyewe na hata kutunza yatima baada ya wagonjwa hao kufariki. Hili ni tatizo kubwa kwa wazee; ni jinsi gani huyu mzee ataweza kuwatunza watoto hawa na hana kipato cha aina yoyote kwa sababu hata jembe hawezi kulishika tena?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto yatima wanazagaa mijini, kufanyishwa kazi zenye hatari kwa maisha yao, ili aweze kumudu mkate wa kurudi nao nyumbani kwa ajili ya wazee hao na wadogo zao waliobaki pale. Kwa sababu Serikali haina uwezo wa kuwasaidia, basi pale wanapohitaji kulipwa mafao yao, walipwe kwa haraka na kama bado mzee huyu ana malipo ya uzeeni, yawe yanarekebishwa mara maisha yanapopanda *(inflation)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo imebaki wazee hawa kupigwa danadana, nenda rud, inasikitisha**.** Hayo yaliyozungumzwa hapa Bungeni kuwa wazee hawa

watakabidhiwa chombo maalum cha kushughulikia malipo yao, basi itekelezwe haraka na hayo yaliyozungumzwa asubuhi ya leo kwamba, watapewa miezi mitatu mitatu malipo yao, basi yatekelezwe yasibaki kwenye makabrasha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzee na kuzeeka ni dhana inayoelezea hatua ya mwisho ya makuzi ya binadamu kuanzia utoto, ujana na hadi kufikia uzee. Mtu anaitwa mzee kutokana na ama umri mkubwa au ukuu wa mahali pa kazi au ukoo. Wazee wetu walikuwa wakifanyakazi za kuajiriwa au kujiajiri hurudi vijijini ambako huenda kuishi baada ya kupungukiwa nguvu za kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali tuwaenzi na kuwaangalia kwa jicho la huruma wazee hawa, kwani ni jukumu letu na tuache mara moja kuwatesa kwa kuwapiga mpaka kufa kwa itikadi za kishirikina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanamke ni kiungo muhimu sana katika jamii yetu, kwani yeye ndio mlezi na mtunza familia. Yeye ndio anayeangalia kama mtoto ni mgojwa au kama hajaenda shule. Kwa ufupi tunaweza kusema, mwanamke ndiye mtunza maadili katika jamii zetu. Kumkomboa mwanamke ni kuikomboa jamii nzima. Mtazamo wa Serikali kuwa wanawake ni watu wa kufanya biashara ndogondogo, umepitwa na wakati. Maisha bora hayaji kwa biashara ndogondogo bali kwa biashara kubwa. Nia ya kila mfanyabiashara ni kuendelea zaidi na kuongeza faida *(success and expansion)*. Ni wakati muafaka Serikali kuanza kuweka mikakati ya kumwezesha mwanamke wa Kitanzania kufanya biashara kubwa. Ili kufanikisha hilo ni lazima Serikali ifanye yafuatayo:-

- Itoe mafunzo bora zaidi kwa idadi kubwa ya vikundi vya akina mama wajasiliamali na kutoa ushauri wa mara kwa mara wa biashara zao.

- Iongeze fedha za mikopo na irahisishe upatikanaji wa mikopo kwa kuhakikisha kuwa,benki zinazohusika na utoaji wa mikopo zinaondoa masharti yasiyoweza kufikiwa na wananchi maskini. Shilingi bilioni moja kwa kila mkoa hazitoshi, maana ili mfanyabiashara aweze kufanya biashara ya kueleweka, atahitaji angalau shilingi milioni moja. Kwa mahesabu haya, shilingi bilioni moja kwa mkoa, zitatosha wafanyabiashara elfu moja tu wakati katika mkoa mmoja kuna wajasiriamali zaidi ya elfu moja. Serikali inapaswa kuongeza fungu la mikopo.

Serikali inapaswa ilinde biashara za wajasiriamali kwa kuwatengea maeneo ya kudumu na yenye wateja wa kutosha, badala ya kuwahamisha mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande wa uwezeshaji kiuchumi kwa wanawake, katika mwaka wa 2006, Serikali ikishirikiana na asasi zisizo za Kiserikali, iliendesha mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake na waliofaidika ni wanawake 500 na wanawake 190 walishiriki katika Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa Dar es Salaam, ikiwa na utofauti wa asilimia 49.6 na ile ya mwaka 2005. Kiwango cha kutoa mafunzo kwa wanawake 500 tu ni kidogo mno kwa Serikali, ukilinganisha na idadi ya wanawake Tanzania nzima. Ni kweli Serikali inatakiwa kupongezwa kwa hilo. Lakini nikiwa na

nia thabiti ya kumkomboa mwanamke huyu, nalazimika kuuliza kati ya wanawake hao 500 waliofaidika; je, ni wangapi wanatoka katika jamii za vijijini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha dhana hii ya uwezeshaji wa wanawake kisiasa na kukuza ushirikishwaji wao katika siasa, Kambi ya Upinzani tunashauri yafuatayo:-

- Tunaliomba Bunge lako Tukufu lijadili athari ya mfumo usio na mpaka wa mtu kuwa Mbunge kupitia nafasi ya Kiti Maalum na kupitisha sheria itakayobadili mfumo huo.
- Tunatoa mwito kwa vyama vyote vya siasa nchini kuwa na Mpango Maalum wa Kuvutia Wanawake katika Siasa, kuwajengea uwezo wa ujuzi wa siasa, kuwaamini na kuwapitisha kugombea nyadhifa za ndani ya vyama na zile za kiserikali kama Serikali za Mitaa, Udiwani, Ubunge na hata Urais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja ni Nguvu, pamoja na wanawake kutofautiana kidini, kisiasa, kielimu, kiuchumi na kijamii, bado wote tunaunganishwa na mahitaji na maslahi yetu kama wanawake. Kwa mantiki hii, bado wanawake wa Kitanzania wanapaswa kuwa na muungano usiojali tofauti hizi. Kwa minajili hii, leo narejesha tena katika Bunge hili Tukufu, kilio cha miaka mingi cha wanawake wa Tanzania, nacho ni kilio cha kutaka kuanzishwa kwa Baraza la Wanawake Tanzania. Hoja na haja ya kuwa na Baraza la Wanawake Tanzania bado ingali nzito na hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna chombo cha kuwaunganisha wanawake wote wa Tanzania. Asasi za wanawake zilizopo, kila moja ina dira na dhima iliyo tofauti na nyingine, kwa hiyo, hizi haziwezi kuwaunganisha wanawake. Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), nao umepoteza uhalali wa kuwa chombo cha wanawake nchini, baada ya kuingia Mfumo wa Vyama Vingi.

Licha ya umoja huo kubeba jina "Tanzania" bado si chombo halali maana huu ni Umoja wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi, wakati pia kuna umoja wa wanawake wa vyama vingine kama wanawake wa *CUF* na Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwa na baraza hili haliepukiki, kujali wanawake si kuchagua wanawake kuwa Mawaziri tu lakini pia la msingi zaidi ni kuwawezesha kuwa na chombo cha kuwaunganisha kwa maslahi yao. Kama Serikali ya Awamu ya Nne inawajali sana wanawake, basi sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha Baraza hili la Wanawake. Mchakato wa kuanzishwa kwa baraza hilo, uanze katika bajeti hii na ushirikishe kikamilifu wanawake wa kada zote Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo kuna sheria nyingi zinazomhusu mwanamke bado hazijaletwa Bungeni, sijui tatizo ni nini hasa ukizingatia kwamba, Waziri wa Wanawake na Waziri wa Sheria ni sisi.

Mheshimiwa Spika, katika nafasi ya kipekee kabisa, napenda kuchukua nafasi hii, kuongelea mtoto wa kike. Sheria zetu katika kumlinda mtoto wa kike, bado zina mapungufu makubwa. Moja ya sheria hizi ni Sheria ya Ndoa ya 1971. Sheria hii inaruhusu mtoto wa miaka 15 kuolewa kwa ridhaa ya wazazi wake.

Mheshimiwa Spika, Rais wa Serikali ya Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameishauri jamii vizuri sana, pale alipotusihi tuwaache watoto wa kike wasome. Hii ni kauli nzuri sana, lakini hakuna sheria inayopinga kumwozesha mtoto huyu huyu kama mimi mzazi nimeridhia. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuwa, wakati sasa umefika wa kuangalia tena uwezekano wa kuboresha sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, bado tatizo la ukeketaji linaendelea katika baadhi ya maeneo nchi mwetu. Inasemekana kwamba, sasa wanaokeketwa ni wasichana wenye umri mdogo ambao hawana uwezo wa kujitetea. Ingawa vyombo vingi vinavyotetea haki za mwanamke, vinaendelea kupiga kelele kuhusu ukeketaji, tunaiomba Serikali kuongeza bidii ya kulishughulikia tatizo hili na hasa kuleta Muswada wa Sheria kali itakayosaidia kuondoa kabisa tatizo hili na Serikali kuisimamia kwa udhati.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa maendeleo ya watoto, Serikali iliwaondoa watoto 16,314 kutoka katika ajira mbaya ya watoto. Hili ni jambo la kutia moyo sana na hivyo ni lazima tuipongeze Serikali, kwani sote tunafahamu madhara ya ajira kwa watoto. Lakini pamoja na hilo, kwa kuwa nia yetu sote ni kufuta kabisa kitendo hiki haramu cha ajira ya watoto, basi kazi yetu ni kujaribu kutegua chanzo kikubwa kinachopelekea watoto kujiingiza kwenye ajira.

Mheshimiwa Spika, Wazungu walisema *if we want to solve the problems, then let us kill the real enemy*. Hivyo, kama nia yetu ni kutokomeza mfumo huu haramu wa kutumikisha watoto, basi tujaribu kutatua chanzo. Kambi ya Upinzani inatambua fika ya kuwa, kuna sababu nyingi zinazopelekea watoto kujiingiza katika ajira, lakini sababu kuu zaidi ni mbili nazo ni umaskini, pamoja na ongezeko kubwa la watoto yatima watokanao na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kuwatoa watoto hao kwenye ajira mbaya na kuwarudisha nyumbani kwao, ambako ndiko walikotoka, hakileti maana, kwani mtoto huyo ni sawa na kumrudisha kule kule alikokimbia ili kujikomboa. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuwa, sasa wakati umefika wa kutafuta mbinu mbadala ya kuwasaidia watoto hawa, kwa kuwawekea makazi maalum ili waweze kupata mahali pa kuishi na elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Spika, suala lingine linalokera na kusababisha usumbufu mkubwa kwenye kadhia hii ni kwamba, katika Wizara zetu, mambo ya watoto yamewekwa katika Wizara kuu mbili; nazo ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Jambo hili linasabisha usumbufu kwa sababu hatuwezi kujua hasa ni nani ambaye anaweza kuulizwa kuhusu uwajibikaji, kwani mambo yanakuwa yanaingiliana na hivyo kusababisha matokeo yasiyo na tija.

Mheshimiwa Spika, Wizara zenye mwingiliano wa kimajukumu zinakuwa na matatizo mengi na hili kosa hatuwezi kulielekeza Wizarani bali kwa mpangaji wa Wizara hizi. Hivyo, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, kwa kuwa nia ni kusaidia ni vyema jukumu hili la watoto likakabidhiwa kwenye Wizara moja na hivyo kusaidia kupunguza mwingiliano huu na mwishowe kuweza kupata nafasi ya kumuwajibisha muhusika na siyo kurushiana mpira kama inavyotokea sasa.

Mheshimiwa Spika, kinachohitajika hasa ni Wizara ipi ikabidhiwe jukumu la kumwangalia mtoto.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuthamini mchango wa Sekta ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali nchini. Suala hili pia limeainishwa kwenye Sera ya Taifa ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001, ambayo ndiyo mwongozo mkuu wa utendaji na uratibu wa *NGOs*, ambayo iko chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, imekuwa ikijitahidi kutekeleza majukumu yake. Aidha, inaratibu na kufuatilia utendaji kazi wa vyombo viwili vya Kitaifa, yaani Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs* na Baraza la Taifa la *NGOs*. Pamoja na jitihada za kutelekeza majukumu hayo, bado idara inakabiliwa na matatizo yafuatayo:-

- Upungufu wa bajeti ya kutosha (fedha), kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za *NGOs* mikoani *(monitoring and evaluation)* ili kuoanisha na taarifa zao za mwaka. Upatikananji wa taarifa hizi utasaidia sana katika kupata mchango wa sekta ya *NGOs* nchini na kuingizwa kwenye Pato la Taifa.

Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs* inatakiwa kufanya kaguzi kuhusu uendeshaji wa shughuli za *NGOs* mikoani na wilayani na hivyo kuishauri Serikali, uendeshaji wa Sekta ya *NGOs* nchini. Suala hili halifanyiki kutokana na ukosefu wa fedha. Chombo hiki sharti kiwezeshwe ili kitekeleze majukumu yake ipasavyo na hivyo kutumia fursa hiyo kurekebisha kero ambazo zinawakabili baadhi ya wadau wa Sekta ya *NGOs* nchini.

- Baraza la Taifa la *NGOs* halijatekeleza majukumu yake ipasavyo kutokana na ukosefu wa fedha. Kwa mfano, Kanuni za Maadili ya *NGOs* bado hazijamalizika, suala ambalo lingesaidia kuondoa kasoro zinazojitokeza sasa katika uendelevu wa Sekta ya *NGOs* nchini. Kanuni za maadili ni muhimu kwa Sekta ya *NGOs* nchini, kujisimamia kikamilifu kwa kuwa wadau wa sekta hii wanafahamiana vizuri nani mchapa kazi au mbabaishaji. Aidha, utekelezaji wa Kanuni hizi, utasaidia kuondoa dhana ya mtazamo hasi kwa Sekta ya *NGOs* nchini na kusaidia katika kukuza utendaji kazi wake.

- Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs* na Idara ya Uratibu wa *NGOs,* wanatakiwa kuwa na usafiri wa kuaminika, ambao utatoa fursa ya kutembelea, kufuatilia na kufanya kaguzi ya shughuli za *NGOs* mikoani na Wilayani. Ili kufanya kazi hii kikamilifu, wanatakiwa kuwa na fedha ya kutosha na angalau magari mawili, yenye uwezo wa kusafiria mikoani. Matatizo mengine yanajitokeza mikoani yanaweza kutatuliwa huko huko wadau waliko, badala ya kungojea hadi yanakuwa makubwa na madhara yake kuongezeka zaidi. Mfano, mnamo tarehe 15 Desemba, 2006, Bodi hii ilikutana na *NGOs* za Mkoa wa Morogoro, Chini ya Mtandao wa *NGOs* za Mkoa wa Morogoro - *UNGO* na kutoa maelekezo mbalimbali kuhusu Sheria ya *NGOs*. Kutokana na ufafanuzi huo,

wadau wa Mkoa wa Morogoro, wameelewa vizuri kuhusu suala hili na hivyo kasi ya usaijili wa *NGOs* kuongezeka maradufu. Safari za kikazi na jinsi hii zinatakiwa ziongezeke na hasa katika mikoa ambayo iko mbali na Dar es Salaam kama vile Kigoma, Rukwa, Tabora, Kagera, Mwanza, Mara, Shinyanga, Singida, Manyara, Mtwara, Lindi, Ruvuma na mingine mingi.

- Wananchi wengi bado hawajapata weledi ya kutosha kuhusu taratibu za usajili wa *NGOs* chini ya Sheria ya *NGOs* Na.24 ya mwaka 2002. Kuna haja ya kufanya jitihada za makusudi ili kuhakikisha kwamba, wadau wanao ufahamu na uelewa wa kutosha kuhusu Sera ya Taifa ya *NGOs,* Sheria ya *NGOs* na taratibu za usajili wa *NGOs.*

Baadhi ya Wasajili Wasaidizi wa *NGOs* katika ngazi ya Mkoa na Wilaya hawaelewi vizuri Sheria ya *NGOs* Na.24 ya mwaka 2002 na taratibu za usajili. Hii imesababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi ambao wanapenda kusajili mashirika ambayo wameyaanzisha kwenye maeneo yao chini ya sheria hii. Utaratibu wa kuwapatia mafunzo ya kina, ufanyike haraka ili kuondoa usumbufu kwa wananchi.

Msajili wa *NGOs* tangu aanze usajili mwaka 2005, amejitahidi kuwa na Benki ya Takwimu ya *NGOs* zote ambazo zimesajiliwa chini ya Sheria ya *NGOs* Na.24 ya mwaka 2002. Hata hivyo, si *NGOs* zote zimesajiliwa chini ya Sheria hii na hivyo kusababisha utata wa kuwa na benki moja ya takwimu za *NGOs* nchini. Serikali ifanye jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba, *NGOs* zote zinakuwa chini ya msajili mmoja ambaye atakuwa na uwezo wa kutoa taarifa ya mwaka kuhusu hali ya Sekta ya *NGOs* nchini na utendaji wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatambua ugumu wa uratibu wa *NGOs* ni kutokana na sheria mbalimbali Serikali iliangalie upya suala hili ili kuwepo chombo kimoja cha kuratibu hizo *NGOs*.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, katika jamii inayokuwa kwa kasi kubwa kama jamii yetu inatakiwa iwekeze thabiti kabisa katika vyuo vya elimu ya maendeleo. Kiwango cha ukuaji wa idadi ya watu nchini ni asilimia 2.9 *(population growth rate).* Kiwango cha wahitimu kinatakiwa kilandane na idadi ya ongezeko la watu kama kweli tunayo nia ya kujiletea maendeleo yetu wenyewe.

Mheshimwa Spika, vyuo vya maendeleo ya jamii ni muhimu sana katika jamii yetu. Tunaishukuru Serikali kwa kuondoa tatizo la maji ambalo lilikuwa linaathiri Chuo cha Tengeru kwa muda mrefu. Mbali ya kuondoa tatizo hilo, bado kuna uchakavu wa vyumba wanavyoishi wanafunzi, jambo ambalo ni hatari kwa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, upanuzi wa majengo katika chuo hicho ni uthibitisho kuwa Serikali inajali. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ipeleke bajeti inayohitajika mapema, kuendeleza ujenzi hapo chuoni isije kuwa kama yale majengo ya TVT kule mikocheni.

Mheshimiwa Spika, wakufunzi wa Chuo cha Tengeru wanahitaji pongezi kutokana na uwajibikaji chuoni hapo na pia tafiti wanazozifanya kuhusu jamii kwa

ujumla. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzifanyia kazi tafiti hizo muhimu na sio kuzipokea na kuziweka kabatini.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla vyuo vyetu vya maendeleo ya jamii, vinahitaji Serikali kuviangalia kwa makini, kwa sababu vingi bado havina walimu, wafanyakazi na miundombinu inayomwezesha mwanafunzi kupata kile kilichokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutenga bajeti ya kutosha ya kuviendeleza vyuo hivi, kama kweli inadhamira ya kuleta maendeleo katika nchi hii. Kwa mfano, Wizara ya Elimu ina mpango wa kujenga vyuo vya ufundi kila wilaya. Tunachoiomba Serikali, badala ya kutumia mabilioni kujenga majengo mapya, wakarabati Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, vilivyopo mawilayani ili vitumike kwa ufundi na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni hodari sana katika kuridhia Mikataba ya Kimataifa. Mikataba hii ni mizuri na kama ingeliletwa hapa Bungeni na Bunge kuridhia na kutekelezwa katika jamii yetu, ingelikuwa jambo la kheri sana na wananchi wangefarijika sana. Mikataba hii imekuwa kama donda ndugu katika nchi hii, kwani iliyo mingi inakuja na kuhifadhiwa badala ya kuletwa Bungeni ili kuridhiwa na kuanza kutumika. Nimelazimika kuliongelea hili hapa, kwani mikataba hii kwa njia moja ama nyingine, inamgusa mwanajamii.

Mheshimiwa Spika, inatia hasara pale unapoona mikataba ambayo Tanzania imesaini mwaka 1964 mpaka leo haijaletwa Bungeni. Je, Bunge liko *busy* muda wote huo wa miaka 43, limeshindwa kujadili mikataba hii na kuweza kuwaokoa wasichana hawa wanaoolewa kabla ya rika la utu uzima?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo kwa nini mpaka leo hakuna lililofanyika katika miaka yote hiyo. Lakini pamoja na hilo, kwa vile nia ni kujenga na sio kubomoa, Kambi ya Upinzani imewasaidia kuorodhesha baadhi ya Mikataba hiyo muhimu na inayowagusa wanawake na watoto ili ipate wepesi kuileta hapa Bungeni. Hii yote ni katika hali ya kusaidiana na kutambua kuwa kila mmoja ana kasoro zake.

Mheshimiwa Spika, hakuna maendeleo ya jamii yoyote kama hakuna demokrasia ya kweli. Demokrasia ya kweli ni ile inayojali wananchi wake. Hii ni pamoja na kuwa na uhuru wa kuchagua viongozi au kuchaguliwa katika jamii husika. Nchi yetu ni ya kidemokrasia na inayofuata Mfumo wa Vyama Vingi. Mfumo huu hata hivyo hautoi uhuru wa kutosha wa mtu kuchagua au kuchaguliwa kuwa kiongozi wa jamii husika.

Nasema hivi nikizingatia ukweli kuwa, demokrasia yetu inalazimisha watu kugombea uongozi kupitia vyama tu ilihali wapo watu wenye uwezo wa kuongoza na wanaopendwa katika jamii lakini wasiokuwa na mapenzi na itikadi wala chama chochote. Hawa wanakosa haki yao ya kidemokrasi ya kugombea.

Mheshimiwa Spika, katika hali kama hii, hoja ya kuwa na mfumo wa kidemokrasia unaoruhusu wagombea binafsi haiepukiki. Mahakama kuu hivi karibuni ilitoa hukumu inayoruhusu haki ya wagombea binafsi (rejea kesi ya mchungaji Mtikila *Vs* Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania). Suala la mgombea binafsi ni suala amabalo halihitaji mjadala ni wakati sasa Serikali ikatimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, yote niliyoyawasilisha ni kwa maslahi ya Watanzania na yote yanawazekana. Ushauri huu wa kiufundi si tu ni ujumbe kwamba, Wapinzani tunaweza, lakini pia ni funzo kwa serikali kuwa nchi haiongozwi kwa maneno matamu, bali kwa sera yakinifu, makini na zinazotekelezeka.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwasiliza wasemaji wote wawili, sasa nadhani ili tuendane na muda, twende moja kwa moja kwenye mchango wa jumla. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Devota M. Likokola aanze kuchangia mada hii, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar naye ajiandae.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa hotuba yao nzuri, lakini pia kwa ufanyaji wao kazi mzuri, ambao unaendana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitachangia kwa kifupi sana katika maeneo matano yafuatayo: Kwanza, nitachangia kuhusiana na suala zima la *fifty fifty*. Pili, nitachangia juu ya uwezeshaji wa Wanawake. Tatu, nitachangia juu ya maendeleo ya jinsia. Nne, nitachangia juu ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali, yaani *NGOs*. Tano, nitachangia juu ya Wanawake wa Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza na suala la *fifty fifty*. Ninakipongeza sana Chama cha Mapinduzi, katika Ibara ya 20 ukurasa wa 149, Chama cha Mapinduzi kimeainisha wazi umuhimu wa Mwanamke wa Tanzania na kimeweka nia thabiti ya kuweza kuinua hali ya jinsia katika nchi yetu na kwamba, ifikapo mwaka 2010, asilimia ya wanawake katika nafasi za kisiasa, kiutendaji na nafasi za maamuzi, inatakiwa iwe nusu kwa nusu, yaani Wanawake na Wanaume.

Jukumu hili ni kubwa na ninaiomba Wizara, iangalie jukumu hili na kuweka mikakati thabiti na katika hili ninapoiomba Serikali, maana yake ninazungumza na wadau wote wa Serikali. Tuanze na Mheshimiwa Rais, ambaye ameonesha kwa vitendo mfano wa kuwathamini wanawake na kuwaingiza katika nafasi mbalimbali za maamuzi. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aige mfano huo, Mawaziri mbalimbali, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmshauri na Watendaji wote. Ninaiomba Serikali katika hili, ianze kutengeneza kaulimbiu ili kila mmoja ajue kwamba, ifikapo mwaka 2010 ni nusu Wanawake na nusu Wanaume katika nafasi zote.

Ninaimba Serikali ishirikiane na wadau wote na hapa kwa kweli ninawaomba sana wadau wote wakiwemo Wanaume, Wanawake, Mashirika ya Dini, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na kadhalika. Ninaomba vyombo au taasisi zote ambazo zinahusika na maendeleo ya Wanawake. Kwa umuhimu mkubwa sana, ninawaomba waandishi wa habari na vyombo vya habari, vitusaidie katika kulieneza suala hili ili kila mwananchi alipo, ajue kwamba itakapofika mwaka 2010, tunatakiwa tuwe nusu, kwa hiyo, tutengeneze mikakati na namna ya kufikia nusu kwa nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie suala zima la uwezeshwaji wa wanawake. Wanawake wa Tanzania katika suala zima la uwezeshwaji, tunahitaji mambo makubwa mawili tu. Kwanza, tunahitaji elimu na mafunzo mbalimbali ya ujasiriamali na kujiajiri wenyewe. Lakini la pili, tunahitaji mitaji na katika hili na katika taarifa mbalimbali inaonekana kwamba, wanawake ambao wamepatiwa elimu, ukiangalia ile taarifa ya uchumi ya mwaka jana, inaonesha kwamba, wanawake ambao wamepatiwa elimu na mfunzo ni 500 tu. Nchi hii ina Wanawake wengi, ninaomba idadi iongezeke, kwani kama tutakuwa tunakwenda kwa mtindo huu, basi wanawake wengi hawatapata elimu na matokeo yake, hawataweza kujiajiri, wala kufanya shughuli zozote za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika masuala mazima ya wanawake kupata mitaji, bado Sekta ya Fedha imewatenga. Wanawake wengi mijini na hata vijijini, bado hawaifikii Sekta ya Fedha na hawazipati hizo pesa. Masuala ya fedha hizi za Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alizozitoa, hatujaambiwa ni asilimia ngapi ya wanawake wamenufaika nazo na hili inaonekana kwamba, bado wanawake hatujanufaika na hiyo mitaji ambayo Serikali inatoa. Ninaomba Sekta ya Fedha, iongeze fursa kwa Wanawake wa Tanzania, kwa sababu pamoja na mambo yote Wanawake tutakayofanya, bila kuwa na mitaji, hatutaweza kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie suala zima la maendeleo ya Jinsia. Jinsia katika nchi yetu ni suala nyeti, ni suala muhimu, hakuna maendeleo bila usawa wa jinsia na bado tunashuhudia katika nchi yetu, mfumo dume unaendelea kutawala. Kwa hili, mimi ninaiomba Serikali, kweli kabisa ni lazima tuangalie kama wanaume watazidi kuwakandamiza wanawake itakuwa ni shida kubwa na maendeleo hayatapatikana. Maendeleo ambayo yanapatikana, ambayo yana umiliki mkubwa wa wanamume, hayana maana yoyote, kwa sababu watu wanataka kuona wanawake na wanaume wanaendelea na kwamba, jamii ni lazima itambue hususan wanaume watambue nafasi ya mwanamke katika kuleta maendeleo ya Tanzania. Wanawake tuna nafasi kubwa sana, bila ushiriki wa wanawake, maendeleo ya Tanzania hayatakuwepo.

Kwa hiyo, watoe hiyo nafasi ili wanawake washiriki kikamilifu na ninawaomba wananchi watambue nafasi za makundi maalum kama vile wanawake, vijana, wazee, watoto na kadhalika. Kila mtu katika jamii hii ana nafasi yake na kama tutaendeleza mfumo dume wa nafasi tu ya watu wachache, basi maendeleo yatakuwa ni magumu sana. Ninaomba sana katika hili na nimeona katika bajeti, ninaomba Serikali iongeze pesa katika *desk* la jinsia.

Katika Wizara nyingi bado hakuna usawa wa kijinsia katika nafasi nyingi za kiutendaji. Nafasi ya jinsia ni ndogo sana, kwa hiyo, ninaomba zile pesa ambazo zimetengwa pale karibu shilingi milioni 137, kwa ajili ya kuendeleza jinsia kwa nchi yetu na hapa tunahitaji mafunzo mengi kuoanisha watu wengi waweze kutambua masuala ya jinsia, kutoa mafunzo hasa hasa kwa wanaume, maana suala la jinsia linahitaji utashi wa ukweli ili watu wote tushiriki katika hilo. Hizo pesa ni dogo na nimeona kwamba, hizo pesa ni za upande wa wafadhili tu. Je, Serikali yenyewe kama iko *serious* na suala la jinsia, imetenga kiasi gani kwa pesa zetu za ndani? Ninaomba Serikali ioneshe *commitment* ya hii, itenge pesa zetu za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali. Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali katika nafasi hii, ninasimama na kuyapongeza sana kwa jitihada wanazofanya katika kuendelea kushirikiana na Serikali kuwaletea wananchi wa Tanzania maendeleo. Baadhi ya mashirika mengi yanafanya vizuri lakini bado kuna mashirika mengine yanasuasua. Ninaomba Kitengo cha Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, kiwezeshwe ili kisaidie haya mashirika yanayosuasua na kiweze kusaidia kuwaelekeza wananchi na hususan wanawake, mifumo mbalimbali ya namna gani ya kusajiri *NGO* au *CBO* zao ili waweze kujiendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo hiki cha *NGO* ni muhimu sana kwa maendeleo yetu na katika kuleta maendeleo ni lazima ushirikiano wa mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, Serikali na wadau wengine. Ninaomba kama kuna pesa zimetengwa basi ziongezeke ili ifanyike kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na taadhima, ninaomba niwazungumzie Wanawake wa Mkoa wa Ruvuma. Wanawake wa Mkoa wa Ruvuma nimesimama hapa kuwapongeza kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kujiletea maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe utakuwa ni shahidi, Wanaweke wa Ruvuma wako mbele kwa mbele kuendelea katika michakato ya kujiletea maendeleo na ninawashukuru kwa ajili ya ushirikiano mkubwa wanaotupa sisi Wabunge Wanawake wa Mkoa ule, ambapo wameendelea kujiunga na *SACCOS* ambazo Mheshimiwa Jenista J. Mhagama alizianzisha, wameendelea kujiunga na Vikoba ambavyo Mheshimiwa Devota M. Likokola alivianzisha na wameendelea kujiunga na *Better Life*, ambayo Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya ameianzisha, Vikundi vy *DMI* – Masista wa Kihindi, *SIDO* – Songea, ikiongozwa na Mama Lucy Sarungi. Lakini hao wote wametoa ushirikiano mkubwa kwa uongozi mzuri na mahiri wa mwanamke mwenzetu, Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Monica N. Mbega. Ninawapongeza sana Wanawake wa Mkoa wa Ruvuma kwa ushirikiano huo, nina imani tutaendelea na Mungu atujalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Asante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nimpongeze Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Ruvuma, kwa mchango

wake mahiri kabisa. Amezungumza suala la usawa wa jinsia na ninaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge katika orodha ya leo walioomba kuchangia mada hii Wabunge Wanaume ni watatu tu. Sasa nadhani kuna nafasi ya Waheshimiwa Wabunge Wanaume kuongeza majina yao katika kuchangia mada hii ya leo ili kuleta usawa wa kijinsia kwa kuanza na hapa Bungeni.

Kwa hiyo, nakupongeza sana Mheshimiwa Devota M. Likokola, naomba nimwite sasa Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar na Mheshimiwa Ali Juma Haji, ajiandae.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika Hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, ambaye ametufikisha tukiwa hapa leo katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kwa niaba ya Wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba, kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza napenda ama naomba kutoa pole kwa familia ya aliyekuwa Mbunge mwenzetu, Marehemu Amina Chifupa. Napenda kutoa pole hizo kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki na vijana wote wa Tanzania, tuwe na subira katika kipindi hiki kigumu, kwa kuondokewa na mpenzi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara hii kwa hotuba yake hii ambayo inaleta mwangaza katika nchi yetu hususan kwa Wanawake nawapongeza sana Mheshimiwa Sophia M. Simba na Mheshimiwa Salome J. Mbatia, Viongozi wote wa Wizara na Wanawake wote wa Tanzania na wengi tukiwemo humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja hii mia kwa mia kabla sijasahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina sifa moja kubwa kwanza, hii ni Wizara Mama ambayo uongozi wake ni mzuri sana na ninafurahia sana kwa sababu inashirikiana bega kwa bega na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake, Vijana na Kazi kule Zanzibar. Napenda sana kuipongeza na ninawaomba waendelee na ushirikiano huo, kwa sababu Wanawake wa Tanzania, tusiposhirikiana tukibaguana, hawa Watanzania Bara na hawa Wazanzibari, basi tutakuwa hatuendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja. Naanza kuchangia katika uanzishwaji wa Benki ya Wanawake. Napenda kuipongeza Serikali yetu Tukufu kwa kuanzisha ama kuwa katika *process* ya uanzishwaji wa Benki hii ya Wanawake, kwa sababu Wanawake ndiyo asilimia kubwa ya nchi. Ila hapa napenda kuomba vilevile kama wanavyoshirikiana Kiwizara basi na haya mambo ya uanzishwaji wa Benki ya Wanawake, iwe wanashirikiana pia na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Wanawake wote Benki hii iwe ni yetu, isiwe ya huku na huko wakawa hawamo.

Naomba sana benki hii kwa ushirikiano mkubwa ikija ikianzishwa, ianzishwe Tanzania nzima, ndiyo Wanawake wenzetu ambao watashirikiana kwa pamoja kwa Tanzania nzima kufanya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuisifia kwa sababu Wanawake wengi katika nchi hii ndiyo wajasiriamali wakubwa, lakini ni vigumu kupata mikopo katika benki ambazo zipo. Benki hii itakuwa yetu sisi wenyewe, tutapata mikopo kwa hiyo, nawahamasisha wananchi wote wa Tanzania, tukiwemo sisi Waheshimiwa Wabunge, tuchangie kuweka hisa katika Benki hii na tumeshaanza. Kwa hiyo, nawahamasisha na wananchi wote, waiunge mkono Benki hii ya Wanawake hapo itakapoanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzangu ameshazungumza kuhusu mfumo dume. Mimi napinga sana mfumo dume, bado haujaondoka hapa Tanzania. Pamoja na kwamba, *fifty fifty* itakuwepo, lakini akina baba wengi wanadharau sana Wanawake, sisemi wote lakini wengi. Wanawake ni wapiganaji, ndiyo sisi ambao tunafanya kazi za kilimo mashambani, ndiyo sisi tunaowalea watoto na ndiyo sisi tunaowalea na wao wenyewe akina baba. Ukishalima na kijembe cha mkono au hata kama ni kwa trekta, ukishafikisha nyumbani baba ndiye anayepanga. Mpunga ukishapatikana au mahindi baba ndiye anayeseme yauzwe hivi au hivi. Inakuwaje kazi niifanye mimi, wewe ndiyo ujipatie mapato? Akina baba ondoeni mfumo dume, nawaomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuanzisha Mfuko wa Fedha kwa Wajasiriamali. Fedha ya Kikwete wengi wanaiita “Pesa ya Kikwete”. Tunampongeza Rais wetu, maana haijawahi kutokea katika miaka yote ya nyuma toka nizaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mikoa yetu ama sehemu zetu ambazo tunatoka, kuna *SACCOS,* kuna mashirika, vikundi vya ushirika mbalimbali, hii pesa imewasaidia sana Wananchi wa Tanzania hususan Wanawake. Kwa nini nimesema hivyo? Kuna vikundi mbalimbali vya *SACCOS*, ambavyo hata hapa Bungeni tunaambiwa kwamba, vinapata na ni kweli kwamba vinapata lakini Serikali ichukue hatua vilevile kuona kwamba hii pesa haiendi kidogo kidogo, isiende chini wengine waiibe, iwe na usimizi mkubwa. Napenda sana hizo fedha ambazo zitatolewa, tumeambiwa kwamba, zitafika kwenye Visiwa vya Zanzibar na ni kweli zipo katika *process* za mwisho katika matayarisha hayo. Lakini naomba Serikali ifanye haraka, unajua tena wenzako wakipata na wewe unategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku nikisimama hapa ninawatetea wanawake wajane na Mwenyezi Mungu, aninusuru nisije nikawa mjane. Lakini hao wajane na wao tunapaswa sisi ambao tuna wanaume, tuwatetee wajane wanadhalilishwa. Mwanamke akiolewa akiwa katika nyumba, anakuwa mzuri, anasifiwa na kila kitu, siku ambayo mume wake atakufa, basi familia ya yule mwanamume hususan makabila mengine, wanawatesa sana hao wajane. Tuwatetea wajane, wanaume wa Tanzania wateteeni ajane wasiteswe. Wajane ni watu wa kuhurumiwa sana na ni watu wa kufarijiwa sana kwa sababu wameondokewa na waume zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa ambacho kinaniuma sana, hukosa hata haki ya kuwapata watoto wao, kwa sababu wananyang'anywa mpaka watoto. Kwa hiyo, mimi naomba sana suala hili Wizara ilifuatilie, kuna wajane wengi sana hapa Tanzania ambao wana matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kimoja ambacho kinanikereketa sana, kule kurithiwa kwa wajane. Mambo ya kurithiwa hawayataki, inakuwa namna gani mwanamke anarithiwa! Halafu anarithiwa mtu hata UKIMWI hajaenda kupima. Ikiwa yeye amefiwa na mume wake wewe unasema mimi nitakuoa tu. Mimi napenda sana wanavyotoa kwenye televisheni hayo maelezo ya michezo mbalimbali ambayo inakuwa *against* na hayo mambo ya kurithiwa wajane, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto yatima wananyanyasika na sisi wazazi tunaona. Hata kama si mtoto wako uliyemzaa, yatima ni mtoto wako. Inakuwa namna gani mtoto yatima unamtesa, unamwona mama yake na baba yake wamekufa, unasema atajijua. Ndugu wa watoto yatima wasiwapeleke kwenye *NGOs* wakalelewa huko, ni vizuri kama watalelewa na wao lakini maadili ya kule nyumbani wanayakosa. Naomba *NGOs* ziendelee kuwalea watoto yatima, lakini na ndugu nao wajitahidi, wazazi wakiondoka watoto wale wawapende na wawalee, watoto yatima ni watoto wetu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto ombaomba wanatokana na hapo hapo kwa watoto yatima na pengine si yatima, pengine katelekezwa. Pengine mtoto kafukuzwa na mama yake, pengine hata mama wa kambo. Akina mama wa kambo wengine siyo wazuri, wanawatesa sana watoto. Kwa hiyo, vilevile tuone kwamba hao watoto ombaomba, Serikali iwasaidie sana tukiwemo sisi Waheshimiwa Wabunge. Tuwasaidie sana watoto ombaomba katika sehemu zetu wapungue ili kuwasaidia kuwaweka katika sehemu ambazo zinastahili. Vilevile ndugu zao wawasaidie hao watoto wasifukuzwe majumbani kwa kuwa wamefiwa na wazazi wao, wawalee ili wasiende kukaa barabarani, mvua ikawanyeshea na jua likawapiga. Mimi ninaongea kwa uchungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma mimi nilikuwa nakwenda Mnadani kununua vitu vya nyumbani. Siku moja nikiwa huko nakula nyama na wenzangu, wakaja watoto, ile mifupa inayoanguka chini wanaokota, inauma sana. Lazima tuwajali watoto hao na katika Taifa letu hili, tuwaondoe kabisa watoto ombaomba na wengine hao ni yatima. Hawataki wao kuwa ombaomba, lakini wanafanya vile hawana pa kwenda, wanapokwenda popote wanafukuzwa. Jamani watoto ombaomba na watoto yatima ni watoto wetu, tuwatunze. Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake anijibu, tunaelewana mimi sitokubali kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanawake wanaotupa watoto, mimi najiuliza hivi ni nani aliyewaambia wawazae? Kwa nini wao wasijizuie kufanya tendo la ndoa, kama wao hawataki kubeba mimba wakapata watoto? Kwa nini wanafanya tendo la ndoa na kama wanafanya tendo la ndoa na wao hawataki kubeba mimba; kwa nini hawatumii njia mbalimbali za kuzuia mimba? Inasikitisha sana na ni ukiukwaji wa haki za binadamu. Mtoto unamzaa unaenda kumtupa kwenye jalala, unamchukua mtoto mzima unamuweka kwenye mfuko wa plastiki, anavuta pumzi mpaka pumzi zinakwisha! Kwa kweli inasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema Serikali ichukue hatua na mimi nataka niambiwe ni watu wangapi ambao wamekamatwa ambao wamefanya kitu kibaya kama hicho? Ni adhabu gani wanayopewa wale wanaozaa watoto halafu wanawatupa kwenye jalala? Inasikitika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ubakaji. Baba mzima, mtoto wa mwenzio ni wako, mtoto wa jirani yako ni wako, hivi kweli unamwona mtoto wa miaka sita ni mzuri sana; unamwona mtoto wa miaka kumi ni mzuri sana, basi jibake mwenyewe. Hii tabia ya kubaka kwa kweli ni kuondoa utaratibu mzuri tulionao katika nchi yetu. Tabia hii inachangia UKIMWI, inachangia mimba za utotoni; kwa nini unambaka mtoto wa mwenzako wakati mtoto wa mwenzako ni wako?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine cha kushangaza, akina baba wengine wanabaka watoto wao, inakuwa namna gani? Serikali inaangalie hili. Ninaiomba sana Serikali ilete hapa Bungeni, sheria kali, sijui hata wafanywe nini? Katika *Radio One* jana wametoa Mkoa wa Kigoma, Mahakama ya kule wamempa adhabu ya kifungo cha miaka 30 na kuchapwa viboko 12 kwa kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka sita na kutia mimba. Naipongeza sana Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mateso ya watoto wanaofanya kazi majumbani. Jamani watoto wanaofanya kazi majumbani si watoto wetu wenyewe; kwa nini umwamini akupikie, akutandikie kitanda, akufanyie usafi ndani ya nyumba yako, halafu unamtesa. Tunazo tabia hizo wanawake, hususan wanawake wengine wakorofi. Unaenda kumchukua mtoto kijijini kwao, mshahara humlipi, unamtesa unamlaza kwenye sakafu, watoto wako wanalala kwenye vitanda, yaani unamtesa hata humpi chakula, unampa ukoko! Kweli huu ni ubinadamu? Wanawake na akinababa, naomba sana tuwatunze watoto ambao tunawachukua watusaidie kufanya kazi nyumbani, kumfanyisha kazi umfanyisha, halafu unamtesa. Serikali imefanya utafiti gani kuona hao watoto wa nyumbani wanateswa kwa kiwango gani? Sisi watu wengine kwa kweli tunawanyenyekea watoto kama hao, unachowafanyia watoto wako basi na yule mfanyakazi unamfanyia. Lakini kwa nini iwe hivyo? Kwa wale wenye tabia hizo waache mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukeketaji, ajenda hii kila mwaka naizungumzia. Ukeketaji na Mheshimiwa Anna Komu kasema ni kinyume cha haki za binadamu. Hivi wao hawajui kwamba, watoto wao wakiwakeketa wanaweza kufa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nafikiri mnakubaliana na mimi kwamba, hawa Waheshimiwa Wabunge wanawake ni moto kabisa. Mwaka jana Waheshimiwa Wabunge Wanawake, historia yangu inanikumbusha nilikuwa hapa Mezani waliongozana hivi hivi. Bahati mbaya sana Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, hajapata nafasi nzuri sana ya kutosha kuzungumzia ukeketaji, kama alivyozungumza

mwaka jana. Naomba nimwite Mheshimiwa Ali Juma Haji na Mheshimiwa Martha J. Umbulla, ajiande.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ingawa tuliambiwa wachangiaji wanaume watakuwa watatu tu. Lakini na sisi tunataka kuonesha kwamba si wanawake tu ambao yanawakereketa mambo haya ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Lakini na sisi tutaonesha moto wetu kwamba na sisi wanaume yanatukereketa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile na mimi ni mara yangu ya kwanza kuchangia kwa kusema, basi sina budi kuungana na wenzangu, kutoa salamu zangu za rambirambi kwa wale ndugu za marehemu waliopata ajali mbalimbali za magari na kwa ndugu wa Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa na kuwaombea marehemu wote, Mungu awalaze mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mada zangu zitakuwa tatu ambazo haidhuru zimekwisha ongolewa, lakini kwa sababu na mimi zinanikereketa, inabidi niziongelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naenda kwenye ubakaji. Suala la ubakaji kwa kweli linaumiza sana na hasa kama walivyosema wenzangu, akina baba watu wazima, midume mizima, ina miaka 50 inakwenda kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka mitano au sita. Kwa kweli hii inakereketa na nadhani wimbi hili linaongezeka kila siku, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake, sijui tuseme kwa nini ama sheria zetu bado labda siyo kali sana? Kwa sababu mimi naona adhabu ya kifungo cha miaka 30 kumfunga mtu ambaye alimbaka mtoto mwenye umri wa miaka sita, haikidhi haja ni ndogo mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo mtu aliyembaka mtoto mwenye umri wa miaka sita kwa kweli ni sawasawa na muuaji. Wengine wanambaka mtoto mpaka anakufa, halafu huyo anaambiwa ni mbakaji, anafungwa miaka 30 jela. Kwa kweli huyo mimi ningesema haifai kufungwa miaka 30. Labda Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar hakusema, lakini mimi ningesema basi wale wanaobaka watoto wenye umri wa miaka mitano au sita, hao wafungwe kifungo cha maisha na wahasiwe wasiachwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa makusudi, mwanamume ambaye ana umri wa miaka tuseme 30, anambaka mtoto wa kike, anaenda kufungwa kifungo cha miaka 30, akitoka huko yeye anakuwa na umri wa miaka 60 au 70, anaoa, wakati yule mtoto wa kike ameshamharibu, madaktari wameshathibitisha kwamba, hatazaa tena, ameshamvurugia maisha yake kwa kila namna. Kwa hiyo, kufungwa kwa miaka 30 haitoshi na yeye ahasiwe asizae kama yule mtoto alivyomfanya asizae tena. Hapa tumeona mfano mzuri ulio hai, wakati Waziri wa Kivuli wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, alipotoa hotuba yake, alisema kwamba, zimebaki siku tatu tu kutimiza miaka 60.

Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, nadhani kesho atatimiza miaka 60. Mtu kama huyo akitoka jela anaweza kuoa mtoto mdogo mwali na akazaa. Lakini leo mtu kama yule akifungwa miaka 30 haitoshi. Naomba hiyo sheria ifanyiwe marekebisho, adhabu ya kifungo cha miaka 30 iwekwe kwingine ambapo nitakusema, lakini hao wafungwe maisha ama wahasiwe ili wasiweze kuzaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninalopenda kuzungumzia ni kuhusu unyanyaswaji wa akina mama, ambao wamefiwa na waume zao na wale watoto ambao wamefiwa na baba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nawapongeza wale waigizaji wa mchezo ambao ulimalizika juzi katika *ITV,* unaitwa Hatia. Mchezo ule mimi nilikuwa naufuatilia sana kwa sababu ya kipengele hiki tu cha unyanyasaji wa yule mama alivyokuwa ananyanyaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama yule baada ya kufa mumewe, shemeji yake kwanza alitaka kumrithi kwa kumwoa, halafu mali zote akazichukua yeye. Mchezo ule unaonesha yule baba akiamka tu panga mkononi, anamtishia yule mama na anawatishia wale watoto maisha yao, wasiguse mali zozote alizoacha baba yao au alizoacha yule mume wake, mali zote ziwe chini yake yeye. Kwa kweli mchezo ule ulituhuzunisha sana na kama hali ndiyo ile katika familia nyingine, ipo haja ya kutunga sheria kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachosema, mchezo ule uliishia kwamba, yule mama alipata watu wakamshauri aende Mahakamani, hatimaye Mahakama ikatoa hukumu kwamba, arejeshewe zile mali zilizobakia, kwa sababu yule shemeji yake mali nyingine alishaziuza, lakini mali zilizobaki ziongozwe na yule mama. Hiyo haitoshi, alishawadhalilisha wale watoto wamekosa kusoma, wakati baba yao kawaachia mali za kuweza kuendeleza wasome vizuri, lakini zile mali amezichukua yeye, watoto wamekosa kusoma, haitoshi kuambiwa kwamba zile mali zirudi kwa watoto.

Baada ya kuhukumiwa zile mali azirudishe na huyo afungwe tena miaka 30 ile irudi huku. Afungwe kwa sababu amewadhalilisha wale watoto wamekosa huduma nzuri na mbaya zaidi aliwatia fitina wale watoto wasielewane hata na mama yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo hayo yapo katika jamii zetu, hatukatai yapo na kwa kweli yanaumiza na hayo ndiyo tunaonesha kwa akina mama kwamba siyo wao tu ambao wanaumia na sisi pia yanatuumiza. Kwa sababu mtoto yeyote mdogo akiumizwa, kama mzazi, unahisi kweli basi ikiwa mtoto wa mwenzako anafanyiwa vitendo kama vile na wewe itakuumiza tu. Kwa hiyo, tunaomba kwamba na sisi watuelewe akina mama yanatuuma sana sio wao tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, kuhusu ukeketaji. Mimi nilikuwa hasa sijui ukeketaji ni nini na mpaka sasa hivi sijui ukeketaji ni nini, isipokuwa nimeona katika maonesho tuliyotembelea hapo nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi machozi yalinitoka siku niliyotembelea katika banda lile la ukeketaji, nilioneshwa jinsi yule mwanamke

anavyokuwa baada ya kukeketwa, macho yangu sikuamini kama kweli ndivyo hivyo. Kwa kweli ipo haja ya kupiga vita vikali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine tumeambiwa kwamba, wanashonwa tu kwa sababu ya wivu wa baba, anashonwa kule sehemu yake ya siri, tulioneshwa yote hayo, siyo siri kwenye yale mabanda ya maonesho. Anamshona yapo makabila tuliambiwa mpaka arudi safarini ndiyo amtoe zile nyuzi, mara ngapi atamshona mwanamke yule? Huo ni udhalilishaji mkubwa. Kila akiondoka baba amshone, akirudi amtoe zile nyuzi, itakuwa mara ngapi? Kwa kweli hilo ni suala gumu na zito na linahitaji kutungiwa sheria mahsusi kama ya ubakaji. Hiyo inasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hiyo ya kushonwa, tulioneshwa nyingine, wale waliokuwa na *demonstration* wakikwambia huyu ndivyo alivyokeketwa hivyo, hutazami mara mbili. Kama una hisia za binadamu huangalii, hivyo ndivyo anavyokuwa mwanamke kweli, inasikitisha. Kwa kweli inasikitisha sana na kuna haja Serikali itunge sheria kali sana kwa wale wanaokeketa. Mbali na hayo, vile vifaa wanavyovitumia, unauliza wanavitumia namna gani? Kuna kisu kidogo, unaambiwa kinapitishwa mpaka inatolewa ile sehemu anayoitaka, huwezi kuangalia. Kuna haja ya kubadilisha sheria na wao watungiwe sheria kali. Kwa sababu wanaume hawakeketwi, wao wanafanyiwa tohara, lakini wanawake wanaokeketwa wanaumizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui hili ni suala mtambuka, lakini nizungumzie hao watu ambao wanajaribu kuanzisha vituo kwa ajili ya kuhudumia watoto yatima au watoto wa mitaani. Kwa kweli sijui kama hili linahusiana, nafikiri litakuwa ni mtambuka pengine Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara hii zinahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kweli kuna watu tunawaona kwenye vyombo vya habari mbalimbali kwamba, wameanzisha vituo kwa ajili ya manufaa yao wenyewe. Wanawatesa wale watoto wanapokuwa kule vituoni, wawanatesa vibaya sana, lakini watoto wale ndiyo wanaowanufaisha kwa kuwapeleka nje kusoma, hawawapatii huduma nzuri, lakini wale ambao wamewaandikisha kwa ajili ya vituo hivyo, hawawapatii haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ningeomba Wizara hii, ifanye utafiti wa kina juu ya vituo vile na kuhakikisha kwamba ni kweli wale watoto wanapatiwa huduma, kama walivyokwenda kuomba au wanafanya ubadhirifu kwa ajili kutafuta manufaa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, Mheshimiwa Mawaziri, katika hotuba yake ameonesha majedwali mengi ya mambo mbalimbali, lakini hatujaona hapo kuna watoto wangapi waliobakwa katika majedwali hayo na taarifa zao kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2007. Hatukuziona hizo taarifa au hakuna, wakati kwenye vyombo vya habari kila siku tunasoma Mkoa fulani watoto kadhaa wamebakwa? Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, wakati anahitimisha hoja yake, atuambie kuanzia mwaka 2000, kama hizo takwimu nyingine zilivyo mpaka 2007, idadi ya watoto waliobakwa kuanzia kwenye Wilaya na Mikoa, wanawake na wanaume kwa sababu

wanabakwa wanawake na wanaume. Mfano ulio hai, juzi nimesoma gazeti moja, baba mmoja alimwacha mke wake akamchukua mtoto wake wa kiume akambaka vibaya sana. Kwa hiyo, mambo hayo yapo kwa watoto wa kike na watoto wa kiume. Kwa hiyo, tunaomba hizo takwimu zioneshwe kama hayo mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Asante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ali Juma Haji, nakushukuru sana. Ni kweli haukutaka kuchangia katika hotuba yoyote, ulikuwa na mambo muhimu sana katika hotuba ya leo. Tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Ali Juma Haji, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Martha J. Umbulla, atafuatiwa na Mheshimiwa Haroub Said Masoud na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, kama muda utatosha ajiandae.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika *session* ya Bunge hili la Bajeti, naomba nitumie fursa hii, kutoa salamu za rambirambi kwa ajili ya kifo cha binti yetu, Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa, ambaye alitutoka. Marehemu Amina Chifupa alitembelea Mkoa wa Manyara muda mfupi tu kabla ya kuugua kwake. Kwa hiyo, wananchi wengi hususan wanawake, walinipigia simu kwamba, waliguswa sana na kifo chake na kwa kweli waliomba sana nifikishe rambirambi zao kwa Bunge hili Tukufu, kwa jamaa, marafiki na ndugu wa marehemu. Namwomba Mwenyezi Mungu, ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza kuchangia hoja hii, naomba pia kuchukua fursa hii ya awali kabisa, kumpongeza sana Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa hotuba yake nzuri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara. Hotuba yao hii ni nzuri na sisi wanawake inatupa changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi sana naomba kumpongeza kwa moyo wa dhati, Mheshimiwa Rais akaya Mrisho Kikwete, kwa kutupa fursa kubwa sisi wanawake katika Awamu hii ya Nne ya Uongozi. Kila mtu atakubaliana na mimi kwamba, wanawake tumeongezewa fursa katika uongozi, katika elimu na katika nyanja zote za maendeleo na kwa hiyo, hatuna budi kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu. Lakini pia tumpongeze msaidizi wake wa karibu sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye amemuunga mkono katika suala zima hili la kuwapa fursa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kabla ya kutoa mchango wangu kwenye hoja hii, nimshukuru sana na kumpongeza sana Naibu Spika, Mheshimiwa Anne S. Makinda, kwa jitihada zake kubwa za kutetea masuala mengi ya kuendeleza wanawake. Jitihada zake zinaeleweka kwa kila mmoja wetu. Bila kumsahau Mwenyekiti wa UWT

Taifa, Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, wote wawili, pamoja na wengine, ambao siwezi kuwataja hapa, kwa jitihada zao kubwa za kuendeleza wanawake kisiasa, wametufikisha mahali hapa tulipo. Hongereni sana dada zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba sasa nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Mimi nitachangia katika maeneo machache, kwa sababu maeneo mengine ambayo nilitaka kuyachangia, yamezungumziwa kwa ufasaha na msisitizo wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nianze na Bajeti ya Serikali. Sote tunaelewa kwamba, katika nchi yetu wanawake idadi yetu ni kubwa kuliko ya wanaume. Kuna asilimia 51, nadhani na zaidi na wanawake tuna vipaumbele vyetu. Kwa hiyo, nitakuja kueleza kwa nini tunalenga pia kuzungumzia Bajeti ya Serikali kwa mtazamo wa kijinsia.

La pili, Sera ya Taifa inaipa kipaumbele maendeleo ya wanawake katika nyanja mbalimbali na hasa katika uchumi na waathirika wakubwa katika suala zima la umaskini ni wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, shughuli zetu za kilimo zinalenga wanawake na Serikali yetu ya Awamu ya Nne, imelenga zaidi kuboresha kilimo. Sasa watendaji wakubwa katika shughuli hizo kuanzia kulima, kupanda, kupalilia, kuvuna na kuweka ghalani, zinafanywa na wanawake kwa wingi zaidi kuliko wanaume. Kwa hiyo, uboreshaji wa sekta hii ya kilimo tungeomba pia ulenge wanawake kwa maana ya kuwapa elimu na nyenzo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la uhaba wa maji na ukosefu wa miundombinu sahihi, linaathiri zaidi wanawake. Bila maji katika vijiji vyetu na suala zima la miundombinu, si rahisi wanawake wakafanya kazi zao kwa ufanisi, hasa za ujasiriamali. Kwa hiyo, ndiyo maana nikasema kwamba, tuangalie Bajeti yetu ya Serikali katika mtazamo wa kijinsia ili kuwapunguzia wanawake mzigo na kuwapa fursa ya kufanya miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti sina maana kwamba, wanawake tuwe na bajeti yetu. Maana yangu hapa ni kwamba, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, iangalie ni nani yupo pale katika kutengeneza Bajeti ya Serikali ili iweze kunufaisha wanawake na hatimaye waweze kunufaika na suala la zima la maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nataka kulichangia ni suala zima la ujasiriamali ama uwezeshaji wanawake kiuchumi, ambalo wenzangu wamelizungumzia kwa ufasaha na msisitizo. Lakini na mimi pia nitaliongelea kidogo kwa kusisitiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo kwanza, niipongeze Serikali kwa sababu ni mwaka mmoja tu tangu fedha hizi za Mfuko wa Rais zitolewe. Lakini katika mwaka huo mmoja, kuna ufanisi mkubwa sana. *SACCOS* zimeanzishwa katika mwaka mmoja, vikundi mbalimbali vimekwishapokea mikopo na vimekwisharejesha mikopo.

Huo ni ufanisi wa hali ya juu. Mara nyingi sisi tunaangalia yale ambayo ni maovu tu, lakini yale ambayo ni ya ufanisi mkubwa, hatuyatambui kwa haraka na kuyasemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kueleza kwamba mimi ni mtaalam wa kutoa mikopo kwa miaka mingi tu, kwa hiyo, naelewa ugumu wa suala hilo. Kwa hiyo, sina budi kuipongeza sana Serikali katika eneo hilo kwamba, imeweza kwa muda mfupi sana, ikahamasisha na kutoa mikopo na kurejesha mikopo ni kitu kipya katika mfumo wa nchi yetu kwa upande wa Serikali. Kwa hiyo, hatuna budi kuipongeza Serikali na tutaendelea kushirikiana nayo na tuna uhakika kwamba, japo kuna matatizo madogo madogo kwa sababu shughuli hii ni mpya, lakini nadhani kadri shughuli zinavyoendelea, mambo yatarekebishwa na kila mtu atapata fursa ya kukopa na hatimaye sote tutanufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na shughuli hiyo. Kuna kilio cha wananchi ambacho ni cha muda mrefu sana, hata kabla mikopo hii ya Mheshimiwa Rais, haijaanza kutolewa. Taasisi zote zinazotoa fedha za mikopo ama za aina hiyo, zinatoza riba kubwa. Sasa hiyo riba kubwa imekuwa kilio cha wananchi kwa muda mrefu, hususan wajasiriamali wanawake na kwa kuwa hiyo riba inawanyima fursa pia watu wengi kukopa, nadhani sasa ni wakati muafaka Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, itupie macho suala hilo kwa sababu kimekuwa kilio kisicho na mwenyewe. Watu wanalalamika kuhusu riba lakini miaka inasonga mbele. Tunaomba Wizara iweze kujizatiti kuangalia mfumo huu ikishirikiana na Benki Kuu, ambayo inaratibu Taasisi za Fedha zinazotoa mikopo ili waweze kuliangalia suala la riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake, ameeleza kwamba, wametoa mafunzo kwa wajasiriamali, lakini mafunzo hayo yametolewa miaka mingi na kwa muda mrefu bila ufanisi mkubwa kuonekana. Sasa tunaomba Wizara, wale wote ambao wamepata mafunzo, wahakikishe kuna ufuatiliaji wa kufikisha hayo mafunzo kwa wajasiriamali wenyewe vijijini. Kuwe na namna ya ufuatiliaji, mafunzo tu watu wanajifunza wanaweka pembeni makabrasha na Bajeti ya Serikali itakuwa imetumika hapo kuwapatia mafunzo watu, lakini bila mafanikio. Kwa hiyo, ni jukumu la Wizara kuweka mikakati ya hali juu, iweze kufuatilia mafunzo, kwa sababu elimu ya uelewa ni muhimu sana katika nyanja hizi za ujasiriamali na hasa kwa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki zetu hapa nchini, kama *CRDB* na *NMB,* zimesaidia katika kutoa mikopo ya kupambana na umaskini. Lakini nilikuwa natoa pendekezo kwamba, Benki Kuu na Benki ya Biashara, nao watoe mchango wao katika kuondoa umaskini nchini kwa kuendesha mafunzo vijijini. Kwa sababu mafunzo ni muhimu sana katika ujasiriamali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka kuzungumzia ni suala zima la masuala ya jinsia ambayo wenzangu wamezungumzia. Bado hii ni changamoto. Unyanyasaji, ukatili dhidi ya wanawake na suala zima la mfumo dume, bado ni changamoto kwa kweli. Sasa tunaomba Wizara kwamba, kwa kuwa Wizara ni Serikali

na Serikali yetu imetuundia hiyo Wizara, hatuoni sababu kwa nini sheria hizi zinazokandamiza wanawake, zisitiliwe mkazo zikaweza kuwa na meno na kushughulikia masuala haya.

Kwa mfano, bado sehemu nyingine ya nchi yetu kama Shinyanga, wanawake bado wanaendelea kuuawa licha ya kwamba, Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanashughulikia. Mashirika haya tunaona kwamba, yanakuwa mstari wa mbele kuliko hata Wizara. Lakini basi Wizara iweke sheria ya kuhakikisha kwamba, suala hili linakwisha. Mbona kuna wanaume wenye macho mekundu lakini wao hawauawi; kwa nini wanawake wenye macho mekundu wanauawa na maeneo mengine ya aina hiyo? Kwa nini Wizara isiweke sheria kali kabisa ikamaliza hili suala na masuala mengine yanayofanana na hayo ya ukandamizaji na unyanyasaji dhidi ya wanawake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia kwa haraka ni la bajeti hii ya mwaka 2007/2008. Tunaona kwamba, katika kabrasha hili Wizara imetenga fedha kwa ajili ya kukarabati majumba ya maendeleo, yale ambayo yanatumika kwa ajili maendeleo ya wananchi. Hali kadhalika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, imetenga pia fedha kwa ajili ya kujenga vyuo vipya. Sasa hili mimi naona kama ni *duplication* ya *resources,* Wizara iliangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Asanteni sana kwa kunisikiliza.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia mambo mawili, matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ulivyokuwa umezungumza leo wachangiaji wamecharuka vizuri sana, wachangiaji wa leo walionitangulia wamenipa raha. Tena natamka kwamba, leo ni raha tupu. Hakuna mchangiaji aliyechangia ambaye amekwenda vinginevyo, isipokuwa kutetea Wizara hii, kutetea wanawake, kutetea jinsia na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono moja kwa moja hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Lakini vilevile nawapongeza sana Waziri, Mheshimiwa Sophia M. Simba, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Salome J. Mbatia, Katibu Mkuu na Bibi Mariam Mwaftisi. Lakini vilevile Wizara hii inasimamiwa na Mwenyekiti Mwanamama, wewe mwenyewe Mwenyekiti Mheshimiwa Jenista J. Mhagama. Hii inathibitisha wazi kwamba, Serikali hii ya Awamu ya Nne, imedhamiria kwa kasi kubwa, kuhakikisha kwamba, ile *fifty fifty* inazungumzwa kwa ukweli na wala si kwa uongo. Wizara imepambika na ukienda huko chini Wakurugenzi ndio hakuna mfano. Wakurugenzi wanawake tele, ingawa na wanaume wamo, kwa hiyo nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingelikuwa kanuni inaruhusu bajeti hii ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii tuimalize hivi sasa, ningetengua kanuni na nikasema tumalize.

Hakuna hoja ambayo tunaweza kusema kwamba, hawa wamefanya hili baya, lakini kwa sababu kanuni hairuhusu, tutaendelea. Lakini ni imani yangu kwamba, jioni sote tutaiunga mkono moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ali Juma Haji, aliyetangulia ni mwanababa. Lakini amezungumzia vizuri kabisa na amehakikisha kwamba, kweli anamtetea mwanamke na kama ilivyokuwa dini yetu inatuambia kwamba, huwezi ukaipata pepo kama hujaunyanyua unyayo wa mwanamke ukaubusu hasa ile ndiyo dhahiri kwamba, tuwaelimishe wenzetu na tuwaenzi akinamama hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia kuhusu Vyuo vya Maendeleo. Aliyetangulia kabla yangu ameanza kidogo. Nadhani Serikali iliwajibika ichapishe vitabu upya kabisa, kwa sababu hali ya fedha ilikuwa ngumu. Lakini nahisi bado haijaangalia baadhi ya mambo ambayo wanafanya *duplication.* Hivi Vyuo vya Wananchi na Wizara ya Elimu nayo imesema kwamba, itajenga kila Wilaya Vyuo vya Ufundi, yaani *VETA*. Sasa rai yangu, Serikali ninaiomba ikae pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa sababu hivi sasa kama sikosei Wizara ya Maendeleo ya Jamii ina Vyuo 58 vya Maendeleo ya Wananchi. Vyuo hivi vimeanzishwa miaka na nia na madhumuni ni ile ile ya *VETA.* Sasa nasema wakae pamoja Mawaziri hawa, fedha zilizotengwa Wizara zote mbili, zilenge mle kwanza, yale majengo mabovu yabomolewe au yakarabatiwe, wapewe uwezo. Lakini tunasema hili halijamalizika unaanza lingine lipya, naomba chonde chonde Waheshimiwa wapenzi wangu Mawaziri wawili, mkae pamoja mjadiliane, mlione hili linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inahuzunisha Wizara hii maisha tunasema kwamba ni kama mtoto yatima. Mtoto yatima imezungumzwa hapa mara nyingi, hana thamani kwa mtu, hana thamani kwa jamii, hela wanazopewa ni kidogo, lakini bado wanaambiwa kwamba, huyo sungura mdogo mumkate tena mkia mumpe mtu mwingine. Shilingi milioni 800 ambazo wamepokonywa hawa, zimesababisha mambo haya yafuatayo na nataja Idara moja tu. Idara ya Maendeleo ya Mtoto ambaye mtoto ndiyo kiongozi wa kesho. Vifungu vichache nitavitaja fedha ambazo wamepangiwa kweli wataweza kuendesha Wizara hii.

Kifungu Namba 20061 wamepewa shilingi 16.8 milioni. Kifungu 600260 wamepewa shilingi 1.2 milioni na kifungu 260400 wamepewa shilingi 540,000 tu. Kifungu cha mafunzo muhimu 260800 wamepata shilingi 4.8 milioni, kifungu 261100 wamepata shilingi 9.7, kifungu 270200 wamepata shilingi 2.1, kifungu 270300 wamepata shilingi 10,000,000, kifungu 270500 wamepata shilingi 13.5 milioni, kifungu 280800 wamepata shilingi 11.6 milioni, kifungu 310300 wamepata shilingi 4.0 milioni. Kifungu 310400 wamepata shilingi 3.2 milioni. Hii ni Idara ambayo inamlea mtoto na ina kazi nyingi, imepangiwa fedha kidogo kama hivyo. Tunaomba sana, chonde chonde mwaka huu hakuna njia, lakini natoa ombi letu, Kamati na mimi binafsi, nasema kwamba, mwakani tuangalie kwa hali yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo lilikuwepo miaka mingi tangu miaka 1995 lilikuwa limeanza hapa ni Benki ya Wanawake. Tumefurahi kuona kwamba,

matayarisho yote yameanza lakini jambo ambalo nalisisitiza, namwomba Mheshimiwa Waziri barua zilizotolewa kwa Wabunge, nadhani hazitoleta kuleta matunda mazuri kama hawatokuwepo Maafisa Maalum katika uwanja huu wa Bunge, wakae na fomu pale, wajaze mbele yao ili fomu zile zikadhaminiwe na Katibu wa Bunge, kama alivyofanya *Community Bank* ya Dar es Salaam. Lakini kwa barua zile kwa Wabunge, sisi wengi wetu zitaishia pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda mbio mbio, nakuja kwenye suala la ubakaji. Mwanababa mwenzangu amezungumza vizuri kabisa. Suala la ubakaji ni jambo ambalo linatilisha aibu kwa nchi yetu sana. Wamezungumza Wabunge wenzangu, mwanamume mzima una umri wa miaka 20, 50 mpaka 60, unamtamani vipi mtoto ambaye ana umri wa miaka miwili au sita, ana raha gani mtoto yule? Inahuzunisha na inatia aibu, kwa baba zima kama mimi nikamchukue mtoto wa miaka 6, 7, 8, 10 au 12; raha gani utakayoipata? Kwa sababu raha ni lazima watu wawili nyie ndiyo muione kwa pamoja, sasa mtoto mdogo yule anaonaje raha! Sasa ushauri wangu, wamezungumza hapa dhana ya wengi kwamba, mwanamume unapomhasi kwamba ndio anakuwa hafai, si kweli. Mwanamume unapomhasi ina maana unamfanya yeye asiwe na uwezo wa kuzaa tu, lakini silaha yake inafanya kazi kuliko zamani. Sasa ushauri wangu tena nasema wazi kabisa, Serikali inisikilize isijidai, maana yake mara nyingi utasikia haki za binadamu, haki za binadamu, binadamu gani hao? Tuamue tunamkata mkono, tunamkata mguu au tunaikata hiyo silaha ambayo imemuharibu yule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir angelikuwepo hapa, kulikuwa na picha ilitolewa mwaka 1995 wanasema: "*Where is our deadly weapon that killed Sister Dorah?*" Sasa *deadly weapon* ni hiyo iliyomuua *Sister Dorah,* basi nayo iuliwe. Asihasiwe, akihasiwa itazidi balaa, akitoka kule hamu atakuwa nayo atawamaliza watoto wote.

Mheshimiwa Waziri, nakwambia tena, Serikali iamue hawa watu waharibifu wanaowaharibu ni viongozi wa baadaye. Mheshimiwa yule kijana aliyeharibiwa juzi ni wa miaka sita, atakuja kukaa hapa kwenye kiti ambacho wewe umekaa na itakuwa aibu. Leo sisi tunamwona *Sister Dorah* yuko pale amekaa juu ya kiti wakati jambazi limemuharibu miaka 20 iliyopita, haifai hayo tuamueni na tunasema tusiogope nchi mbalimbali zinazosema hapana vibaya, hakuna. Tunakuja kwenye biashara ndogo ndogo. Mara nyingi nikisema hapa lazima nizitaje biashara ndogo ndogo. Serikali inapiga kelele juu ya kumwezesha mwanamke. Mikopo inayotolewa yote hiyo ni ya kumwezesha mwanamke na watoto, vijana, lakini sasa tunapanga vingine tunafanya vingine. Bado Wizara ya Maendeleo ya Jamii itafute njia ya kuzungumza na baadhi ya Wizara, nasema tena Wizara ikae izungumze na Majiji yetu haya, kuna mafisadi wanawafisidi makusudi kina mama wasiendelee, kina mama waendelee kunyanyaswa ndani ya nchi hii, itakuwaje ninyi mnawapa fedha mnawakopesha halafu hao hao mnawapiga marungu na jungu la uji wa moto unawaangukia unawaunguza mpaka matiti yao, kweli tunawajali akinamama hawa? Namwambia Mheshimiwa Waziri, atafute njia za busara kuona hayo hayawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa sababu bado dakika zangu mbili, watoto hawa wa mtaani, watoto wasiokuwa na walezi, watoto, wazee waliokufa kwa kila kitu. Natoa ombi kwa jamii yetu, haidhuru kuna watoto wengine wazee wao wote wamefariki lakini bado majirani na watu waliokuwa karibu lazima tuwajali. Hebu tujiulize humu Bungeni, kuna Wabunge wangapi? Lakini tuwaulize Wabunge hao waliokuwemo humu ndani hawana uwezo angalau miongoni mwao kila mmoja kwa uchache, tupewe watoto yatima watano tuwachukue majumbani mwetu. Kama zoezi hilo Mheshimiwa Waziri utalifanya, tafuta wakati wa Bunge uje orodha na mahali vituo ambavyo yatima wapo, imani yangu kama Mzee Ali Hassan Mwinyi aliweza kufanya hayo, siamini kwamba Wabunge sisi hatuwezi. Kwa sababu unapomfanyia wema yule mwenye shida, Mwenyezi Mungu, ndipo anapokuongezea. Lakini unapokuwa wewe unapata fedha tu ukasema nitumie mimi na mke wangu au mke atumie na mumewe, Mwenyezi Mungu atakuadhibu, tena adhabu yenyewe kubwa.

Mheshimiwa Waziri, naomba ombi langu hili ulichukue tena nategemea ataamua kila mmoja maana ninaulizwa hapa nyuma wewe utachukua mwanamke au mwanamume, yeyote nitamchukua. Nitachukua nikawalee watoto wanaume na watoto wanawake, lakini tuhakikishe kila Mbunge mmoja, tunapiga makelele tu hapa. Tukapime UKIMWI, tukafanye vipi, lakini hatujali watoto yatima wanaoteseka katika vituo. Fedha za *NGOs* wanasema wanawahudumia wao, si kweli *it is only 20 percent* ya *NGOs* zinazowahudumia kikweli. Fedha nyingi zinakwenda mifukoni, ndani ya *briefcase* mpaka lini tutakuwa hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja hii mia kwa mia, lakini ombi langu hili ulikubali. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Haroub Said Masoud. Waheshimwia Wabunge, Mheshimiwa Haroub Said Masoud ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii. Naomba nimwite Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na leo niko hapa kuweza kuchangia Wizara hii. Kwanza, nakupongeza kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hii leo na pili nawashukuru Viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani, kwa kutuongoza vizuri katika Kambi yetu. Vilevile natoa pole kwa familia ya Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, pamoja na Wabunge sote tuliofiwa na kuondokewa na Mbunge mwenzetu huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naanza kuchangia hotuba hii. Kwanza, naisikitikia Wizara hii kwa bajeti yake ndogo iliyopangiwa, hailingani kabisa na uzito wa Wizara hii. Nawapa pole Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi ngumu mliyopangiwa. Nataka kuongelea matatizo ya watoto wa kike wanayoyapata. Watoto wa kike naomba wajengewe mabweni kwa sababu watoto hawa wakiunganika pamoja, wanapata hamu ya mapenzi na ikiwapata hamu hiyo wanaweza kubeba mimba na kupoteza masomo yao.

Pindi atakapobeba mimba mtoto huyo baada ya kujifungua, basi naiomba Serikali imrudishe shuleni aweze kuendelea na masomo ili mtoto huyo asinyanyasike. Sasa naongelea mambo matatu. La kwanza ni ubakaji kama walivyozungumzia wenzangu, la pili ni ukeketaji na la tatu ni wazee vikongwe kuuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkeketaji anayemkeketa mtoto inampelekea kutoka damu nyingi na kupoteza maisha. Kwa hiyo, mhalifu huyu maana mimi namwita mhalifu, akikamatwa au akishikwa huyu, hana adhabu yoyote isipokuwa afungwe kifungo cha maisha. Wala wasionewe huruma, kwa kuwa ni mzee kwa sababu wanaofanya kazi hii ni mangariba na ni wazee, kwa hiyo basi, wasionewe huruma kwa umri wao. Nataka kuongelea juu ya ubakaji kama wenzangu walivyozungumza, mbakaji yeyote anayekamatwa, apelekwe Mahakamani na hukumu yake ni kama walivyozungumza wenzangu, ahasiwe. Ahasiwe au afungwe kifungo cha maisha ili na yeye dunia aione chungu, kama yule mtoto aliyemkatishia maisha. La tatu, nazungumzia kuhusu wazee wanaouliwa kwa ajili ya kudhaniwa kuwa wao ni wachawi. Mtuhumiwa anapokamatwa anamtendea unyama mzee wa mwenzake au mzee wake mwenyewe, kwa kumkatakata na kumchinja kama nyama, basi naye huyu auliwe na kama hatouliwa basi huyo naye afungwe kifungo cha maisha, asiweze tena kurudi mtaani akafanya mambo kama yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali naipongeza kwa kutoa mikopo ya wanawake ili kuwawezesha kuanzisha *SACCOS* na kuziimarisha. Lakini nasikia Mfuko huo utapelekwa na Zanzibar. Pindipo utakapopelekwa Zanzibar, basi usitolewe kwa ubaguzi, usitolewe kisiasa kabisa, utolewe na watu wote tuenee kwa sababu sote ni wanawake na sote ni Watanzania. Vilevile nawaasa watoto wanaotembea mitaani kuwa ombaomba. Kila mzazi anahitaji mtoto wake akae naye vizuri na kumtunza ili asiwe ombaomba mitaani. Jambo la kwanza litakalomnusuru kutembea mitaani ni kumpeleka kusoma shule. Mtoto huyo watakapomwona ni sugu, basi ampeleke kwa majiranai wamkanye mtoto wao yule ili asiendelee na tabia ile, isiwe sisi wenyewe tunachochea vitendo hivyo vya kiharamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuokoa muda, sina mengi kwa sababu wenzangu mengi wameyaongelea, yangu ni hayo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nimshukukru sana Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika. Huyu ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii na kule kwenye Kamati anaitwa mama mlezi. Maneno yake ni mafupi, lakini huwa yanakuwa mazito sana. Waheshimiwa Wabunge, nafikiri muda uliobakia hautaweza kuturuhusu kuwa na msemaji mwingine, labda kama kuna msemaji ambaye yuko tayari kusema kwa dakika kumi kati ya Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Maria I. Hewa. Kama ndivyo hivyo, basi ninaomba niwataje wasemaji watakaoanza kuzungumza jioni. Tutaanza na Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, atafuata na Mheshimwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Zainab M. Vulu na Mheshimiwa George B. Simbachawene, atakuwa msemaji wetu wa mwisho kama muda utatutosha kwa wasemaji wote hawa wanne.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutamka majina ya wasemaji wa leo jioni, ninawashukuru wachangiaji wote waliochangia kwa asubuhi hii ya leo. Naomba sasa nisitishe Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.52 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati Kikao kinasitishwa mchana, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Zaynab Vulu na Mheshimiwa George Simbachawene, walikuwa wametajwa. Mheshimiwa Beatrice Shellukindo!

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa hii nafasi ya mwanzo mchana huu na mimi kwa kweli, nichukue fursa hii kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Sophia Simba pamoja na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Hapa niseme tu, mnavyoniona hivi, ujasiri wote huu na nguvu yangu yote hii na kuingia kwangu hapa Bungeni na kabla ya hapo, Bunge la Afrika Mashariki, ni kutokana na kutayarishwa na Mheshimiwa Sophia Simba, yeye ndiye *mentor* wangu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza Katibu Mkuu, Mama Mariam Mwafisi, Wakurugenzi wote ambao wengi wao nimefanya nao kazi, watumishi wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kweli wanafanya kazi nzuri katika mazingira magumu. Naomba nikiri tangu mwanzo, mimi ni Afisa Maendeleo ya Jamii, hiyo ndiyo *profession* yangu ya mwanzo kabla ya kuingia kwenye sekta nyingine kwenye digrii zangu. Tulikuwa tunajiita *Community Development Officers Proper (CDO Proper)*, na ndio maana nina uchungu sana nikisikia mambo ya maendeleo ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo awali baada ya kumaliza Chuo mwaka ule wa 1978 tulikuwa ni Idara tu. Lakini baadae tulipokuja kuwa Wizara, tulifurahi sana, tukafarijika sana. Lakini, kumbe furaha yetu haikuwa ya muda mrefu. Maendeleo ya Jamii ikawa ni jina la Wizara lakini shughuli zenyewe za maendeleo ya jamii zikawa hazipo. Hii nasema kwa dhati kabisa, lakini namshukuru Mungu, hapo baadae ilikuja kuanzishwa Idara ya Maendeleo ya Jamii kama Idara nyingine nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu niseme, watu wengi hawajui maendeleo ya jamii ni nini! Na hii inadhihirika katika mifano mingi sana. Inajieleza yenyewe maendeleo ya jamii, jamii ni nani? Jamii yote tunajua ni akina nani. Lakini cha kushangaza hata Wizara ile ilivyokaa kaa, haijakaa sana kama ya maendeleo ya jamii. Naomba tu niseme Afisa Maendeleo ya Jamii ndiye kila kitu katika jamii, ndiye anajua kuwasiliana nao, ndiye anayejua namna ya kuzungumza. Wengi hapa huwa mnanishabikia, mnasahangaa kuwa nimejua wapi kuzungumza, naweza nikaishi na mtu

wa aina yeyote, mgumu, mwepesi na naweza nikavumilia hali zote, ni kutokana na *background* ya maendeleo ya jamii, tunafundishwa namna ya kufanya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema yote hayo ili tu nionyeshe umuhimu wa maendeleo ya jamii kwa jamii yetu. Naomba niseme kwa kweli kupanga ni kuchagua kama ambavyo walishasema wengine hapo awali. Lakini lazima niseme kwamba pamoja na kwamba fedha ni kidogo, inadhihirisha jinsi ambavyo tunaona hakuna umuhimu wa maendeleo ya jamii hata pale ambapo kuna fedha kidogo halafu bado zinatolewa nyingine. *(Makofi)*

Nadhani wenzangu wamesema asubuhi na Waziri amesema milioni 800 *plus* zimepunguzwa katika kile kidogo kilichopo. Yote hii inadhihirisha kwamba watu hawajui maendeleo ya jamii ni nini na wala wanastahili kupata nini, wanaona tu tupunguze hapa, laiti watu wangejua umuhimu wa maendeleo ya jamii, wasingefanya hilo jambo ambalo limefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vyuo, kwa kweli nasema machache kwa sababu naona mengi yamekwishazungumwa. Utashangaa Wizara hii katika Vyuo vile vya Maendeleo ya Jamii ukijumlisha kwa pamoja inakuja kitu kama bilioni 1.4. Lakini utashangaa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imepangiwa shilingi bilioni 18 kwa ajili ya mambo ya *vocational skills* na hao ukiangalia mwisho wa siku, wanafanya shughuli zile zile. Sasa mimi nasema kwa sababu kupanga ni kuchagua na tusiende kwa mazoea kwa sababu tumezoea namna Fulani, je, Serikali inaonaje ikaunganisha zile shilingi bilioni 18 za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na hizi za maendeleo ya jamii?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hawa tayari wana vyuo ambavyo havitumiki ipasavyo *(under utilized)*, havina *facility* za kutosha, lakini mwishoni mwa siku wanatoa kada ya aina ile ile. Je, kwa nini visiunganike hii bilioni 18 na hii shilingi bilioni 1.4 tukafanya kitu kinachoeleweka na kikaonekana kwa muda mfupi ili tuweze kutimiza ile *slogan* yetu ya kasi mpya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu kuthibitisha kwamba maendeleo ya jamii siyo kitu kinachothaminiwa, siku moja nilikutana na mzazi mmoja akaniambia, Beatrice mimi nahangaika, kila chuo ninachomtafutia mwanangu, nimekosa. Lakini nikikosa kabisa basi mwisho itabidi tu niende maendeleo ya jamii. Ilinisikitisha kwa sababu mimi ni Afisa Maendeleo ya Jamii na ile siyo nafasi ya mwisho! *In fact* mimi naona ni nafasi ya kwanza katika shughuli za nchi yetu tukitaka maendeleo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 54 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, inaonyesha pale jedwali jinsi ambavyo watumishi kwa kweli ni wachache sana hasa katika Halmashauri zetu hizi. Lakini pale pale inashangaza kuona kwenye ukurasa wa 51 wa hotuba hiyo hiyo lile jedwali lenye takwimu pale kuanzia mwaka 2000 hadi 2007, idadi ya watu ambao wameingia kwenye vyuo ukilinganisha na idadi ya watu wanaomaliza, wengi sana hawapo! Hapa naomba Mheshimiwa Waziri nijue tu ni sababu gani inayofanya watu wengi namna hiyo walioanza vyuo kutokumaliza kama ipasavyo. Angalau hata wakipungua watano, inaeleweka labda ni kwa vifo na kadhalika. Lakini

wanapopungua kwa idadi kubwa kama vile, kwa kweli kuna haja ya kuchunguza kabisa ni kwa nini au je, ni ile ile hali ya kwamba maendeleo ya jamii haina umuhimu kabisa?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nasema hivi, maendeleo ya jamii kwa jinsi nilivyosema hapo awali, tumezungumza juzi wachimbaji wadogo wadogo wapewe semina, sijui mambo ya barabara, mambo chungu mzima, sekta hii ya maendeleo ya jamii ndiyo kazi yake, wangekuwa wanapewa fursa hizi, wanakuwa na mtaalamu mmoja mathalani wa madini, wanakuwa na mtaalamu mmoja na wale ambao wanajua lugha ya kuongea na wale watu waweze kuelewa, watumieni Maafisa Maendeleo ya Jamii. Maafisa wa Mandeleo ya Jamii ukienda maeneo mengine kwa sababu ya *frustrations* wamekuwa aidha, walevi, kama siyo walevi wengine wameingia kwenye shughuli za binafsi, biashara, wengine wameamua kuwa wakulima, wamebobea huko, ile kazi haionekani! Hii ni kwa sababu ya *frustrations* na inasikitisha sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi nasisitiza sana, hawa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii japo ni wachache, lakini pia wanaonekana kama hawana kazi kwa sababu kwanza kabisa hawana vitendea kazi na kwa sababu tumesema sasa hivi wahudumiwe na Halmashauri zao, kwa kweli mimi naomba kama ilivyo sekta nyingine ambazo zinaonekana kuwa muhimu kwamba wanapatiwa fedha, basi mimi naomba hawa watu angalau hata kama ni *OC* au mpango wowote wapewe fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisemee Kilindi; nilikutana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya, Mwantumu Dossy wiki iliyopita, nikamwambia mbona kazi fulani na fulani jamani hamfanyi? Lakini ukiangalia ukubwa wa lile eneo, barabara na miundombinu ilivyo hafifu, hawana hata gari! Nikauliza *stationery* mnanunuaje? Akasema ndiyo hivyo, saa nyingine tunapewa na Halmashauri na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani wakati umefika sasa hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii wapewe umuhimu wao ili angalau waweze kufanya kazi kwa kusaidiwa kupewa vitendea kazi na kupewa fedha na pengine hata kama usafiri utapatikana hata yale magari ambayo yametumika Serikalini yanauzwa, basi yasukumeni kwenye Wilaya kule, hawa watu waweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kwamba ni mengi ambayo ningependa kusema katika sekta hii. Lakini, pia moja naomba niliseme, ile Wizara ya Maendeleo ya Jamii ni Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, sasa tunaposema jinsia, hatuna maana ya akinamama tu kwa sababu kuna tabia moja Afrika akinamama mara nyingi huwa tunaangaliwa kwa jicho la tofauti japo Awamu ya Nne nampongeza Mheshimiwa Jakaya Kikwete na Serikali yake, tangu Awamu ya Tatu niseme, wameweza kuongeza idadi ya wanawake, lakini nimeona kwamba niseme ile Wizara nadhani pia inaachwa achwa kwa sababu wamepangwa akinamama tupu, inaonekana ni Wizara ya akinamama. Naomba Serikali, sisemi wale akinamama wahamishwe, lakini nasema naomba tuwe na mchanganyiko ili na wanaume wajue kwamba na wenyewe ni sehemu ya ile jinsia. Tutakapokuwa na mchanganyiko na mawazo tofauti tofauti, nadhani tutaangaliwa na Serikali kwa jicho la tofauti ili na fedha ziende pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile naomba na napendekeza kuwa kuna Maafisa Maendeleo ya Jamii wengi ambao wamestaafu, hawajachoka, lakini wamestaafu kutokana na umri na sababu nyingine, lakini bado wanaweza kazi. Nimtaje hapa, Mama Kwisuja kule Kigoma, Mama Luwilo yuko kule Pwani, Mwalimu wangu Muhungutwa, wapo, akina Mama Mtoka, Musoma wapo wanakaa na wanazeeka na hii elimu. Nasema yaelekea sisi kizazi cha sasa hatujui umuhimu wa maendeleo ya jamii. Hatuwezi kuunda Tume kama zinavyoundwa Tume au Kamati, tuite Kamati ambayo itakaa kwa muda mfupi na kupendekeza ili waweze kuonyesha mwelekeo, Je, tufanye nini ili Idara ya Maendeleo ya Jamii au Wizara ya Maendeleo ya Jamii iweze kufanya kazi zake ipasavyo? Wapo wengi, mimi najua wakitafutwa watatoa maoni na mawazo na tutafika mahali. Kwa sababu awamu hii ni ya ari mpya na mmeshaona kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu huwa anapenda mambo yaende kwa kasi, naamini na hili amelichukua kwa sababu analisikia na ataweza kuona afanyeje ili kada hii itumike ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge, kwa kumalizia, Mheshimiwa Jakaya Kikwete amesema maisha bora kwa kila Mtanzania. Maisha bora Tanzania yatafika pale tu mtakapotambua umuhimu wa sekta fulani fulani hususan sekta ya maendeleo ya jamii na kuipa kipaumbele ili iweze kufanya kazi. Taarifa na maamuzi yote tunayofanya hapa, Maafisa Maendeleo ya Jamii wakikabidhiwa wakielimisha wananchi, tutakwenda kwa pamoja na kwa kasi ambayo kwa kweli itakuwa siyo tu kasi mpya, bali ni kasi ya ajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme nawapongeza tena. Naunga mkono hoja na ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze na mimi kuchangia mawili, matatu kuhusu Wizara hii, tuseme Wizara yetu kwa sababu kama mnavyoona ni Wizara inayoongozwa na akinamama. Kwa hiyo, ni vyema tu na mimi niweze kutoa mawili/matatu kuhusu Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nitoe pongezi nyingi tu kwa Wizara hii kwa namna wlivyoiandaa hotuba yao ambayo inavutia na ina mengi ambayo yanagusa akinamama, inagusa jinsia, jamii, watoto na inagusa wanaume, labda niseme hivyo pia. Kwa hiyo, ninawapongeza sana. Lakini pia niendelee kuungana na mwenzangu aliyemaliza kuzungumza sasa hivi, tunavyoongelea Wizara hii, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, jamani, hata na mimi nimekuwa …hebu ngoja niiseme kwa ujumla; Wizara hii wakati na mimi ningali msichana, nakua, hakuna Wizara niliyokuwa ninaipa kipaumbele na kuiheshimu na kuienzi na kujua ajira duniani hapa au ajira Tanzania hapa ni mama au bwana maendeleo, ndiye niliyekuwa namtambua kabisa. Hata katika mavazi, ukitaka kujua kuvaa vizuri, ona mama maendeleo alivyovaa. Ukitaka kujua uvaaji wa suti nzuri, ona bwana maendeleo alivyovaa, ukitaka kujua upishi mzuri, kajifunze kwa bwana au bibi maendeleo. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa, leo kwa nini hii Wizara inapuuzwa? Hebu tuulizane, kwa nini inapuuzwa Wizara hii? Ukweli kabisa ndiyo Wizara ya mwisho inayopewa mafungu kidogo kabisa

kwa nini? Kwa nini tusiende sambasamba na Wizara zingine? Wizara hii ndiyo inayotutoa kabisa katika kujua mambo mengi ya kimaisha ya kila siku, lakini ndiyo inapunguziwa fedha, ndiyo ukiangalia mpaka hata na Waziri mwenyewe analalamika, anasema Wizara yangu haina fedha! Eeh Mungu, utaiendeshaje? Lakini basi nadhani wahusika, kilio hiki mnakisikia na nadhani mtamfikiria Waziri huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza kabisa ambacho ningependa kuongelea ni kuhusu suala zima la Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Katika hotuba ya Waziri na katika taarifa ya Kamati, wameongea wakiwa wanazungumza suala zima la kuweka kumbukumbu za Mashirika haya, suala zima la kuimarisha vituo vya watoto yatima na watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Ni kweli vituo hivi vipo, *NGOs* hizi zipo. Lakini mimi kinachonishangaza sasa na yameanza kutokea kwamba *NGOs* hizi zilizo nyingi zinaanza kufa kwa sababu zinatangaza kabisa kwamba wafadhili wetu hawana fedha tena za kutufadhii, wameacha kutufadhili kwa hiyo, sasa zinakufa, tena mojawapo iliyo *live* ni ya Kuleana ya kutoka Mwanza tumeiona wote kwenye luninga, tumeisoma wote kwenye magazeti. Sasa sisi pale Mwanza, Shirika hili lilikuwa linabea watoto, kwa kweli lilikuwa linafanya vizuri, siwezi nikalibeza sana na ilikuwa imefikia hatua wanapeleka watoto shuleni. Wakimwona ana maendeleo mazuri, wanampeleka kabisa katika shule ya msingi, anaendelea mpaka sekondari, wanaye, sijui lakini kama waliweza kumfikisha mpaka katika *level* ya Chuo Kikuu. Lakini walau waliweza kumfuatilia mtoto huyu mwenye kuonyesha nia. Sasa wametangaza vita hivyo kwamba hawawezi tena kwa sababu wamekosa wafadhili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii ni hatari na wala sikushangaa nilipoona kwenye luninga hivyo hivyo na kwenye vyombo vingine vya habari, nesi mmoja ambaye anafanya kazi za hatari sana za kuondoka usiku, kakamatwa nesi wa watu, amevunjwa mkono, amenyang'anywa pochi, amefanyajee, anawahi kwenda kazi. Mimi nikahisi tu ni vibaka ambao sasa hivi wameanza kuzagaa mjini Mwanza kwa sababu ya kukosa mahali ambapo walipaswa wawe *confined,* walelewe baadae waweze kuwa na maadili mazuri. Kwa hiyo, katika hali hii kama ndivyo kweli *NGOs* zinafika mahali zinatangaza hatari hii, tunyanyuke sasa, vinginevyo tutafanya vibaka wazagae mitaani, maana ndiko wanakofungiwa hawa watoto, sasa wanapokosa mahali, wanaachiwa huru waende wapi? Wanachukulia wangali watoto wadogo, wanakuwa hawajui kwao. Sasa wanafanyaje baada ya kutangaza hatari kama hiyo?

Naiomba na kuishauri Wizara kwa kweli katika hili kwamba kweli kama zipo *NGOs* ambazo zilikuwa zinategemea *entirely* wafadhili au labda zilikuwa zinatengea sehemu kubwa ya wafadhili, mzifuatile kama Wizara. Tembeeni mzione, isije tukaibua tena kitengo kingine au kikundi fulani cha vijana ambao watakuwa hatari mitaani na hasa hasa wale wanaotembea usiku kiajira au katika starehe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, napenda niongelee sasa la ukeketaji. Ukeketaji, kuna mtu anaitwa kwa cheo cha Ngariba, anayemwita Ngariba na kumuenzi sijui nani! Wanapowabeba hawa watoto kwenda kuwakeketa, wanakwenda wanawatoa sehemu zao za siri hao watoto. Sisi tunajua na tunawaona na tunawafahamu. Serikali inatangaza katika taarifa zake, ongezeko la vifo vya watoto, wanatangaza surua tu, wanatangaza

malaria, wanatangaza magonjwa mbalimbali na UKIMWI, hivi, nani anatangaza vifo vya wakeketwaji? Watoto wengi sasa hivi kwa taarifa yenu wanakufa kwa sababu ya ukeketaji. Wamejifunza mbinu mpya hawa Ngariba hawa! Sasa hivi kwa vile Taifa linatangaza kukamatwa hawa wakiwa wanawapeleka porini kwenda kufanya mambo yao ya kutoa hizo sehemu hizo, wameshagutuka.

Sasa hivi wanawakeketa watoto wachanga, Bunge hili napenda lisikitike sana katika hili. Wanakeketa watoto wachanga kwa sababu mtoto anapozaliwa sijui ndio wanawaita hawa Ngariba nyumbani, nadhani wanawaita nyumbani, maana kwenda porini huko na mama bado ana maumivu, ni shida. Anaitwa huyo, akwenda kumkeketa mtoto mchanga. Bado mtoto ana kitovu kibichi, naomba mumsikitikie mtoto huyu wa kike, jamani! Ana kitobu kibichi, bado anaongezewa donda la pili kwenye sehemu zake za siri. Bado mtoto huyu, *let's say* anakua, akikua, anasubiriwa tena teso lingine la tatu la kuzaa, maana wakati wa kuzaa lazima atapasuka tu kwa sababu ya lile kovu, anapasuliwa tena anashonwa, teso lake la tatu. La nne, mwanamke huyu sasa kakua, anasubiriwa na teso la mfumo dume na la tano kufa!

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli jamani huyu Ngariba huyu, napenda nipendekeze, mimi sitaki wanyongwe, haki za binadamu zitanipigia kelele. Lakini niombe, hivi kama tunaweza kuwasaka majambazi, kama tunaweza kuwasaka wahalifu na kuwapigia kura za siri, kwa nini sasa hivi isifike kwenye makabila husika tupige kura za siri kuwasaka mangariba hawa! Tuwapate, wapatikane, wahojiwe na wakiri kukana tendo hili hadharani, peke yake ndiyo tutapunguza haya madhara ya kudhalilisha jinsia hii. *(makofi)*

Mimi bahati nzuri natoka kwenye kabila ambalo haligusi sehemu, si mume wala mke. Lakini kabila ninazozifahamu, mnazidi mno! Acheni na komeni jamani! Mwanamke anastahili heshima yake ya kuishi na kufa akiwa na viungo vyake vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa niende haraka haraka hasa kuhusu hivi vyuo hivi ambavyo kwa kweli ni vibovu, ni vibovu, ni vibovu! Chuo kimojawapo ni Buhare ambako Mheshimiwa Anna Abdallah kweli alikuwa huko kwa miaka nenda rudi, mama wa sifa yake huyu, alikuwa ndiye Mkuu wa Chuo hapo! Kimekwisha, kimekwisha na ni cha wasichana jamani!

Naomba, sijakataa kwamba Wizara haijagusa popote, lakini, hebu nacho mkififikirie, naomba mkifikirie Chuo cha Buhare, Musoma. Wanawake nawatafuta mahala popote nchi nzima walipo pamoja na kwamba natoka Mwanza, lakini mahala panapoguswa mwanamke mimi lazima niseme! Jamani hao wanawake wafikiriwe Chuo chao hebu naomba mkitembelee Mawaziri wangu. Kitembeleeni, muone jinsi mtakavyoweza kukisaidia, ni Chuo cha zamani, kinafundisha watoto *Certificates,* naomba muende mkakione kama nacho hata mnaweza mkabana bana, kwa sababu mimi pendekezo langu la mwisho ni kuomba jamani hizi fedha kidogo mlizotoa kwenye Wizara hii, hebu zirudisheni jamani tukapate walau kukihudumia hicho Chuo cha Buhare, tukapate walau kutoa elimu. Asubuhi walisema wanaume waelimishwe kuhusu suala zima la ukeketaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu kweli na lenyewe liingie angalau kwenye fungu hilo. Mwanamme akielimika, mkizaa mtoto katika hali niliyoisema leo, akizaliwa mtoto wa kike, hivi kweli wewe mwanaume utakubali mwanao aende akachezewe ovyo ovyo! Hebu basi mfike mahali hawa wanaume waelimishwe. Akimbeba na kwa vyovyote vile atakuaga tu kwamba naenda mtoto hivi hivi, si unakataa! Kwa hiyo, jamani hizi hela hebu niombe Wizara, hebu rudisheni basi, tuione Buhare na tuone jinsi ya kuweka katika mafungu ya kuelimisha, ya kutoa elimu kwa maana ya kuzuia masuala mazima haya ya ukeketaji na kudhalilisha akinamama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, *fifty fifty*! Wamesema, binadamu wote ni sawa, maana wewe ukisema uko hivi mwanaume, ulivyo wewe sivyo nilivyo mimi na mimi nilivyo na wewe siyo hivyo. Sasa lazima tukutane mahala tukubaliane wote ni sawa. Sasa basi hebu ifike hata kama basi tumewahi mno, lakini liwaingie kikweli kweli kulijadili suala zima la kuwa *fifty fifty!* Tunatosha! Wanawake vipi, tunatosha au siyo? Tunatosha au hatutoshi? Tunatosha wanawake! *(Kicheko/Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Sana tunatosha! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, baada ya hapo naunga mkono hoja! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana! Awali ya yote, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara kwa hotuba nzuri iliyotoa na mafanikio japokuwa wananyimwa fedha za kutosha, lakini jitihada zao tunaziona na sisi tuko sambamba nao, tunawaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, kwa kuwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni Wizara mtambuka, inaingia kila mahala, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze Mhehimiwa Rais kwa zoezi alilolifanya kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja kwa kwenda kuhamasisha jamii na yeye mwenyewe akiwa mfano katika kupima virusi vya UKIMWI. Kwa hakika, kwa kumbukumbu zangu, yeye ndiye Rais wa kwanza katika Bara la Afrika kwa kutoka hadharani na kupima na kuhamasisha jamii ili na sisi tutoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika napenda na mimi nichukue nafasi hii kwa wenzetu wa Upinzani kwa kuona suala hili kwamba ni la Kitaifa na wao wakajitokeza, naomba wawe na moyo huo huo, bila kusahau waandishi wa habari wa Kimataifa na wa Taifa hasa wa *BBC* ambao na wao walirusha matangazo kwa kipindi kirefu kwa siku ile ili kuelimisha jamii na dunia kwa ujumla kuona Rais wetu anavyopenda wananchi wake na ndio maana akasema Tanzania bila ya UKIMWI inawezekana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na nilikuwa na sababu ya kuanza na utangulizi huo kwa sababu Wizara hii ina mzigo mkubwa. Inatulea sisi wanawake, wanaume na jamii yote kwa ujumla. Lakini tatizo kubwa lipo kwa watoto ambao mimi mpaka sasa hivi ninapatwa na kigugumizi. Sijui mtoto yuko kwenye Wizara

gani na katika hizi Wizara nyingine zote sijui imejiweka vipi kwa sababu ukienda kwenye Maendeleo ya Jamii mtoto unamkuta, ukienda kwenye Wizara ya Elimu mtoto unamkuta, ukienda Wizara ya Sheria mtoto unamkuta, ukienda Wizara ya Usalama wa Raia mtoto unamkuta, ukienda Wizara ya Fedha, mtoto pia unamkuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapozungumzia suala la mtoto yatima, kuna mtoto yatima ambaye anakwenda kwenye shule za msingi na kuna mtoto yatima ambaye anatakiwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na yeye aonyeshe anamsaidia vipi mtoto huyo. Sasa nini chimbuko la watoto yatima katika nchi yetu. Watoto yatima wengi wanatokana na vifo vya wazazi wao kufa kutokana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Sasa basi Serikali, imeweka mkakati gani kuweza kuwasaidia watoto yatima? Watoto yatima wengi tunasema walelewe na jamii. Lakini jamii tumeandaa vipi kulea? Huko vijijini tunakosema watoto wapelekwe wakalelewe nako wana matatizo, chakula shida, kulala kwake tatizo, maji hajua atayapata wapi, akitoka asubuhi aende akatafute kuni aje akae chini aanze kumtunza yule mtoto. Unaweza kumkuta pengine mtoto huyo yatima na yeye tayari ameshaambukizwa virusi vya UKIMWI. Huyo mama hapo hapo bado ana watu ndani wagonjwa au ana wazee anaowalea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sijui jamii imeandaliwa vipi na Wizara hii. Hili nilikuwa nataka pia nipate ufafanuzi. Matokeo yake hawa watoto yatima wanatoka vijijini kwa kukosa huduma muhimu. Unaweza kukuta haendi shule hana mtu wa kumlipia ada, hana mtu wa kumnunulia *uniform*, hakuna *NGOs* zozote zinazowasaidia kule matokeo yake mtoto yule anatoka anakwenda Dar es Salaam, akifika Dar es Salaam anakuwa omba omba kwa bahati mbaya anaweza akadanganywa kama akiwa msichana kwa sababu ya shida na yule mtoto akakubali, akijikuta kabla ya umri wake amebebeshwa mimba bila kutarajia.

Sasa mimba hiyo anayoibeba, inawezekana mzazi anajua au mzazi anajua au mzazi hajui. Lakini matokea yake mzigo ule unabaki wa yule msichana peke yake hakuna popote Serikali inapoweza kusema inamsaidia. Lakini ndiyo maana nikasema mtoto pia kwenye Wizara ya Usalama wa Raia, naye anaingia, yule mtu anajulikana. Kama yule mtu anajulikana kwa nini basi wasitolewe hata kwenye tangazo la gazeti kuwa *wanted?* Akamatwe, ahukumiwe kama tunavyofanya kwa majambazi, kama tunavyofanya kwa watu wengine ambao nao wanafanya uhalifu. Kwa hiyo, na ule pia nao ni uhalifu wa aina yake.

Sasa hao watoto yatima ndiyo matokeo yake tunakuta wengine tunawaita wanaishi katika mazingira magumu, wengine tunasema hawana walezi, lakini walezi hatujawaandaa. Kwa hiyo, ni jukumu la Wizara, Bajeti yenyewe ndiyo finyu kama hivi sijui sasa watakachokifanya hapo ni kipi kiweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye shule mtoto kwa Mkataba wa Kimataifa ambao tumeingia mtoto ana haki ya kila kitu, ana haki juu ya sheria zake, ana haki ya elimu, ana haki ya kupata afya bora, ana haki ya kupata chakula na ana haki ya kucheza. Lakini ni shule ngapi ambazo zina viwanja vya michezo katika Mikoa au Majimbo yetu mpaka sasa hivi? Kama hakuna je, Wizara husika utakuta tena mtoto anaingia kwenye

Wizara ya Ardhi. Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuandaa viwanda vya michezo kwa watoto hao kwa sababu ni muhimu watoto na wao wapate michezo. Sisi wenyewe mfano mzuri Jumamosi, tunakwenda kwenye michezo, sasa iweje watoto tuwakoseshe viwanja vya michezo na wao waweze kupata nafasi ya kucheza ndipo tutakapoweza kuinua vipaji na wao wakapata ajira na tukaleta maendeleo ya Tanzania kwenye nyanja za michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nilikuwa naangalia jedwali la kwenye kitabu cha hotuba ambayo ipo ukurasa wa sita. Kuna idadi ya watoto ambao wanasomeshwa katika vyuo vya watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Nimeangalia idadi hii na ukiangalia idadi ya watoto wa mitaani unakuta idadi ni ndogo sana. Sasa sijui Serikali ina mkakati gani wa kuweza kusaidia kuongeza idadi ya wanafunzi hao ili na wao wawe walimu kwa wenzi wao ili na wao wawe changamoto kwa wenzi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine hili ni suala letu sisi wenyewe jamii, tuangalie tulikotoka, malezi ya sasa hivi yanatisha. Kuna ule msemo ambao hata mama yetu Mama Salma Kikwete amesema mtoto wa mwenzio ni mtoto wako, lakini sasa hivi maeneo mengi unakuta wanasema mtoto wa mwenzio ni mkubwa mwenzio au mtoto wa mwenzio siyo wako. Sasa hili ni tatizo, maadili yamepungua, Maafisa Maendeleo ya Jamii wanapaswa warudi kwenye maeneo ya jamii wakasaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika na sisi wenyewe turudi kwa jamii tuweze kwenda kusaidia ili kurudisha malezi yetu ya kizamani. Awe mtoto wa mwenzio ni wako, anapokosea umkanye lakini siyo anapokosea unamwacha au ndiyo wa kwanza wewe wa kumsaidia kufanya maovu. Hilo ni tatizo kubwa sana na tusipoliangalia kwa kweli jamii yetu itakakokwenda ni kubaya zaidi, tutakapofikia itakuwa kama wenzetu wa Ulaya, ambao wenzetu wamepitia kwenye *process* kama hii ya kwetu lakini ikafikia mahali wamekuwa na sheria zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi tusipoangalia mtoto wa mwenzio ukitaka kumgusa unapoona ni kosa hilo ni tatizo kubwa. Tuwe na wajibu wa kwamba kila mtu mtoto ni wake, tuone kwamba ni mtoto wake, anapokosea basi uweze kumrekebisha, siyo unamuona mtoto mwenzio kamtunza vizuri kwa mfano ndiyo kwanza unamsodolea unakwenda unambebesha mimba unamwacha, hilo ni kosa. Mtoto wa mwenzio unapoona ana njaa unatakiwa usogee umsaidie. Chukua kilo moja, mbili ya chakula umpelekee badala ya kumfanya huyo mtoto aonekana amepotea hana wazazi, hana jamii inayomzunguka. Kwa hiyo, tukiliangalia hilo nafikiri tunaweza tukafika mahali panapoweza kutusaidia na sisi tukaongoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imefanya tafiti ya kutosha na ya kina, katika ukurasa wa 16 wamesema kwamba walifanya utafiti wa kuona nini ongezeko la watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Lakini sababu kubwa ya mafanikio haya ya hizo tafiti wamegundua kwamba tatizo kubwa ni umaskini uliokithiri katika jamii zetu. Sehemu kubwa ya maskini katika jamii zetu ni wale wanaoishi vijijini ambako kuna matatizo mengi ambayo yanahitaji kupata msaada wa hali ya juu na isitoshe na kupata elimu ya hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba tu Wizara inisaidie kunieleza nini mkakati wa Serikali kuhusu hawa watoto yatima na watoto wa wanaoishi katika mazingira magumu na hata kuangalia kwa nini basi kuna baadhi ya shule watoto wawe wanachapwa na hili tatizo tulilitoa huna sababu ya kumchapa, unachopaswa kuchapa ni kuona nyoka mpige, ukiona mkubwa mwenzio mpige lakini usimpige mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja nashukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani mimi nitakuwa ndiyo mchangiaji wa mwisho. Ukiwa mchangiaji wa mwisho kuna hasara zake. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Wewe sema tu.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa mchangiaji wa mwisho kuna hasara kwamba unaweza kukuta mengi yamesemwa na wengi lakini na mimi nina jambo kidogo ambalo nilitaka ku-*share.*

Kwanza nimpongeze Waziri wa Wizara hii, pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii na watumishi wote kwa hotuba nzuri ambayo wametuletea wakiomba fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli za Wizara hii. *(Makofi)*

Lakini mimi nilikuwa na jambo ambalo nilipenda na mimi niliseme kwamba kwa namna yoyote ile itakavyokuwa hatuna njia mbadala inayoweza ikazidi wajibu wa wanafamilia katika kutunza watoto wao. Tutatengeneza vituo, tutaanzisha *NGOs* mbalimbali, lakini bado msingi na wajibu wa watoto kulelewa ni wajibu wa wazazi na wanafamilia kwa ujumla. Niliposoma katika kitabu hiki ukurasa wa 21 wamezungumzia kwa kifupi juu ya suala la familia na kwamba hata mwaka jana wameweza kuadhiminisha siku ya familia.

Mimi nilikuwa na wazo tu kwamba basi mkazo mkubwa uwekwe katika kuifanya hii siku ili iweze kutoa matunda yanayokusudiwa. Hakuna kitu muhimu kama familia. Msingi wa jamii ni familia na jamii ndiyo inayounda Taifa. Kama jamii itakosa maadili kwa hakika hakuna Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa mfano mmomonyoko uliopo wa maadili katika familia ndiyo unaopelekea matatizo mengi ambayo yanasemwa hapa. Mimi ningeshauri kwamba ni vema sasa Wizara ikafikiria badala ya kufikiria tu habari ya jinsia kwa namna ambayo tafsiri kubwa inafanywa hapa tafsiri kwa maana kama ya wanawake hivi. Lakini jinsia ni ya wote wanaume na wanawake. Hata pengine tafsiri ya Wizara yenyewe hii inatafsiriwa pengine tofauti na tafsiri hali ya Wizara yenyewe. Wizara hii ni ya maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto hapajasemwa kwamba ni Wizara ya Wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Wizara hii ina wajibu mkubwa wa kuangalia namna gani tujenge familia zetu, namna gani tuondokane na matatizo ya kijamii katika hali ya sasa ya utandawazi na maendeleo mbalimbali duniani.

Mimi ningefurahi kama katika mtazamo wa familia kwa sasa kama Wizara hii itaona umuhimu wa kuanzisha somo la familia likafundishwa kuanzia mashuleni. Wajibu mwingi unaokwepwa na unaosababisha watoto wanaoishi katika mazingira magumu yanatokana na wanafamilia kutokujua wajibu wao. Ni imani yangu kubwa ni kwamba inatokana na watu kukwepa wajibu wao kama wangefundishwa wana jamii na wafamilia kuhusu wajibu wa kuwatunza ndugu zao haya yote yasingelikuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie mmomonyoko wa maadili katika jamii na nianzie pale pale kwenye familia kama ninavyosema kuna haja ya kuanzisha mtaala wa kufundishwa mashuleni juu ya wajibu na mambo mbalimbali katika familia. Katika sheria kuna sheria lakini pia kuna *morals* ambazo nazo zina-*behave* kama sheria lakini hazina *sanction. Morals* huwezi ukahukumiwa kwa ku-*derogate* au ku-*offend moral*. Lakini mtu anahukumiwa kwa ku-*offend* sheria. Katika hali hiyo, mimi nadhani kama *moral* imekuwa *offended* na ni *moral* ya muhimu sana ni afadhali *moral* hii ikatungiwa sheria. Hatuwezi leo tukasema kwamba watu waachiwe tu kwa sababu ni uhuru wao kwa mfano ukipita hata barabarani unamkuta mtoto wa kike au mtoto wa kiume amevaa nguo ya ajabu sana. Tunazungumzia UKIMWI hapa, unamkuta mtoto wa kike amevaa kinguo kiko karibu kabisa na nanihii hapa. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Nini?

**MHE. GEORGE SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, na unamkuta akijitahidi sana amevaa ya kubana sana na yenyewe *transparent*. Sasa katika hali hii kama tutasema tu mambo haya yajiendee tu tukayaacha tu yajiendee tu mimi naamini baadaye familia itakufa. Kuna haja Serikali ikatengeneza sheria kama nilivyosema kwamba *morals are not enforceable.* Lakini inapofikia kwamba inakwenda kuua kiini cha uwepo wa familia na utamaduni wa Taifa ni muhimu tukaiwekea sheria. Hivi tukisema leo hii tutunge sheria kwamba mtoto wa kike ukivaa nguo angalau ifike kwenye goti kuna ubaya gani? Hivi tukisema kwamba leo tutunge sheria kwamba nguo unapoivaa isiwe *transparent* ya kuonyesha maungo ya mwili kuna ubaya gani? Kwa hiyo, mimi ningeshauri Wizara i-*look forward* na iangalie kazi hii ambayo ni ngumu kuangalia *the way* jamii inavyoji-*behave*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili ku-*preserve* hiki ninachokisema na mimi nimeamua nizungumzie hiki kimoja tu kwa maana ya familia, tumekuwa na sheria toka enzi ya mkoloni tulikuwa tuna sheria ya *Affiliation Ordinance*, tumekuwa na *Adoption Ordinance* na baadaye zimekuwa *Acts* lakini baadaye tumekuwa na *The Home of the Child Act* na baadaye tumekuja kuwa na *The Law of Marriage Act 1971*, hizi zote ukiziangalia zinajaribu kujenga kitu kinaitwa familia kwa sababu familia ndiyo mwanzo wa Taifa lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiziangalia sheria hizi kama zingefuatwa na kama zitawekewa mabadiliko kidogo kwa mapungufu yaliyojitokeza kulingana na wakati wa sasa bado zina uwezo wa kufanya kazi nzuri sana na hata haya matatizo yanatokea kwa watoto yatima wanaowekwa vituo wanatelekezwa yasingekuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, familia, ni kitu kitakatifu, kama Wizara hii haita-*devote* muda wake na kazi yake kubwa kuhakikisha kwamba familia zinastawi, hatutakuwa na jamii iliyo na kiwango cha ustaarabu. Hali ya sasa ya maadili ni mbaya sana, yamezungumzwa mengi hapa lakini yote yanatokana na kuanguka kwa maadili katika familia, baba ameshindwa kuchukua wajibu wake, mama ameshindwa kuchukua wajibu wake, mtoto ameshindwa kuchukua wajibu wake na ndiyo sasa sababu ya kuanguka kwa maadili katika familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya Serikali ikatukumbusha kwa kutumia hata sheria juu ya wajibu wetu katika kutunza na kulea familia zetu. Haiwezekani mtoto wa kaka yako ukashindwa kumtunza ukasema huyu ni yatima, haiwezekani mtoto wa dada yako ukashindwa kumtunza ukamtangaza kwamba ni yatima, haiwezekani mtoto wa jirani yako ukashindwa kumsaidia na anapokuomba msaada unamgeuza mke, hii ni mbaya. Ni kwamba maadili katika jamii yameshuka. Serikali ifanye kitu, zamani hata hizo *morals* zilikuwa zina namna yake. Nakumbuka kuna makabila kama Wamasai, Wairaki walikuwa wanawatenga wale watu wanaofanya makosa katika jamii. Mtoto akizaa kabla ya kufika muda wa kuolewa akapewa mimba anatengwa na jamii. Kulikuwa kuna *selection,* leo hii mimi sioni kama kuna ubaya kama tutaweka sheria ili iweze kushughulika na wale wanaokiuka maadili. *(Makofi)*

Mimi sina matatizo na *fifty by fifty*. Lakini hii *fifty by fifty* isije ikawa ni zawadi, iwe *subject to competition*. Ikiwa kama zawadi baadaye mtaambiwa *seventy by thirty,* baadaye mtaambiwa *eighty by twenty* hapa hapa. Mimi naamini kwamba *this thing should go gradually* vitaenda, viende taratibu. Twende taratibu lakini leo *fifty by fifty* kesho mtaseme *sixty by forty* nadhani twende *gradually* sina ugomvi na hilo lakini liwe *subject to competition. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie la mwisho juu ya sheria ya mirathi. Sheria ya mirathi inaawatesa sana akinamama na inawatesa sana akinamama kwa sababu ya msingi wa sheria yenyewe. Msingi wa sheria ya mirathi inatokana na maamuzi ya familia baada ya kifo cha marehemu hasa inapotokea kwamba aliyekufa ni mwanaume katika familia basi kikao kile kinapokaliwa huwa kinakaliwa kwanza hakina *limitation of time*, hawasemi lini kikao kitakaa. Kikao kile cha familia kinapokaa hukaa katika wakati ambao huyu mama mjane yupo katika majonzi makubwa sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, anashurutishwa na kujikuta amekubaliana na maamuzi ya wanafamilia ambayo kwa wakati ule wamejifanya wazuri katika kusaidia kumzika mume wake, lakini ni wabaya kwa sababu wanataka kumdhulumu mali zake. Sheria iko wazi inasema kuhusu migawanyo ya mali. Naomba Wizara hii sasa ku-*pressurize* na kuhakikisha kwamba sheria kama hizo zinaletwa hapa Bungeni na kufanyiwa marekebisho. Haiwezekani msingi wa sheria ikawa inatokana na maamuzi ya wanafamilia

waliomshinikiza yule mama afanye maamuzi wakati akiwa katika majonzi makubwa haiwezekani. Wao hutumia msingi ule wa maamuzi wa kikao cha kifamilia kama fimbo eti mimi ndiyo nimechaguliwa na ukoo, mimi ndiyo ninayesimamia, akinamama wengi wanaonewa sana. Ili tuwasaidie katika hili mimi ningeshauri Wizara ilete mabadiliko ya sheria iseme ni wakati gani mama huyu ashiriki vikao vya familia.

Aidha, kile kiapo aende akasemee kwenye Mahakama, siyo wapeleke muhtasari wa kikao cha ukoo ambacho kinaleta matatizo makubwa sana baadaye katika *process* ya kudai mirathi na nani amsimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi ningewashauri akinamama kwamba katika vikao vile vya mirathi msikubali kusimamiwa sema nitasimamia mimi, useme mali hii ya mume wangu tumechuma naye nitasimamia mimi. Anayekuja huyu awe wa kukusaidia tu lakini siyo wa kusimamia mirathi. Kesi nyingi zipo akina mama wanahangaika barabarani kila siku ni mirathi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi huo ndiyo mchango wangu nashukuru sana na naomba kuunga hoja mkono. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulikubaliana kwamba tuwe na wasemaji wanne kwa mchana huu ili tutoe nafasi nzuri kwa watakaojibu hoja halafu tuingie kwenye Kamati ya Matumizi.

Lakini nilitaka kusema mambo mawili. Hii habari ya mirathi nyie wanaume wenye fedha hamuandiki kwamba nitakapokufa mke wangu atakuwa msimamizi wa mirathi hamuandiki. Lakini kama itafikia wanawake wakawa asilimia 70 wanaume wakawa asilimia 30 basi itakuwa *crisis* kwa hiyo hali hiyo haitatokea. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kutusaidia ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliposimama hapa mwaka jana wakati kama huu wa Bunge la Bajeti nilikuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Kwa unyenyekevu na utii mkubwa, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuniteua kwa mara nyingine, safari hii katika wadhifa wangu mpya wa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Ninaahidi kuendelea kufanyakazi kwa ari, nguvu na kasi kwa kushirikiana kwa karibu na Mheshimiwa Waziri wangu mpya na viongozi wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia za marehemu kwanza ya Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti pamoja na maofisa waliopoteza maisha katika ajali ile. Pia familia za Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa, Mbunge wa zamani Mheshimiwa Stephen Kazi, pamoja na Mheshimiwa Omar Chubi, bila ya kuwasahau familia za waliopoteza maisha katika ajali za Singida, Mbeya, Arusha na Mwanga, Kilimanjaro na kwingineko. Mungu azilaze roho za marehemu hawa mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuwapongeza sana wananchi wa Kilimanjaro hususan wanawake kwa kufanyakazi kwa bidii na kuchangia kukua kwa uchumi katika nchi hii, ujumbe wangu kwao ni kuwa nitaendelea kuwa mtumishi wao msikivu, mnyenyekevu na mchapakazi wa hali ya juu kama walivyonilea. Ninawapenda sana na Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru vile vile familia yangu kwa kunipa *support* na upendo siku zote akiwemo mume wangu Joseph Mbatia, watoto wangu Yolanda, Charles, Boniface na Phillip. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, ambazo kwa kweli ni nyingi. Kwanza, nianze kwa kuwashukuru sana wote waliochangia hoja zetu. Kwa kweli hii ni changamoto kubwa kwetu na hizi hoja zinatupa changamoto ya kuweza kuzidisha kasi ya ufanisi wa majukumu yetu katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kuhusu kuupatia Mkoa wa Rukwa watumishi wa kutosha na vitendea kazi, hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Paul Kimiti. Jukumu la kuajiri watalaamu wa maendeleo ya jamii ni la Halmashauri kupitia bodi za ajira. Wizara kupitia washauri wa sekta ya maendeleo ya jamii wa sekretarieti za Mikoa itaendelea kuhimiza Halmashauri kuajiri watalaamu wa kutosha wa maendeleo ya jamii ili waweze kushirikiana na jamii katika kubuni, kupanga na kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo kwa lengo la kuongeza tija na kutokomeza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya mkakati wa kufikia asilimia 50 katika ngazi mbalimbali za maamuzi. Hoja hii imetolewa na Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Fatma Mikidadi na Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya.

Napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge, kuwa Wizara yangu imeanza mchakato wa kufikia asilimia 50 ya wanawake Bungeni, Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Halmashauri na taasisi nyingine zote ifikapo mwaka 2010. Shughuli ambazo zimeshafanyika ni kuunda Kamati ya watalaamu, kwa ajili ya kuwezesha mchakato mzima wa kufikia asilimia 50. Aidha, Wizara pia itaainisha mapendekezo ya mifumo na kuwasilisha kwa wadau kwa ajili ya kupata maoni na kuandaa mpango wa kazi wa utekelezaji ili kufikia asilimia 50 ya uwakilishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wizara inatambua kuwa jukumu la kumuinua mwanamke kielimu ni lake, hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe. Tunakubaliana na Mheshimiwa Dr. Mwakyembe kuwa Serikali inatambua kuwa jukumu ni lake la kuwaelimisha wanawake na imeanzisha mfuko wa kuwawezesha wanawake ambao ni watumishi wa Serikali. Mfuko huo unasimamiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti na Utumishi wa Umma. Aidha, mafunzo yanatolewa kwa wanawake kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na vyuo vingine nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pametolewa hoja kwamba *NGOs* zimekuwa zikifanyakazi kwa ufanisi hafifu na kuna malalamiko makubwa kuhusu matumizi mabaya ya fedha za wafadhili ya kutowafikia walengwa. Hivyo Serikali idhibiti na kufuatilia utendaji wa kazi za *NGOs* hapa nchini, lakini vile vile Serikali iangalie uwezekano wa kuunganisha sheria zote zinazohusiana na usajili wa *NGOs* zipewe nguvu yaani meno katika kufuatilia utekelezaji wa kazi za *NGOs*.

Aidha, Wizara ifuatilie kwa karibu utendaji wa *NGOs*, zinazoshughulikia masuala ya jinsia, watoto na UKIMWI. Hoja hii imetolewa na Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Juma Killimbah na Mheshimiwa Mwinchoum Msomi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuleta ufanisi sheria ya *NGO* inayataka mashirika haya kuwasilisha taarifa za kazi na taarifa ya fedha iliyokaguliwa kwa msajili wa *NGO* kila mwaka. Msajili huhakiki taarifa hizi na kufuatilia ili kubaini usahihi wa taarifa hizi. Wizara pia inaandaa tovuti ambayo taarifa mbalimbali za *NGOs* zitaingizwa.

Aidha, Serikali itafanyia kazi ushauri wa kuunganisha sheria zinazohusu usajili wa *NGOs* na pia kuipa sheria nguvu ya kufuatilia utendajikazi wa *NGOs* kwa kushirikiana na Bodi ya Baraza. Tatizo kubwa katika ufuatiliaji wa kazi za *NGOs* imekuwa ni ukosefu wa rasilimali fedha na vitendea kazi katika kuiwezesha Wizara kufuatilia kikamilifu shughuli za *NGOs*, nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni Mashirika yasiyo ya Kiserikali yapatiwe mbinu zote ili watafiti mipango waweze kufikia malengo ya MKUKUTA. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Vuai Abdallah pamoja Mheshimiwa Maria Hewa. Serikali na *NGOs* ni wabia muhimu katika ujenzi wa Taifa letu. Serikali itaendelea kuzishirikisha *NGOs* katika kupanga na kutekeleza mikakati mbalimbali nchini ikiwemo MKUKUTA. Msukumo utawekwa katika kuzijengea uwezo ili waweze kutekeleza majukumu ipasavyo. *NGOs* zisijikite katika miji na majiji tu, waende pia vijjini.

Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Stella Manyanya, ni kweli *NGOs* nyingi zimejikita sana katika maeneo ya mjini hasa kwa kuwa wengi wanaozianzisha taasisi hizi ni wakazi wa mijini. Serikali kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la *NGOs* litahimiza *NGOs* kutandaa hadi vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Idara ya *NGO* iwezeshwe kifedha ili kusaidia *NGO* za wanawake kuelimisha kuhusu taratibu za usajili wa *NGO*, hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Bujiku Sakila na Mheshimiwa Mwinchoum Msomi. Serikali inatambua umuhimu wa Idara ya Uratibu wa *NGOs* na inafanya jitihada za makusudi ili kuhakikisha kwamba idara hiyo inawezeshwa kifedha. Maoni haya yatazingatiwa katika Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2008/2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha zinazotolewa kwa taasisi mbalimbali kwa ajili ya watoto yatima zitolewe kwa uwazi na utafiti wa kina ufanyike ili kuhakikisha watoto yatima wanatendewa haki. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Ali Juma Haji na Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwazi kuhusu fedha za yatima unatakiwa uwe wa pande zote yaani taasisi zinazotoa fedha kwa *NGOs* zinazolea watoto yatima na pia *NGOs* zinazopokea fedha hizo ambazo wanapata kutoka kwa wahisani ili kuwe na uwajibikaji kwa wadau wote. Sheria ya *NGO* ya mwaka 2002 inazitaka *NGOs* kuwasilisha taarifa ya kazi ya fedha iliyokaguliwa ili kuhakikisha uwazi katika kupokea na kutuma fedha za yatima na kuhakiki kazi zilizofanywa. Msajili wa *NGOs* hukakiki kazi zilizofanywa. Msajili wa *NGOs* huhakiki na kufuatilia usahihi wa taarifa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, taarifa za fedha za *NGOs* zitaingizwa katika tovuti kama ambavyo nimekwishakutangulia kusema.

Kuhusu Bodi ya Taifa ya uratibu wa *NGO* kuwa na uwakilishi Bungeni, hoja hii imewasilishwa na Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, kwa sasa Wizara yangu ipo katika mchakato wa kuteuwa Wajumbe wapya wa Bodi ya Taifa ya uratibu wa *NGOs* ambao watakuwa madarakani miaka 2007/2008 hadi 2009/2010. Hivyo ushauri wa Mheshimiwa Mbunge utazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna upungufu wa Bajeti ya kutosha kuwezesha utaratibu na ufuatiliaji wa *NGOs* Mikoani, kuwezesha Bodi ya Taifa ya uratibu wa *NGOs,* Baraza la Taifa la *NGOs,* usafiri wa kuaminika kufuatilia kazi za *NGOs,* kutoa waledi yaani *awareness* kwa wasajili wasaidizi na wananchi kwa ujumla.

Hoja hii imetolewa na Kambi ya Upinzani na vile vile Mheshimiwa Maria Hewa.

Kuna haja ya kuwezesha uratibu na ufuatiliaji utendaji kazi wa *NGOs* nchini. Serikali katika Bajeti yake ya mwaka 2008/2009 itaangalia uwezekano wa kuongeza Bajeti katika kuratibu *NGOs* na pia kushirikisha wafadhili kusaidia sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie waraka ili fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake yaani *WDF* zipelekwe kwenye *SACCOS* badala ya kupeleka fedha hizo kwenye Halmashauri. Hoja hii imetolewa na Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyambe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake yaani *WDF* ulianzishwa kwa Azimio la Bunge kwa mujibu wa *Exchequer and Audit Ordinance* ya mwaka 1961 kwa lengo la kuwafikia wanawake wajasiriamali hasa wale wa vijijini.

Aidha, Wizara imeandaa mwongozo kuhusu uendeshaji mfuko wa maendeleo wa wanawake ambao pamoja na mambo mengine umeweka bayana utaratibu wa utoaji wa mikopo kwa wanawake. Halmashauri husika ndizo zinazosimamia utaratibu wa utoaji wa mikopo hii kwa kufuata mwongozo huu. Hivyo tunaupokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na tutaufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile naendelea kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuwa wao ni Wajumbe wa Kamati za Mikopo katika Halmashauri wanazotoka na hivyo tunawaomba wafuatilie kwa karibu utendaji wa mfuko huu. *(Makofi)*

Kuhusu Serikali iendelee na taratibu zote muhimu ili kuhakikisha uanzishwaji wa benki ya wanawake, uanzishaji wa benki ya wanawake uwekewe muda maalumu yaani *timeframe,* hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar na Mheshimiwa Margaret Mkanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Kamati na Waheshimiwa Wabunge waliotoa hoja hii kuwa Serikali iendelee na taratibu zote muhimu za kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa kuuza hisa. Uanzishwaji wa benki utategemea upatikanaji wa shilingi bilioni mbili, hivyo Wizara itaendelea kuhamasisha ununuzi wa hisa kama ambavyo umekwishaanza humu kwa Waheshimiwa Wabunge. Tutafanya kazi hii kwa kadri ya uwezo wetu ili kuweza kuanza mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naib Spika, kuhusu hoja ya baadhi ya Halmashauri zinatoa mikopo kwa wanawake kwa upendeleo, hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili kuwa mikopo inayotolewa na *WDF* inatolewa kwa wanawake wote bila kujali itikadi zao. Wizara imeandaa mwongozo kuhusu uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake ambao pamoja na mambo mengine umeweka bayana utaratibu wa utoaji wa mikopo kwa wanawake. Halmashauri husika ndizo zinazosimamia utaratibu wa utoaji wa mikopo hii kwa kufuata mwongozo na Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe katika Kamati za Mikopo katika Halmashauri wanazotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia na hoja kwamba Halmashauri ngapi zimekopesha wanawake na kwa kiasi gani, hoja hii imekuja kutoka kwa Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali ilianzisha mfuko wa maendeleo wa wanawake kwa nia ya kuwafikia wanawake wote hasa wale walio vijijini. Fedha za mfuko huu zimeshatolewa kwa Halmashauri 118. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 916 zimetolewa kwa Halmashauri hizo kwa kipindi cha kuanzisha mwaka 2001 hadi 2007 na marejesho ni mazuri ni kwa asilimia 82. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, je, wanawake wangapi wamefanikiwa kupata mikopo ya mfuko wa uwezeshaji. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Said Arfi, tunaomba kumwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalifikisha swali hili katika Wizara inayohusika kwani jambo hili linashughulikiwa na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ambao wanasimamia mfuko wa uwezeshaji ili kupata taarifa sahihi. *(Makofi)*

Kuhusu vikundi vya akinamama vya uzalishaji vipewe msaada wa kuongeza ujuzi ili waendane na ushindani katika uzalishaji wa bidhaa bora, vikundi hivyo ni Mwanamke na Maendeleo - Kiomboi, Jipe Moyo – Shelui, Maendeleo ya akina mama -

Kinampanda na kikundi cha wanawake – Ndago, hoja hii imeletewa na Mheshimiwa Juma Killimbah.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Juma Killimbah kuwa ni muhimu kwa vikundi vya wanawake wazalishaji kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali. Naomba nimfahamishe Mheshimiwa Juma Killimbah kuwa Halmashauri huwa zinatenga asilimia 10 ya riba ya mfuko wa *WDF* kwa ajili ya mafunzo kwa vikundi vya wanawake. *(Makofi)*

Serikali itamke kupitia Bajeti hii agizo kwa Halmashauri zinazozembea kutenga fedha za mfuko wa wanawake ili waweze kupeleka kwenye Halmashauri husika, hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali ilishatoa agizo la kuchangia mfuko huu kupitia tamko la Waziri Mkuu la mwaka 1995 kuwa Halmashauri zichangie asilimia 10 ya mapato yao katika Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, hivyo kwa mujibu wa tamko hilo Halmashauri zinapaswa kuchangia mfuko huu. Kwa vile Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe wa Kamati za Mifuko ninawaomba wahimize Halmashauri kuchangia mfuko huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala la kukata kabisa watu wanaopatikana na suala la kubaka. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Adam Malima na Mheshimiwa Haroub Said Masoud. Kwa kuwa hili ni suala linalogusa haki ya mtu ya kuishi, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge suala hili litashughulikiwa kwa kuangalia upya Sheria ya Makosa ya Kujamiana ya mwaka 1998 kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba naSheria ili kubaini namna ya kushughulikia masuala yanayopatikana na hatia hii kisheria. *(Makofi)*

Kuhusu suala la kurekebisha sheria zinazowakandamiza wanawake, hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya na Mheshimiwa George Simbachawene, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali inaendelea kufuatilia Sheria zenye upungufu kijinsia. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, Sheria ya Mirathi na Sheria ya Watoto. Wizara itaendelea kuwasiliana na Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu marekebisho hayo. *(Makofi)*

Kuhusu wanawake 500 wamewezeshwa kwa kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali, je, kati ya wanawake hao ni wangapi wanatoka vijijini? Hoja hii imetolewa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Devota Likokola na Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi. Mafunzo ya ujasiriamali yanayotolewa kwa wanawake, huwa yanatolewa kwa wanawake wakati wa maonyesho na hutolewa kwa mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani. Aidha, vikundi vya ujasiriamali vinavyoshiriki huchaguliwa na Halmashauri mbalimbali zilizopo nchini ambako wanawake walio wengi hutoka vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la sheria itoe mafunzo zaidi kwa idadi kubwa zaidi kwa vikundi vya akinamama wajasiriamali, Serikali iongeze fedha za mikopo na irahisishe upatikanaji wa mikopo kwa kuhakikisha kuwa benki zinaondoa masharti

yanayowezesha kufikiwa na wananchi maskini. Hoja hii imetolewa na Kambi ya Upinzani.

Mafunzo bora zaidi yanahitajika kwa akinamama wajasiriamali. Mafunzo ya mara kwa mara yamekuwa yakitolewa kwa makundi mbalimbali yakiwemo makundi ya wenye VVU kulingana na mahitaji. Mikopo mbalimbali imekuwa ikitolewa kupitia taasisi za kifedha. Kulingana na sera za biashara, kila taasisi hujiwekea riba wanayoona inakidhi mahitaji. Serikali imeanzisha mifuko mbalimbali yenye masharti nafuu kwa nia ya kulenga wenye kipato cha chini kama vile mfuko wa maendeleo wa wanawake.

Kuhusu kuanzisha kwa Baraza la Wanawake Tanzania, mchakato wa kuanzisha Baraza la Wanawake Tanzania ulianza siku nyingi na hivi sasa suala hilo liko Mahakamani. Aidha, Serikali ilianza mchakato wa kuanzisha chombo cha wanawake Tanzania chenye lengo la kuunganisha wanawake wote. Suala hili lilifikia ngazi ya juu Serikalini na kuonekana ni vyema Wizara zinazoshughulikia Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iumaarishwe na kama nilivyosema suala hili liko Mahakamani kwa hiyo, kwa sasa hivi mikono yetu imefungwa. *(Makofi)*

Kuhusu unyanyasaji wa wanawake, vipigo visivyo vya msingi, vinavyopelekea wanawake kiuwa na vilema na viungo hata kufa, Wizara imechukua hatua gani? Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Rosemary Kirigini. Katika kushughulikia masuala ya unyanyasaji ya wanawake ikiwemo vipigo ambavyo hatimaye huwaletea vilema vya viungo na hata kufa, Wizara imeendelea kuelimisha wasimamizi wa utekelezaji wa sheria kwa kuhusisha Mahakimu na maafisa wa polisi katika baadhi ya Mikoa kuhusu sheria zinazowalinda wanawake dhidi ya vitendo vya ukatili ikiwemo vipigo. Aidha, mafunzo haya yataendelea kutolewa nchi nzima. Natoa wito kwa wanawake nchini kuhakikisha wanatoa taarifa katika vyombo vya sheria wanapofanyiwa vitendo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wizara iendelee kutoa elimu ya suala la jinsia, maana hata kwenye ngazi za uongozi Mkoani, Wilayani na kadhalika bado jinsia inaonekana kama ni suala la wanawake au linahusu mambo ya wanawake, hoja hii imetolewa na Mheshimiwa William Shellukindo, bwana. *(Makofi)*

Nakubaliana na Mheshimiwa Willliam Shellukindo kuwa elimu ya jinsia bado inaonekana kuwa ni masuala ya wanawake. Napenda kumfahamisha kuwa mafunzo ya elimu ya jinsia yanaendelea kutolewa katika ngazi mbalimbali wakiwemo waratibu wa dawati la jinsia ambao wapo katika Mikoa, Halmashauri na Maafisa Maendeleo nao wanaendelea kutoa elimu hiyo kwenye sehemu husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naomba niunge hoja hii mkono mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwanza kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja ambayo niliiwasilisha Bungeni leo asubuhi. *(makofi)*

Katika kuhitimisha kwanza nitumie fursa hii kumshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, kwa mchango wake mkubwa katika kujibu hoja ambazo zinahusu maeneo mbalimbali na hivyo amenirahisishia kazi kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote walioshiriki katika mjadala huu kwa kuandika na kwa kauli. Kwa kweli haijawahi kutokea, ni Waheshimiwa wengi sana wameleta maoni yao, na hii inaonyesha ni jinsi gani mambo ya jinsia mnavyoyajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwatambue kwa majina Waheshimiwa Wabunge kumi ambao wamechangia mjadala kwa kuongea hapa Bungeni. Nao ni Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Zaynab Vullu na Mheshimiwa George Simbachawene. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwatambua Waheshimiwa Wabunge 58 ambao wamechangia kwa maandishi nao ni kama ifuatavyo, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili, Mheshimiwa Mtutura Mtutura, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Sevelina Mwijage, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Jacob Shibiliti. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Eliatta Switi, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Castor Ligalama, Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Margaret Mkanga, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Capt. George Mkuchika na Mheshimiwa Devota Likokola. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Sigfrid Ng'itu, Mheshimiwa Fatma Abdalla Tamim na mwisho Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Nilifikiri umenisahau!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge 15 ambao walichangia kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nao ni kama ifuatavyo, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Stella Manyanya na Mheshimiwa Bahati Ali Abeid. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Meryce Emmnauel, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Florance Kyendesya, Mheshimiwa Anastazia Wambura na Mheshimiwa Lucy Mayenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri na michango mingi ya hiyo, ambao wamezungumza ni ushauri na changamoto ambazo tumezipokea na tunaahidi kuzifanyia kazi kikamilifu na tutawaandikia kila Mbunge aliyechangia ili aweze kuona tunavyoshughulikia jambo alilolizungumza. Tutafanya hivyo, kwa sababu ni wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwatambua wote waliochangia sasa kabla ya kujibu hoja ambazo zimejitokeza, napenda niseme mambo machache ya jumla. Napenda niseme kuwa masuala ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni masuala mtambuka, hivyo shughuli zake hutekelezwa na Wizara mbalimbali kwa mashirikiano ya karibu sana. Kwa mfano masuala ya watoto ni masuala ambayo yanashughulikiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara karibu zote pamoja na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Hii imepelekea masuala mengi ya Wizara ambayo yamezungumzwa hapa mengine mengi ni ya Wizara yanayohusika na Wizara nyingine moja kwa moja lakini kwa vile Serikali ni moja nimejitahidi kwa uwezo wangu kuyajibu masuala ambayo yamekuja mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika Ibara ya 11 ya hotuba yangu, Serikali imekubali kutekeleza mapendekezo ya kuimarisha sekta ya Maendeleo ya Jamii ili iweze kuchangia kikamilifu katika kuboresha maisha ya Watanzania. Mapendekezo hayo yanahusu kuimarisha Idara ya Maendeleo ya Jamii, kuongeza idadi ya watumishi wa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri, watumishi wa vyuo na kuwapatia vitendea kazi vyote muhimu zikiwemo vyombo vya usafiri na nyenzo nyingine za kufanyia kazi. Maeneo mengine ni kukarabati na ujenzi wa majengo ya vyuo vilivyo chini ya Wizara, kuimarisha vikosi vya ujenzi na mafunzo ya ufundi. Kukubalika kwa waraka huo, kunaonyesha dhamira thabiti ya Serikali ya kutaka kazi ya Wizara hii iimarike.

Kuhusu suala la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kujenga vyuo vya ufundi katika kila Wilaya na matumizi ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 58 vilivyo chini ya

Wizara yangu, tutakaa pamoja na mwenzangu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na kupanga jinsi ya kutekeleza azma hiyo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni la usawa wa kijinsia, hili si suala la Serikali peke yake bali ni suala la jamii ya Tanzania kwa ujumla. Tutakapolielewa suala hili na kulizingatia katika maisha yetu hakutakuwa na jinsia moja kunyanyasa jinsia nyingine. Kutakuwepo na mgawanyo mzuri wa kazi na mapato yatokanayo na kazi hizo. Hakutakuwa na mauaji ya wanawake wakongwe, kurithi wajane na kubaka. Hapa ningependa nimnukuu Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati alizungumza hivi kuhusu mwanamke. Alisema, nanukuu: "Huwezi kupata pepo kama hujaunyanyua unyayo wa mwanamke na kuubusu." Kwa hivyo, Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wangu anazungumzia kumuenzi mwanamke. Utakapomuenzi mwanamke basi usawa wa kijinsia utakuwepo dhahiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyo Makamu Mwenyekiti wangu ni Mheshimiwa Haroub Said Masoud, hiyo nukuu imetoka kwa Mheshimiwa Haroub Said Masoud leo asubuhi aliitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa ufafanuzi wa hoja za Waheshimiwa Wabunge katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la kuboresha Sekta ya Maendeleo ya Jamii. Suala hili limezungumziwa na Waheshimiwa wengi ikianzia na Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Capt. George Mkuchika, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na Mheshimiwa Maria Hewa.

Ninazungumzia kuongeza jitihada ya kupata fedha ya kutekeleza mapendekezo ya kuimarisha sekta ya maendeleo ya jamii. Wizara inakubaliana na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu kuwaelimisha wadau mbalimbali kuhusiana na mapendekezo ya Serikali ya kuimarisha sekta ya maendeleo ya jamii kwa madhumuni ya kupata rasilimali na kutekeleza mapendekezo hayo. Wizara imeshaandaa mkakati utakaowasilishwa kwa wafadhili kwa madhumuni ya kupata fedha za kutekeleza baadhi ya mapendezo. Hali kadhalika Wizara imeshaandaa sehemu yake ya programu ya maboresho ya elimu nchini kwa madhumuni ya kupata fedha za kuboresha majengo, miundombinu na huduma mbalimbali katika vyuo vya maendeleo ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiaw Naibu Spika, vivyo hivyo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI itaendelea kuzihamasisha Halmashauri kuongeza watumishi wa kada ya maendeleo ya jamii ili kukidhi mahitaji ya kuwa na watumishi walau mmoja kwa kila kata na kufufua matumizi ya majumba ya maendeleo.

Hoja nyingine ambayo ilitolewa na Kamati ya Maendeleo ya Jamii ni kuhusu kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya kisasa. Wizara inakubaliana na Kamati kuwa pale teknolojia ya kisasa zinapotumika zinasaidia sana kupunguza ugumu wa kazi hususan kwa upande wa wanawake na kwa kuwa wanaume watashiriki katika kugawa

baadhi ya kazi za wanawake. Wizara inaendelea kutafuta fedha za kuhamasisha na usambazaji wa teknolojia sahihi ambazo nyingi ziko katika kitita cha teknolojia sahihi ambacho kimetolewa na Wizara miaka miwili iliyopita. Katika mwaka wa 2007/2008 Wizara imetenga kiasi kidogo kwa madhumuni hayo, imetenga shilingi milioni 50 kwa madhumuni ya kusambaza teknolojia na kufundisha teknolojia rahisi. *(Makofi)*

Kamati ya Bunge pia ilizungumzia umuhimu wa wataalamu wa maendeleo ya jamii ambapo Mheshimiwa Beatrice Shellukindo naye amezungumzia kwa maandishi na pia amezungumzia kwa kutamka hapa Bungeni. Serikali inatambua umuhimu wa wataalamu wa maendeleo ya jamii katika jitihada zake za kuboresha maisha ya Watanzania na katika kufanikisha kufikia kwa sekta mbalimbali za kiuchumi na za kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa kuzingatia hilo Serikali imekubali kutekeleza mapendekezo ya kuimarisha sekta ya maendeleo ya jamii kwa kuzingatia uwezo wake kibajeti. Aidha, nawaomba Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuzihamasisha Halmashauri kuhusu utekelezaji wa mapendekezo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Rosemary Kirigini na Mheshimiwa Paul Kimiti, walizungumzia kuwa Wizara iendelee na juhudi za kuunganisha Chuo cha Tengeru na Chuo cha Mzumbe kwa madhumuni ya kuondoa tatizo la upungufu wa wakufunzi katika Chuo cha Tengeru. Wizara yangu itazingatia ushauri wa Kamati wa kuendeleza juhudi za kuunganisha *affliate* Chuo cha Tengeru na Chuo Kikuu cha Mzumbe kwa madhumuni ya kuondoa tatizo la upungufu wa wakufunzi katika Chuo cha Tengeru. Aidha, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kusomea chuoni kwa kuendelea na ukarabati na ujenzi wa majengo mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati ya Maendeleo ya Jamii imezungumzia umuhimu wa vikosi vya ujenzi na mafunzo ya ufundi. Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mbunge wa Tumbe naye pia amezungumzia juu ya umuhimu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vikosi vya ujenzi na mafunzo ya ufundi ni sehemu muhimu ya sekta ya maendeleo ya jamii na vimezingatiwa katika mapendekezo ya kuboresha sekta. Vikosi hivyo vitaendelea kuimarishwa kadri Serikali itakavyopata uwezo wa kibajeti. Hata hivyo vikosi hivi havikuanzishwa kwa madhumuni ya kufanya kazi ya ukandarasi. Vikosi hivi vilianzishwa mwaka 1962 kwa madhumuni ya kuchangia kiufundi katika kazi za kujitegemea za wananchi wenyewe kama vile ujenzi wa madarasa, zahanati, barabara za vijijini na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili kupata wataalamu wengi wa maendeleo ya jamii, hayo yamezungumzwa na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum. Wizara inakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kuongeza idadi ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili kuweza kupata wataalamu wa kutosha wa kada ya maendeleo ya jamii. Katika juhudi ya kutekeleza hilo Wizara imedhamiria kuteua vyuo vitatu kutokana na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili viweze kutoa mafunzo ya Cheti cha Awali na Cheti cha

Maendeleo ya Jamii. Pia Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI itaendelea kuzihamasisha Halmashauri kuajiri watumishi wa kada ya maendeleo ya jamii ili kukidhi mahitaji kufikia ngazi ya kata na hatimaye kijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii unaendelea kuzungumzwa kwani Mheshimiwa Jacob Shibiliti naye anazungumzia Chuo cha Misungwi. Ningependa kumjibu kuwa Wizara inakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge kuhusu umuhimu wa kukamilisha ukarabati wa majengo machache yaliyobakia, kwa vile tumekarabati kwa sehemu kubwa Chuo cha Misungwi na mimi pia niliwahi kutembelea chuo hicho, lakini kwa mwaka wa fedha 2006 Wizara ilitenga kiasi cha shilingi milioni 30 kukamilisha ukarabati wa baadhi ya majengo. Pia kwa mwaka huu wa fedha Wizara imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa samani wa chuo hicho. *(Makofi)*

Kuhusu Chuo cha Buhare kufanyiwa ukarabati na matengenezo ya majengo na kujengewa uzio. Mheshimiwa Rosemary Kirigini amezungumzia hilo. Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhare kilitengewa shilingi milioni 180 kwa ajili ya ukarabati wa baadhi ya majengo ya chuo kwa fedha ya mwaka 2006/2007. Kutokana na ufinyu wa Bajeti Wizara, Uongozi wa Chuo uliagizwa kupanda miti kuzunguka eneo la chuo hadi fedha za kujengea chuo uzio zitakapopatikana. Wizara inatambua uchache wa wakufunzi uliopo Chuoni Buhare na kwa mwaka huu wa fedha chuo kitaongezewa wakufunzi sita. Aidha Chuo cha Buhare kitapatiwa gari mara tu fedha zitakapopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mbunge wa Kilindi, ilizungumzia kuhusu idadi ya wahitimu Chuoni Tengeru kuwa pungufu ikilinganishwa na waliodahiliwa na pia ametoa mwaliko wa kutembelea jimbo la Kilindi. Nijibu tu kwanza kwamba nitatembelea kabla ya mwaka huu kumalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu idadi pungufu ya wanaodahiliwa, upungufu wa wahitimu katika Chuo cha Tengeru unatokana na sababu kuu zifuatazo, uwezo mdogo wa kitaaluma wa wanachuo hasa wale wanaodahiliwa kutoka kazini 60% huwa tunawatoa kutoka kwa wale ambao wana vyetu wafanyakazi wa Halmashauri kwa hiyo, hawa wanakuwa na uwezo mdogo na waliokaa muda mrefu toka kuhitimu kwao, wamekuwa wanakaa muda mrefu na cheti kwa hiyo, uwezo wao unakuwa mdogo sana. Kuahirisha kwa hiari masomo kutokana na matatizo mbalimbali Wizara itaendelea kutembelea Wilaya mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Kilindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nikiwa katika vyuo vya wananchi naona hivi vimezungumzwa sana hasa katika masuala ya uchakavu wa majengo na miundombinu ya vyuoni, pia uchakavu wa thamani na upungufu wa vitendea kazi. Hayo yamezungumzwa na Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Yono Kivela, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Capt. George Mkuchika, Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Maria Hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu tu kwamba nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kuwa hali ya vyuo vingi ni mbaya na ina matatizo mengi, mimi mwenyewe nimeshuhudia vina hali mbaya kwa kweli, hivyo Wizara yangu inayo mkakati wa kuviimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa kuvipatia fedha za ukarabati wa majengo na miundombinu pamoja na uendeshaji kutokana na fedha zinazotolewa kulingana na Bajeti ya kila mwaka ili kuboresha mazingira ya kufundishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Vyuo 10 vimefanyiwa ukarabati na kati ya hivyo vyuo vitatu vimewekewa umeme wa nguvu za jua. Kwa mwaka 2007/2008 vyuo 22 vitafanyiwa ukarabati kwa kumalizia vilivyokwishaanza vikiwemo vyuo vya Buhangija na Ndembo, Chisalu na Malampaka. Aidha, Vyuo vya Chala, Chilala, Chisalu, Sengerema, Kiwanda, Sofi, Kalumo, Msanginya na Muhukulu vimepatiwa pikipiki mwaka huu. Wizara imetenga fedha za ukarabati wa vyombo vya usafiri vyuoni kwa mwaka 2007/2008 na Chuo cha Chisalu ni kimojawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza alizungumzia kuhusu *water rights* ambazo tumepata barua yake kwamba yupo mfadhili anataka kuwasaidia kuweka maji katika chuo chao kwa hiyo, mimi ningependa kumjibu tu kwamba Wizara yangu itafuatilia kwa karibu upatikanaji wa *water rights* ili kuwezesha Chuo cha Kiwanda kupata umeme kutoka Mto Zigi aidha, utaratibu wa kupeleka *satellite dish* vyuoni utaendelea kila mwaka ili kuwezesha *station* kuonekana vizuri.

Mheshimiwa William Ngeleja ningependa kumjibu kwamba vile vile vyuo vya Sengerema na Karuma Wilayani Sengerema bado vinamilikiwa na Wizara yangu na vinaendelea kuhudumiwa kwa kadri ya upatikanaji wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa wakufunzi vyuoni, Mheshimiwa Felix Kijiko aliuliza hilo, Wizara yangu inatambua upungufu mkubwa wa wakufunzi uliopo vyuoni aidha, Wizara inaendelea kuimarisha vyuo hivyo kwa kuomba kibali cha ajira kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa mwaka huu watumishi 98 wameajiriwa na kupangiwa vituo mbalimbali vya kazi vyuoni.

Mheshimiwa Yono Kevela, anazungumzia kupanua kozi na kuongeza mafunzo ya udereva na umakenika, kuhusu upanuzi wa kozi ya mafunzo ya udereva na umakenika ni jukumu la chuo chenyewe kutokana na mahitaji yaliyopo katika jamii, Wizara imeandaa vitini vya kufundishia na kupelekwa vyuoni ili kuvisaidia vyuo kubuni na kuimarisha mafunzo kufuatana na uhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalifan na Mheshimiwa Anastazia Wambura walizungumzia kuwa kuanzishwa vyuo vya *VETA* kila Wilaya ni mzigo kwa Serikali ni vema kuboresha na kuimarisha vyuo vya maendeleo ya wananchi vilivyopo kila mkoa na Wilaya 58 ili vitumike kwa vile kimsingi vinalingana majukumu, naungana na Waheshimiwa Wabunge kuwa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vinahitaji kuimarishwa badala ya kujengwa vyuo vipya vya *VETA* kila Wilaya. Chini ya programu ya sekta ya elimu upo utaratibu wa kuratibu kazi na mipango ya

sehemu za sekta hiyo kupitia kamati ya ushauri ya uendeshaji na sehemu hizo ni *basic education* inayohusisha elimu ya msingi, *treasury education* inayohusisha elimu ya juu na *vocational and focus education* ambayo inajumuisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kufufua vyuo na kuwezesha wahitimu kujitengenezea vitendea kazi, hii imeulizwa na Mheshimiwa Lucy Owenya na Mheshimiwa Eliatta Switi, Wizara inakubaliana na Waheshimiwa Wabunge juu ya ushauri huo, suala hili limo katika mapendekezo ya kuimarisha sekta ya maendeleo ya jamii ambalo imepitishwa na Baraza la Mawaziri. Aidha, katika programu ya kuimarisha sekta ya elimu nchini upo utaratibu wa kuviimarisha vyuo hivi kupitia programu ndogo inayohusu *vocational and focus education sub sector*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, aliulizia suala lililopo katika ukurasa namba 51 kuhusu wanafunzi wanaosajiliwa kuwa wengi na wanaodahiliwa wachache nadhani hilo nimeshakujibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niingie kwenye suala ambalo limezungumziwa na Waheshimiwa wengi nalo linahusu watoto, suala la watoto kama nilivyosema ni suala mtambuka na nitajaribu kulijibu suala hili kwa jinsi nitakavyoweza pamoja na kwamba masuala mengine yaliyoulizwa moja kwa moja ni masuala ya Wizara ya Katiba na Sheria na mengine ni ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii lakini kwa vile Serikali ni moja nitaweza kuyajibu. *(Makofi)*

Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ilizungumzia Wizara kuandaa mikakati ya kutosha kuunganisha juhudi za kuwahudumia watoto. Wajibu wa Wizara yangu ni kuandaa sera, mkakati wa utekelezaji wa sera, programu ya miongozo inayohusu watoto. Aidha, watoto wanashughulikiwa na sekta na Wizara mbalimbali kama nilivyozitaja hapo mwanzo. Kamati ya Maendeleo ya Jamii pia ilizungumzia kuhusu suala la wanaume waelimishwe kuhusu tatizo la ukeketaji na adhabu kali itolewe kwa wanapatikana na hatia ya kuwakeketa watoto wadogo kama kifungo cha maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hili limezungumzwa kwa uchungu sana karibu na Waheshimiwa Wabunge wote waliozungumza. Niseme tu kwamba Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto imepanga kutoa mafunzo kwa Wabunge na wasimamizi wa sheria wakiwemo wanaume na wanawake kuhusu madhara ya ukeketaji na mbinu za kutokomeza mila hiyo.

Aidha, kwa kupitia maafisa mendeleo ya jamii waliopo kwenye Wilaya, Kata na Vijiji inahamasishwa kuondokana na mila hiyo ya ukeketaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Wizara imetoa mafunzo kama hayo kwa wasimamizi na watekelezaji wa sheria *royal enforces* Kamati ya Bunge ilizungumzia hilo lakini Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir na Mheshimiwa Maria Hewa, wote walizungumzia suala hilo na nashukuru Mheshimiwa

Maria Hewa alizungumzia kuhusu mbinu mpya ya kukeketa watoto tumepata taarifa hiyo na tunaifanyia kazi, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningependa niseme tu kwamba sheria peke yake zitashindwa kufanya kazi kwa sababu tuna sheria ya makosa ya kujamiana ya mwaka 1998 lakini inabidi jamii ibadilike, sisi sote tuwe mstari wa mbele kuhamasisha jamii kujua madhara ya suala hili la ukeketaji na tukumbuke kwamba ukeketaji unafanywa katika hali ya usiri mkubwa kwa hiyo, tunahitaji jamii yote ione madhara yake ili tuweze kuwatambua wale ambao wanaendelea na tatizo hilo. Mikakati maalumu iandaliwe ya kuwalinda watoto wadogo dhidi ya ukeketaji, Kamati ya Maendeleo ya Jamii imezungumzia hilo, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha amezungumzia hilo na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar amezungumzia na karibu atoe machozi katika suala hili, namwambia kwamba ni kweli lazima tufunge mikanda tulishughulikie kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Maendeleo ya Jamii na Mheshimiwa kepteni George Mkuchika, alizungumzia kuhusu kuandaa Muswada wa Sheria ya Watoto na kuuleta Bungeni mapema. Nafurahi kumfahamisha kwamba Muswada wa Sheria ya Watoto kwa kweli umeshatayarishwa na uko chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na ninaamini katika kipindi cha muda si mrefu sheria hii itakuwa tayari italetwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Suala la vituo vya kulelea watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira hatarishi limezungumziwa na Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, limezungumziwa pia na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar na Mheshimiwa Lucy Owenya wote wamezungumzia suala la vituo vya kulelea watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia sera tuliyonayo watoto wanatakiwa kulelewa katika jamii na siyo kwenye vituo, kupeleka watoto kwenye vituo iwe ni hatua ya mwisho hata hivyo Serikali kwa kushirikiana na wadau inaandaa mfuko wa watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi ili kuweza kuwasaidia, uanzishwaji wa mfuko utawezesha watoto hawa kupata mahitaji yao muhimu kama vile elimu, chakula, mavazi aidha, pale itakavyowezekana vituo vya kulelea watoto vitaanzishwa katika asasi mbalimbali zinazoshughulikia watoto. Vile vile Serikali imeweka utaratibu wa usajili na ufuatiliaji wa vituo hivyo chini ya Sheria ya Makao namba nne ya mwaka 1968 inayosimamiwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa ni vitendo vibaya vya wasichana wanaotupa watoto mara baada ya kuzaa kitendo ambacho ni chanzo cha ongezeko la watoto yatima na watoto wa mitaani, lakini hapo hapo amezungumzia kwa kusema wasichana hao warudishwe shuleni mara baada ya kujifungua na adhabu kali itolewe kwa wasichana wanaofanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yamezungumziwa na Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwaga, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed

pia na Mheshimiwa Faid Mohamed Bakar amelinzungumzia hilo kwa uchungu sana, tatizo hili ni la kijamii hivyo nashauri kila mmoja wetu azidi kuhamasisha jamii kukemea vitenda hivyo. Aidha, wasichana na wanaoshawishi wasichana kutenda vitendo hivyo watakapopatikana wataadhibiwa kulingana na sheria za nchi.

Kuhusu kuwarudisha shuleni wale waliozaa, Serikali inaandaa utaratibu wa kulishughulikia suala hili ili wasichana hao waweze kurudishwa shuleni. Mtakumbuka Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, alilizungumzia vizuri sana suala hili la wasichana wanaopata mimba na mjadala unaendelea kwa sababu hili ni suala la kijamii, ni lazima tupate maoni kutoka sehemu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Wizara yangu bado inasema elimu ni haki ya watoto wote wakiwemo watoto wa kike, hata yule aliyepata mimba kutokana na mkataba ambao tumesaini ni haki ya watoto wote kupata elimu, kwa hiyo, ni jukumu la wazazi na sisi kufikiria ni kwa vipi tunaweza tukawarudisha hawa watoto mashuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Felix Kijiko alisema ni jukumu la Wizara kuhakikisha kuwa walaemavu wanaoteseka karibu nchi nzima wanapata huduma muhimu ambayo wanatakiwa kupatiwa kutoka Serikalini. Masuala yanayohusu watu wenye ulemavu yanashughulikiwa na Wizara zaidi ya moja kwa kuzingatia aina ya tukio. Kuhusu suala hili Wizara italishughulikia katika Wizara inayohusika kwa maelezo zaidi nitashukuru kama Mheshimiwa Felix Kijiko tutaonana baadaye ili nimpe maelezo mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itoe takwimu kuonyesha ukubwa tatizo la watoto yatima, hayo yamesemwa na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mbunge wa Singida. Niseme tu kwamba mpaka sasa inakadiriwa kuwa wapo watoto milioni 2.5 wanaoishi katika mazingira hatarishi na ndani yao wamo watoto yatima. Hata hivyo Serikali ikishirikiana na wadau mbalimbali inaendelea na mchakato wa kufanya uchambuzi na utambuzi wa watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi ambapo hivi sasa uchambuzi na utambuzi watoto hao umefanyika katika Wilaya 39.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vikundi vya watoto wanaoishi katika mazingira magumu visaidiwe kwa nguzo za kiufundi na taaluma nyingine, Tawi la *KIWOHEDE* lilichopo Kihomboi, Jimboni Iramba lipewe nyenzo kwani linafanya vizuril hayo yamesemwa na Mheshimiwa Juma Killimbah.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia programu mbalimbali imekuwa ikitoa elimu ya ufundi kwa watoto walio katika mazingira magumu, vyuo vyetu karibu vyote vinavyoendesha mafunzo ya ufundi vinawachukua watoto yatima na wanasoma bure huko. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inatekeleza pia programu maalumu ya kutokomeza utumikishwaji wa watoto katika kazi za hatari. Aidha, Wizara itaendelea kuwasiliana na *KIWOHEDE* ili kuona ni namna gani tunaweza kuona mahitaji ya nyenzo kwa malengo ya kuwasaidia *KIWOHEDE* waliopo Singida. Kuhusu watoto wa mitaani kuwa ndio nguvukazi na Taifa la kesho, hayo yamezungumzwa na Mheshimiwa Nuru

Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa mkakati wa Kitaifa kuhusu malezi, huduma na ulinzi wa watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi ambao kwa ujumla wake inaelekeza pamoja na mambo mengine kuwajengea watoto hao malezi bora katika shughuli za kujitegemea. Mheshimiwa Savelina Mwijage wa Viti Maalum alitaka kujua kwa nini Wizara haitembelei Kagera kwani yapo mambo mengi. Napenda kumfahamisha kwamba tulishatembelea Kagera na tumejionea mambo mengi na tutakapopata nafasi tutaenda tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya amezungumzia je, Serikali ina mkakati gani ili makundi haya ya watoto walemavu yafaidike kutoka Serikalini na Wizara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikishirikiana na wadau inaandaa mikakati mbalimbali ikiwemo kuanzisha mfuko wa kusaidia watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi. Madhumuni ya mfuko ni kuhakikisha watoto hao wanapatiwa mahitaji ya msingi kwa maisha yao.

Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis alishauri kwamba watoto wapewe elimu, malezi na huduma zote za lazima hii nadhani nimeshajibu, Mheshimiwa Castor Ligallama alizungumzia mabadiliko ya sheria ya matunzo ya mtoto. Napenda kumjibu kwamba Serikali inaendelea kufanya marekebisho ya sheria zinazohusu ndoa, haki na malezi ya watoto, aidha, inaandaa masuala ya sheria ya watoto kutokana na ukweli kwamba sheria hizo za watoto zilizopo zilikuwa zimepitwa na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaamini wengine wataniuliza baadaye, naomba kutoa hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa uamuzi wake mpaka tuingie kwenye hatua inayofuata.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 53 – Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

Kifungu 1001 – *Administration and General* ... ... ...Shs. 1,153,241,200/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Adam Malima ndio niliowaona, tutaanza na Mheshimiwa Adam Malima.

**MHE. ADAM K.A. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, programu namba 10, *vote 53 sub vote 1001 250100* mshahara wa Waziri. Katika kuwasilisha masuala niliyompelekea Waziri mchana nilizungumzia masuala ya sera kama ambavyo umekuwa unatuagiza tufanye katika kifungu hiki, kuna suala moja ambalo nimeomba nipate ufafanuzi na nadhani kwa sababu ya muda hakupata muda wa kunijibu, nilikuwa nimemuomba kwa kutambua namna ya masuala ya mtambuka wa masuala yake ya Wizara yake, nilikuwa nimeomba Waziri anipe majibu ya tathmini ya kitaalamu ambayo nimemuomba ifanywe kwa kushirikiana na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, ili kutathmini michango ya jamii za kina mama katika uchumi wa Watanzania haswa tukizingatia kwamba akinamama ni asilimia 51 ya *population* yetu, lakini pili kuna taarifa ya wataalamu inayosema kwamba kwa Afrika yetu asilimia 80 ya chakula kinachozalishwa kinazalishwa na akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimemuomba Waziri aniambie haswa katika suala la utekelezaji wa sera kwamba kuna suala la akina baba kwenye baadhi ya jamii zetu na kuna wengine majimbo yao humu Waheshimiwa Wabunge ndugu zangu sipendi kuwataja lakini kina baba wanakusanyika saa nne asubuhi wanapata kilaji. Huko nyumbani kuna mtu ambaye anafanya kazi, analea watoto na wanazidi kudumaza mchango wa akinamama na uwezo wa akinamama kufanya kazi za maendeleo yake binafsi, nilikuwa nimemuomba Waziri badala ya kutupa maelezo ya kwamba tunafanya mikakati, nilikuwa nimemuomba kama anaweza akatupa *specific time* ya kwamba labda kwenye Bunge lijalo atakuja na mapendekezo ya kisheria ya kushughulikia suala hili. Lakini lingine ...

**MWENYEKITI:** Kilaji gani hicho?

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kilaji ni kinywaji yaani kilevi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la haki za watoto ambalo nilikuwa nimelizungumzia kwenye mchango wangu na Naibu Waziri amejaribu kunijibu kidogo lakini katika jibu lake Mheshimiwa Naibu Waziri amesema suala hili linagusa haki za mtu kwa hiyo, inabidi tuwe waangalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala kubwa zaidi ambalo mimi naliona ni haki za mtoto ambazo kusema kweli kwangu mimi kama Mbunge haki za mtoto zina kipaumbele kuliko haki za mhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia haya nilikuwa naomba nirejee kwenye kifungu namba 72 cha hotuba ya Waziri kinasema hivi; "Kumekuwepo na wimbi la ongezeko la vitendo viovu vya ukatili, unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto katika familia na jamii." Hapo hapo kwenye hotuba yake

Mheshimiwa Waziri amesema; “Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria itaendelea kupitia sheria mbalimbali ili kuzirekebisha zile zinazowanyima wakawake haki na watoto na kadhalika.“

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu nilikuwa nimemuomba Mheshimiwa Waziri katika mchango kwamba aniambie inawezekana kwamba tuna matatizo ya kisheria kwenye suala la mimba za watoto na ndio maana hata Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja kwangu alikuta tuna kesi za mimba 50 kwa mwaka ule uliopita na kwa mwaka huu tayari tuna mimba 20 kwa Mkuranga tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Adam Malima, kwa kutambua mchango mkubwa wa wanawake katika Taifa letu, namshukuru kwamba amepata hizo taarifa za kusema mwanamke anazalisha asilimia 80 ya chakula ambacho kinaliwa Afrika lakini pia mwanamke huyo anamiliki asilimia 20 ya ardhi ambayo inalimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kumjibu swali lake, mimi napenda kumjibu kwamba mpaka sasa hapakuwa na tafiti zozote zilizokuwa zimefanyika kuhusu mchango wa wanawake katika Pato la Taifa. Hata hivyo upo utafiti ambao unaendelea kufanyika ujulikanao kama *Time Used Survey*, utafiti huu unaendeshwa na *National Budget Survey* kwa kushirikiana na *TGNP*. Masuala yanayoshughulikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya mchango wa wanawake wa *non monitory income activities* na jinsi zinavyochangia katika Pato la Taifa, utafiti huo kwa sasa uko kwenye ngazi ya uchambuzi wa takwimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu haki za mtoto na sheria mbalimbali kama nilivyosema katika hotuba yangu ni kweli sheria hizi zipo katika hatua nzuri na kwetu sisi zilishatoka na Wizara ya Katiba na Sheria imeahidi kwamba mpaka itakapofika mwanzoni mwa mwaka ujao sheria hizi zitakuwepo ikiwemo moja ambayo tumeitunga *specific* kwa ajili ya watoto. Kutokana na wimbi la vitendo viovu dhidi ya watoto ni kweli pamoja na sheria ngumu ambayo tunatunga bado jamii inatakiwa iwajibike kujua kwamba hivi vitendo ni viovu hata tukitungaje sheria bado, sisi kama Wabunge tuna kazi ya ziada kuhamasisha wananchi na kuelimisha kuhusu madhara ya vitendo hivi viovu. Ahsante.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 53 program 10 sub vote 1001,* kifungu kidogo 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi tu wakati Naibu Waziri akijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge aligusia suala la ajira la Maafisa Maendeleo ya Jamii kwamba wanatakiwa waajiriwe na Halmashauri zao. Halmashauri nyingi hazina uwezo wa kulipa watu wanaotegemewa sana katika maeneo yetu katika Halmashauri zetu, sijui Mheshimiwa Waziri atakuja na mkakati gani wa kuhakikisha hawa watu waajiriwe kutoka kwenye Wizara yake moja kwa moja ili waweze kuwajibika vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba katika kujibu hoja zake amezungumzia suala la mikopo, mifuko ambayo imeidhinishwa kisheria kwamba wanawake wakopeshwe asilimia 10 kutoka kwenye Halmashauri za Wilaya, lakini bahati mbaya sana Halmashauri nyingi hazina uwezo hazikuweza kutenga mafungu kama haya kwa ajili ya kuwakopesha akina mama na vijana, je, Waziri atanieleza wana mikakati gani kuhakikisha Halmashauri hizi zinahakikisha fedha hizi zinatengwa kuhakikisha akina mama na vijana wanapatiwa mikopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho ni kwamba Mheshimiwa Maria Hewa, amezungumzia sana suala ambalo limeonekana katika kituo chetu cha watoto pale Mwanza cha Kuleana. Watoto wale wameonekana kwenye TVT wanalia, wanahitaji elimu wapatiwe. Kama Wizara kuwanusuru hawa watoto na walikuwa wamelelewa katika kituo kile na hatimaye sasa mwenyewe amewaachia tu hivi hivi na watoto wanataka elimu. Je, Waziri atanisaidia vipi watoto hawa waliopo katika kituo hiki cha Mwanza angalau basi hata kama sisi Wabunge tulichangia hapa michezo, je, hatuwezi tena kuchangia watoto kama hawa wanaopata matatizo kama hayo ili wapate fungu la kuwapeleka katika maeneo ya shule ili wapate elimu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi tafadhali.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Esther Nyawazwa, kwa swali lake zuri ambalo litasaidia kuelewa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira za Maafisa Maendeleo ya Jamii, sisi kazi yetu kubwa ni kuwasomesha yaani kutoa elimu na tunawafuatilia shughuli zao. Lakini ajira yao kila Halmashauri ndiyo inaajiri Maafisa wa Maendeleo ya Jamii na hakuna suala hapa la kusema kwamba Halmashauri haina uwezo, isipokuwa Halmashauri inaomba Idara Kuu ya Utumishi kibali cha kuajiri kama wanavyoajiriwa Maafisa wengine.

Sasa namshauri sana Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine wakiwa katika Halmashauri zao wawahimize Wakurugenzi waajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii ili kila Kata iwe na Afisa Maendeleo ya Jamii ambaye Afisa Maendeleo ya Jamii ndiyo *characteristic* katika jamii, yeye ndiye anahamasisha elimu, kilimo na kadhalika, yeye Afisa Maendeleo ya Jamii ndiye anayeweza kuhamasisha wananchi kubadilisha miundo yao ya zamani kuwa mambo ya kisasa ambayo maendeleo ya jamii wanafundishwa na wao katika Halmashauri sisi tunaandaa mafunzo yao tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu kutenga mafungu ya *WDF.* Ni kweli sisi kama Wizara tunatoa kiwango kidogo lakini tunahitaji Halmashauri itoe 5% na sisi tunatoa vile vile. Kwa hiyo, Wabunge ni Wajumbe katika Halmashauri, sasa mimi siwezi kuwa na mkakati wa kulazimisha zile Halmashauri wakati sisi Waheshimiwa Wabunge tupo jikoni mle mle. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuhakikishe kwamba Halmashauri zetu zinatenga fungu hili kwa ajili ya kukopesha akina mama. Lakini tukumbuke kwamba benki inakuja hawa akina mama, watakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kuwekeza kwa hiyo, wale akina mama kama wakiweza kukopeshwa katika vikundi vyao

na wao pia wanaweza kununua hisa na hivyo pia watakuwa wawekezaji wakubwa katika benki yetu. Kwa hiyo, naomba sana muhamasishe Halmashauri zikubali kutenga fungu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kituo cha Kuleana, watoto wanalilia elimu. Mimi nasikitika sana kuona kwamba kuna watu wanaweka watoto vituoni na wanashindwa kuwalea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NGOs* zote zinatakiwa ziwe na mpango wa kujiletea faida na faida hizo ndizo zitakazowawezesha kuwalea wale watoto. Katika mwaka unaofuata Idara yangu ya *NGO* inatarajia kuendesha mafunzo ili kuwaelimisha wale ambao wanaanzisha vituo au wanaanzisha *NGO* wasiwe wanategemea tu wafadhili kwa sababu hii inaonyesha wafadhili walianza na baadaye wakaondoka hawa watoto wamebakia hawana la kufanya lakini niseme tu elimu ni bure pengine wawe na matatizo mengine, isipokuwa kama ni elimu ya sekondari ni kitu kingine. Lakini hawa inaelekea ni watoto wadogo hapa katika kituo cha Kuleana, Mwanza, nadhani wakionana na Mheshimiwa Margaret Sitta, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ataweza kuwasaidia zaidi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Anna Maulidah Komu.

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi wakati nikitoa mchango wangu, *Vote 53, Programme 10, Sub Vote 1001,* Kifungu kidogo 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi nilipokuwa natoa mchango wangu niliomba kuambiwa kuhusu wanawake wanavyolalamika na kuomba wawe na chombo chao kinachowaunganisha kama Wanawake wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili nililileta hata mwaka jana hapa Bungeni na mwaka huu nimelirudisha tena kutokana na kilio cha wanawake, je, ninachokiomba na kutaka kukijua hii kesi ambayo ndiyo imekuwa kifungo cha kufuli kufunga wanawake wasio na chombo chao ina miaka mingapi sasa Mahakamani na je, kweli hii kesi ndiyo kisingizio cha kumfanya mwanamke asiwe na chombo chake kwa sababu kuna kesi iko Mahakamani? Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Anna Maulidah Komu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ambayo tumempatia ambayo yamejibiwa vizuri na Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi bado nasema kwamba chombo cha wanawake hata sisi wengi tunataka kiwepo lakini itakuwa vigumu kuanzisha chombo kingine cha wanawake wakati chombo kingine kilishaanzishwa kipo Mahakamani. Kwa

hiyo, kilichobaki tusubiri ile kesi iishe na tutaendelea na chombo cha wanawake ambacho tunakitaka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kuhusu toka lini kesi iko Mahakamani ni kwamba toka mimi nilipokuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto yaani toka mwaka 1995. Tunaendelea.

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado...

**MWENYEKITI:** Kuhusu nini?

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyosema kwamba kwanza hiyo kesi ina miaka chungu nzima hapo Mahakamani, Serikali sidhani kama inashindwa kuingilia kati kwenye kesi hiyo na kuuliza, mimi tatizo langu ni kwamba ina miaka mingapi na kesi hii itakwisha lini ili hawa wanawake wapate haki yao ya kuwa na chombo chao, basi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikijua tu ina miaka mingapi na hii kesi iko kwenye kiwango gani sasa hivi na itakwisha lini ili hawa wanawake wasikie kutoka Serikalini na Serikali inasema nini kuhusu wao wanavyotaka kuunda au kuanzishwa kwa chombo chao. Sina la ziada.

**MWENYEKITI :** Kuna kifungu hapa kinakataza kujadili mambo yaliyopo Mahakamani, natangaza sasa kwamba ni marufuku kuzungumza mambo yaliyopo Mahakamani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nimekwambia kesi hiyo ipo Mahakamani toka mimi nikiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto, sasa unaweza kufanya hesabu. Tunaendelea na Mheshimiwa Devota Likokola.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA :** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Vote 53, Programme 10, Sub vote 1001* Kifungu kidogo cha 250100, mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi wa masuala mawili madogo, kwa muda wa miaka miwili mfululizo sasa tumeshuhudia Siku ya Wanawake Duniani haisherehekewi Kitaifa na wakati huo huo siku nyingine zinasherehekewa Kitaifa kama vile Siku ya Wazee, Siku ya Watoto, Siku ya Familia, Siku ya Mazingira, Siku ya UKIMWI na Siku ya Dawa za Kulevya. Wanawake wengi wanategemewa kupata miongozo na mambo mengi katika siku hiyo ya Wanawake Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeuliza mara nyingi na tumepewa sababu kwamba Wizara haina pesa ya kusherehekea siku hiyo Kitaifa, lakini Wizara hiyo hiyo inasherehekea siku hizo Kitaifa kama Siku ya Watoto na Siku ya Familia. Hili linatokana na kukosa umuhimu wa Siku ya Wanawake Duniani au ni kwa sababu gani?

Swali la pili, napenda kupata ufafanuzi juu ya majibu ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa mengi hapa kutokana na kushindwa kutekelezeka kazi za Maendeleo ya Jamii kulingana na ufinyu wa Bajeti ya Wizara hii na Serikali imekuwa ikipanga vipaumbele na umuhimu wa mafungu katika Wizara mbalimbali, je ni kwa nini Wizara hii ina Bajeti finyu sana? Na kwa nini sasa wakati wa kupaga *cealing* ya Wizara hii Waziri anakuwa wapi kujenga hoja ili Wizara yake iwe na fedha za kutosha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devota Likokola, swali la mwisho hajibu, la kwanza atajibu. Yeye Mheshimiwa Waziri atasemaje? Unafikiri hapendi pesa? Mheshimiwa Waziri jibu la kwanza. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimjibu Mheshimiwa Devota Likokola, kuhusu Siku ya Wanawake Duniani. Ni kweli Siku ya Wanawake ni siku ya muhimu sana kwa sababu tunakumbusha masuala mengi yanayohusu wanawake na inasherehekewa dunia nzima.

Kwa Tanzania katika miaka hii ya karibuni siku hii inasherehekewa Kimkoa, ilikubalika na kuamuliwa kwamba iwe inasherehekewa Kitaifa mara moja katika miaka mitano, hii ni kutokana na gharama kubwa ambayo sherehe kubwa kama hii inagharimu na kama alivyoanza kwa kusema kwamba Wizara haina uwezo na ina Bajeti finyu na hiyo si kwa sababu tunapenda isipokuwa ni sababu ya hali ilivyo ya Bajeti zote, hakuna Bajeti ambayo inatosheleza. Lakini kwa hili katika kipindi hiki cha miaka mitano ni lazima tutakuwa na mwaka mmoja ambao ndiyo sikukuu hiyo itasherehekewa Kitaifa.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 *Finance and Account*... ... ... ... ... ... ... Shs.309,535,300/=
Kifungu 1003 *Policy and Planning* ..... ... ... ... ... ... ...Shs. 287,554,000/=
Kifungu 2001 *Training and Folk Dev. Colleges*... ...Shs.2,332,716,700/=
Kifungu 2002 *Community Development* ... .. ... ... ... Shs.1,266,756,300/=
Kifungu 2003 *Community Development*
*College - Tengeru*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Shs. 215,921,100/=
Kifungu 3001 *Gender Development* ... ... ...... ... ... ... Shs. 570,654,900/=
Kifungu 3002 *Children Development*... ... ... ... ... ... Shs.365,378,200/=
Kifungu 4001 *NGOs Coordination*... ... ... ... ... ... ... Shs. 239,853,300/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

Kifungu 1001 *Administration and General* ... . ... ... ...Shs. 882,900,000/=

Kifungu 1003 *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... .. Shs.120,000,000/=
Kifungu 2001 *Training and Folk Dev. Colleges*... ... Shs. 799,400,000/=
Kifungu 2002 *Community Development* ... ... ... ... ... ..Shs.738,600,000/=
Kifungu 2003 *Community Development*
*College – Tengeru*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Shs. 240,100,000/=
Kifungu 3001 *Gender Development* ... ... ... ... ... ... ... Shs.137,085,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy F. Owenya.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Vote 53,* Kifungu 3001, *Sub vote 6259*. Sitarudia hotuba ya Waziri kwa kuokoa muda, ukurasa wa 32 kifungu namba 63.

Nataka anipe ufafanuzi kwamba wanatoa mafunzo kwa kozi za jinsia za aina gani na wameshasomesha wangapi na kwa *level* ipi? Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Ni kile kifungu kinachohusu *Advocacy and Gender Development Programme.* Uliza tena!

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua kwamba wanatoa mafunzo ya kozi za jinsia za aina gani na vile vile wameshasomesha wanafunzi wangapi na kwa *level* ipi?

**MWENYEKITI:** Atasema aina ya kozi, lakini idadi ya wanafunzi, hapana. Mheshimiwa Waziri mnafundisha kozi za aina gani na kwa *level* gani, hiyo unaweza.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafundisha kozi mbalimbali kwenye vyuo vyetu na kwenye semina mbalimbali ambazo tunaendesha, masuala hayo pia yanahusiana na masuala ya haki za wanawake, mambo ya ukeketaji na masuala mengine.

Mheshhimiwa Mwenyekiti, utaona kwenye majedwali mwisho ukurasa namba 52 utaona kwamba tumekuwa tukitoa mafunzo kwa maafisa maendeleo ya jamii kwenye vyuo vyetu na wengine, ni kama *refresher course* kwa maafisa maendeleo ya jamii pote walipo kuhusu elimu inayohusu haki za mtoto, haki za Wanawake na masuala ya sheria mbalimbali kama *SOSPA* na mengine. Tumekuwa tukiendesha mafunzo katika Mikoa mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Nimekaa hesabu kwa sababu *advocacy* siyo lazima uwe na hesabu ndogo unaweza kuwa na watu wengi tu, ni *advocacy*.

Kifungu 3002 *Children Development*... ... ... ... ... ... ... Shs. 942,768,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima James Mdee.

**MHE. HALIMA JAMES MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Vote 53, Sub vote 3002*, Kifungu 4316 - *Basic Education and Life Skills Programme.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya ahadi ambazo Mheshimiwa Rais alikuwa akizitoa ilikuwa ni kusomesha watoto yatima bure wakiwemo watoto ambao wazazi wao wamefariki kwa UKIMWI. Sasa katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri anaonyesha kwamba kuna tafiti mbalimbali ambazo amezifanya na tayari matokeo anayo katika Wilaya 39 juu ya idadi ya watoto yatima.

Sasa ninataka Mheshimiwa Waziri aniambie kama hili fungu ambalo kifungu chake ambacho nimekitaja hapa ndicho ambacho kitatumika kufundisha hawa watoto na kama hakipo kifungu chao kiko wapi? Na kama Wizara yake ni mtambuka anashirikiana na Wizara nyingine atuambie ni watoto yatima kiasi gani wamesomeshwa au wanatarajia kusomeshwa ili kuweza kukidhi ile ahadi ya Mheshimiwa Rais. Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho anachozungumza ni kweli tunapata *funds* kutoka *UNICEF* ambazo zinashughulikia masuala ya watoto katika kuwaelimisha watoto na pia tunakuwa na semina zinaingia humo humo kuwa-*empower* wale ambao wanashughulikia masuala ya watoto kuhusu *life skills.*

**MWENYEKITI:** Bado swali lingine kwamba unashirikiana na Wizara ngapi na zipi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashirikiana na Wizara zinazohusiana na masuala ya watoto kama Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi hasa katika *Early Child Rule Development* na TAMISEMI na mambo mengine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumzia elimu sizungumzii semina, Mheshimiwa Waziri anajibu semina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa aniambie kama elimu halipo au Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inatoa hivyo au hiyo ilikuwa ni ahadi tu ambayo haitekelezeki? Naomba anijibu.

**MWENYEKITI:** Waziri wa Elimu ya Msingi anaweza kujibu. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika kujibu hoja ya Mheshimiwa Halima Mdee, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto hasa kupitia mipango ya MMEM, MEMKWA na hasa MMEM pia inaangalia

elimu ya awali na MEMKWA pia kwa watoto waliokosa elimu katika njia rasmi yaani mfumo rasmi. Kwa hiyo, tunashirikiana kwa kuelimisha watoto kwa namna hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nimsahihishe Mheshimiwa Mbunge kwamba nimesema tunatoa elimu na semina kwa sababu wale ambao wanatoa ile elimu lazima tukae nao waelekezwe jinsi ya kutoa hiyo elimu. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*
*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2007/2008 Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liyakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kesho tunaendelea na Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia tena ni siku moja.

Sasa wakati natoa uamuzi wangu kwenye Kamati ya Bunge Zima, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu alitaka kujua habari ya Baraza la Wanawake lililokuwa limeanzishwa na mimi nikamwambia maelezo yaliyotolewa na Wizara yanatosha na kwamba hatuwezi kujadili kwa sababu suala lenyewe liko Mahakamani na si vizuri kuanza kusema lini litakwisha ama Serikali iingilie Mahakamani, nadhani unajua kwamba ni lazima tuache Mahakama ifanye kazi zake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kifungu kinachotukataza sisi ni Kifungu cha 50 (3) ambacho kinasema; "Ni marufuku kwa Mbunge yeyote kuzungumzia jambo lolote ambalo linangoja uamuzi wa Mahakama, au jambo lolote ambalo linajadiliwa na Mkutano uliopo au uliotangulia." Sasa sisi tuwaachie kwenye Mahakama kama walishazungumza hutakiwi kurudia tena. Kwa hiyo, ndiyo sababu nimekuomba usidai zaidi kwa sababu lipo Mahakamani.

Baada ya kusema hivyo ninaahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01:45 Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa, Tarehe 20 Julai, 2007 saa tatu asubuhi)*